ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 19 Aprili, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na shughuli zetu ambazo zimo katika orodha ya shughuli za leo, naona na leo ukumbi wetu pale juu katika eneo la wageni tunao wageni wengi. Wageni waliopo leo katika ukumbi wa juu ni wanafunzi wa Skuli ya Sekondari Vikokotoni, idadi ya wanafunzi hao ni 70 na wameambatana na walimu wao. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tutambue kuwepo kwao na niwaombe wageni wetu hawa pamoja na walimu wao waliofuatana nao wasimame ili muwasalimie Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Wale pale vijana 70 na walimu wao wa Skuli ya Sekondari Vikokotoni pahala ambapo huwa mnapazungumza sana Waheshimiwa Wajumbe basi leo wamekuja kusikia nini mnachokizungumza katika ukumbi huu kwa ajili yao. Nakushukuruni wageni wetu ahsanteni sana karibuni sana katika shughuli zetu. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 66

Malimbikizo ya Madeni ya Wafanyakazi wa Wizara ya Afya

Mhe. Panya Ali Abdalla – Alijibu:-

Mhe. Waziri kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya kutokana na malimbikizo ya madeni inayodaiwa na wafanyakazi hao pindi wanaporudi likizo au kurudi safari za masomo nje ya nchi.

(a) Je, Wizara ina mpango gani kutatua tatizo hilo.

(b) Wizara haioni kuwa inawatoa ari wafanyakazi wake ya kufanyakazi zao kiufanisi kwa vile wafanyakazi hao wananyimwa haki zao za msingi.

Mhe.Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli tuna maombi mengi sana ya wafanyakazi waliokwenda likizo ambao hawajapataa fedha za likizo tena muda mrefu. Hii imetokana na kutokuwa na mpango endelevu wa kulipa fedha hizo ingawa miaka ya nyuma sana fedha hizi zilikuwa zikitolewa. Lakini kukawa na malalamiko kwa sababu wengine wanapewa kidogo wengine wanapendelewa na wengine hawakupata kabisa. Kubwa zaidi kulikuwa na udanganyifu wa kupindukia na ufinyu wa fedha.

Mhe. Spika,

a) Kwa kuliona hilo, Wizara inajipanga na kuandaa utaratibu ambao utawezesha Kurugenzi kupitia mgao wao wa *other charges* kutenga fungu la fedha maalum kwa ajili ya likizo, badala ya utaratibu wa hivi sasa kubebeshwa mzigo huo Idara ya Utumishi ya Makao Makuu ya Wizara.

b) Wizara yangu inalielewa hilo na inaweza ikawa ni sababu moja wapo ya kupunguza ufanisi wa kazi. Lakini ufanisi wa kazi ni zaidi na kukosa pesa za likizo, kuna sababu nyengine zaidi moja wapo ni moyo wa uzalendo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kweli wafanyakazi wamekosa malimbikizo yao haya ya fedha za kwenda likizo. Je, Wizara yako inakabiliana vipi na suala hili ili kuweza kuwapatia wafanyakazi hawa ili waweze kuwa na moyo wa kizalendo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama vile nilivyojibu kwenye swali mama kwamba baada ya kulielewa suala hili Kamati Tendajo ya Wizara nikishiriki mimi mwenyewe tumetayarisha utaratibu wa kuhakikisha angalau basi vatu wanakwenda likizo kwa mpango maalum na wale wachache wanaokwenda wapewe haki yao kama ilivyotakiwa, badala ya kila mwaka watu wakaenda hawana kitu ikawa linalimbikizwa deni. Utaratibu huo tumeshaupanga wizarani na kwamba kila idara itakuwa sasa katika fedha zake inabidi itenge fedha maalum kwa kuwalipa wafanyakazi wanaokwenda likizo. Hii ni haki yao na wanastahiki kuipata hata kama fedha zitakuwa chache.

Nam. 67

Uhaba wa Wafanyakazi katika Hospitali ya Wete

Mhe. Panya Ali Abdalla - Aliuliza**:-**

Mhe. Waziri Hospitali ya Wete ina tatizo kubwa la uhaba wa wafanyakazi jambo linalokwaza ufanisi wake.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna mpango gani wa kuongeza wafanyakazi kwenye hospitali hiyo.

(b) Je, hao wachache waliopo hivi sasa wanalipwa malipo baada ya saa za kazi *(overtime).*

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala hili la wafanyakazi huko Pemba limekuwa likitajwa na kuulizwa kila mara. Wizara yangu ina upungufu mkubwa wa wataalam wa fani mbli mbali za afya katika hospitali zetu nchini na sio Wete tu isipokuwa hospitali zote. Hata hivyo, huduma zinaendelea kutolewa pamoja na mazingira magumu ya kazi yanayowakabili wafanyakazi wetu.

(a) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika suala moja huko nyuma kwamba ndio maana mwaka jana tuliajiri wafanyakazi wasiopungua 267 na asilimia 60 ya hawa tuliwapeleka Pemba kwa kufikiria upungufu huu. Lakini tunaelewa kwamba upungufu huo haukumaliza tatizo isipokuwa imesaidia. Hii inadhihirisha ni kiasi gani wizara inalitambua tatizo la upungufu mkubwa wa wafanyakazi ulioko Pemba na kukabiliana nalo ipasavyo.

(b) Utaratibu wa kulipa posho wafanyakazi wa afya kwa kufidia upungufu wa wafanyakazi haujawekewa mpango maalum na bado haupo. Posho kwa kawaida huwa zinalipwa kwa wafanyakazi wa afya wale ambao hawaingii *shift* na wanapoitwa kutoa huduma baada ya saa za kazi ndio wanaostahiki kupewa posho *(overtime)* ingawa nalo si kubwa la kutosheleza kama vile ambavyo tungependelea lakini hukata pua tukaunga wajihi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwepo na upungufu huo na wafanyakazi wanajitahidi katika kufanya kazi ambazo nyengine walipaswa wafanye wenzao.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuwapa motisha wafanyakazi hawa ili wasivunjike moyo waendelee na uzalendo wao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi na nina furaha kwamba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ananisikia hapa nikieleza hili.

Kwa kiasi miezi miwili sasa tuko katika majadiliano na Waziri wa Utumishi kuzingatia masuala haya. Lakini masuala yenyewe yanahitaji utaratibu ambao uko nje ya uwezo wa Wizara ya Afya, inabidi tuandike tujieleze turejeshewe masuala, pale litakaposimama tutawaambia wafanyakazi kile tulichofanikiwa.

Lakini suala la motisha na kuwapa moyo wafanyakazi hasa wale wanaofanya kazi zaidi ya zile walizotakiwa ni suala ambalo linanipa shida sana katika kusimamia huduma za afya.

Maana ninawajibika kumlazimisha mfanyakazi afanye lakini ananambia na mimi nawajibika vile vile kupewa kinachonistahiki. Lakini masuala ya utumishi yako nje ya Wizara ya Afya, ni suala tunalojadiliana na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na pale tutakapofanikiwa matunda watayaona. Lakini hilo tunaendelea nalo si chini ya miezi mitatu sasa kulijadili na wenzetu.

Nam. 93

Upatikanaji Walimu wenye Sifa za Kusomesha Walemavu

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Aliuliza**:-**

Kila mtoto mwenye ulemavu anahitaji kupatiwa huduma inayofaa kutoka kwa mwalimu anayefaa katika kumwezesha kupata elimu bora.

(a) Je, skuli ngapi tayari wanao walimu wa kufundisha watoto wenye ulemavu kwa mfano viziwi, wasioona na wenye matatizo ya akili.

(b) Je, Serikali ina mpango gani katika kuwapatia walimu wenye sifa/uwezo wa kufundisha watoto wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa wanafunzi wote wakiwemo wale wenye ulemavu wanahitaji walimu wenye sifa za kuelimika pamoja na kupatiwa huduma mbali mbali ndipo wanafunzi hao wataweza kujifunza na kuwezesha kupata elimu bora. Wizara yangu inatekeleza elimu mjumuisho ili kuhakikisha wanafunzi wote wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu wanasoma pamoja bila ya ubaguzi wowote na wote wanafaidika na elimu inayotolewa. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa zipo skuli 86 (50 Unguja na 36 Pemba) zenye walimu waliopatiwa mafunzo ya kuridhisha na mbinu za kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu, wakiwemo wanafunzi viziwi, wasioona na wenye ulemavu wa akili.

(b) Mafunzo ya cheti cha ualimu wa elimu mjumuisho yanatolewa katika Chuo cha Kiislam Mazizini. Walimu hawa tayari wana cheti cha ualimu na cheti cha elimu mjumuisho ni sifa ya ziada kwa walimu hao. Wahitimu 230 tayari wamehudhuria mafunzo hayo na hivi sasa wanafundisha katika skuli mbali mbali. Pia baadhi ya walimu wanahudhuria mafunzo ya stashahada ya elimu mjumuisho katika Chuo cha Ualimu huko Tanzania Bara. Vile vile mafunzo mafupi yanatolewa kwa walimu wetu kupitia vituo vya ualimu tisa vilivyoko katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, maskuli mengi ya elimu mjumuisho tunayokwenda tunakuta mwalimu mmoja mmoja wakati kuna wanafunzi wa aina mbali mbali za ulemavu ambao kila mmoja ana shughuli zake anazofanyiwa. Je, katika walimu walioajiriwa juzi wasiopungua 200 kuna walimu wangapi wenye sifa hizi walioajiriwa katika maskuli kufundisha watoto hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, walimu wote 230 ambao tumesema tumewapa mafunzo haya wapo katika skuli zetu mbali mbali za Unguja na Pemba. Mhe. Spika, ni kweli alivyosema mama yangu Mhe. Raya Suleiman Hamad kwamba wanafunzi wale wana mahitaji mbali mbali, kuna wale walemavu viziwi wao wanahitaji mafunzo ya alama yaani mwalimu awe anaweza kufundisha lugha ya alama. Lakini kuna wenzetu wanafunzi wasioona wale wanahitaji walimu wenye taaluma maalum

inayojulikana kama kujifunza kwa kutumia nukta nundu. Lakini katika hao walimu wetu wote ambao tunawapeleka maskulini uwezo wa kufundisha wanafunzi hao wanao.

Mhe. Spika, tukichukulia kama ndio kwanza tunaanza, tumeanza hili zoezi mwaka 2004. Kwa taarifa ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, katika nchi ambayo inafanya vizuri katika zoezi hilo basi Zanzíbar tunaongoza kwa sababu tunalifanya hili zoezi kwa vitendo. Wale ambao wanatufadhili katika zoezi hili basi wakitoa mfano husema nendeni mkajifunze Zanzíbar kwa sababu muda ambao tumeanza ni mchache lakini uwezo wa kwenda na wanafunzi wetu hivi sasa ni mkubwa.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitaka nieleze Baraza lako tatizo ambalo tulikuwa tunalo kubwa katika ufundishaji huu ni vifaa, vifaa vya kufundishia wenzetu hawa ni ghali mno. Kwa sababu kama wenye ulemavu wa macho kuna kifaa kile cha elimu ya mwanzo, halafu wakitoka hapo wanakwenda kwenye *braille machine* ni shilingi milioni 1.5 na havipatikani hapa Zanzíbar wala Tanzania Bara, kwa nchi ya karibu basi ni Afrika Kusini.

Lakini nataka niwaeleze kama vifaa hivi tayari tunavyo stoo kwa wingi na tunatarajia kuvigawa. Maafisa wetu wako katika maskuli hivi sasa kuhakikisha kama tuna wanafunzi wangapi ambao wana mahitaji haya ili vifaa hivi viweze kuwafikia. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wapo baadhi ya wazee wanawaficha watoto wao kwa ajili ya ulemavu na kukosa haki zao za msingi. Je, Mhe. Naibu Waziri una mikakati gani ya kuwaelimisha wazee hao ili wawafichue watoto wao na wapate haki yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kama bado kuna wazee ambao wanawaficha watoto wao kwenda maskuli ili kupata elimu. Mhe. Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na masheha tunaifanya kazi hii kwa kupitia maskulini, tunashirikiana na masheha tunawaita wazazi wote ili kuhakikisha kila mtoto basi ana haki ya kupata elimu. Hivi karibuni Mhe. Spika, maafisa wangu walikuwa wamo katika hili zoezi kwa sababu tuna skuli nyengine karibu 34 ambazo tunataka kuwapelekea hii elimu mjumuisho mbali ya zile ambazo nilizungumza mwanzo kwenye jibu langu mama. Kwa hivyo, maafisa wale wanapita maskulini na tayari wametoa mafunzo hayo wametoa hamasa na kwa wazazi kushirikiana na masheha wetu ambao wamo katika skuli husika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa tu nimjulishe kitu kimoja. Wenzetu katika Idara ya Watu wenye Ulemavu na Wizara ya Elimu vile vile wanawachukua wale watu ambao wana ulemavu na kuwapeleka katika vyuo vya Arusha na huwa wanakuwa *sponsored* na *UNDP*. Je, kwa upande wa Zanzíbar wizara ina mpango gani katika suala kama hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikiri bado wizara mpaka hivi sasa haijawa na mpango huo, mpango ambao tulikuwa tunauendeleza mpaka hivi sasa ni huu ambao tumezungumza. Lakini nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba hivi vifaa tulivyovitaja ambavyo tayari tunavyo katika wizara yetu basi ni wao hawa ambao kwa kiasi kikubwa wametusaidia kupata hivi vifaa.

Nam. 112

Uchakavu wa Skuli ya Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Kwa muda mrefu Skuli ya Msingi na Sekondari ya Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja inakabiliwa na tatizo la kuvuja mapaa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wanafunzi.

(a) Mhe. Waziri ni hatua gani Wizara imechukua katika kuondoa kero hiyo.

(b) Je, Wizara yako itakuwa tayari kushirikiana na wananchi kwa upande wao kujitolea nguvu kazi na Serikali kuchangia mabati na mbao ili skuli hiyo iweze kufanyiwa matengenezo ya haraka kabla ya kuanguka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 112 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya mapaa ya majengo ya Skuli ya Msingi na Sekondari ya Kitogani yanavuja na hivyo kusababisha usumbufu kwa walimu na wanafunzi wakati wa kipindi cha mvua. Mapaa yanayovuja ni yale ya majengo ya zamani yaliyoezekwa mabati ya *asbestos*. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara inaelewa ubovu wa bati wa skuli hiyo, lakini kutokana na uchache wa fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa skuli, Wizara yangu kwa sasa haina uwezo wa kutosha kukarabati majengo ya skuli zetu nyingi zilizoko katika hali kama hiyo kutokana na wingi wa majengo yanayohitaji kukamilishwa ili skuli zetu ziweze kuchukua wanafunzi wapya wa darasa la kwanza. Natoa ushauri kwa Mhe. Mwakilishi akishirikiana na Kamati ya Skuli wajitahidi kuyafanyia ukarabati wa muda mapaa hayo hadi hapo Wizara itakapokuwa na uwezo wa kutosha.

(b) Kama nilivyosema katika swali lililotangulia, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na wananchi wa Kitogani katika kuyafanyia matengenezo baadhi ya majengo hayo kwa kadri uwezo wetu kifedha utakavyoruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na ushauri alioutoa Mhe. Naibu Waziri Mwakilishi jimboni kwake ana wizara karibu mia moja. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwangu mimi imegawika katika vifungu 26 na yeye mwenyewe shahidi katika jitihada anazozichukua katika Jimbo la Muyuni. Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi tulipitisha sheria ya kulinda haki za watoto ikiwemo wanafunzi kupata elimu katika mazingira bora.

(a) Je, wizara yako inatekeleza na inalinda vipi sheria hiyo.
(b) Kwa kuwa serikali kila mwaka inapitisha bajeti. Kuna sababu gani ya kutokujengwa skuli ile.
(c) Wananchi wa Jimbo la Muyuni wako tayari kutoa gharama ikiwemo misumari, miunda na gharama za ufundi. Je, wizara yako iko tayari kutoa mabati 300 ili kunusuru hali hiyo ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kila mwaka inapitisha bajeti. Kwa mwaka huu tulipitisha bajeti ya ujenzi wa madarasa mapya. Kwa zile skuli ambazo walimu na wazee wanajenga basi sisi wizara humalizia. Kwa mwaka huu tulikusudia kumalizia skuli 200 na pia kuna skuli ambazo tulizipa vipaumbele zile ambazo tutazifanyia ukarabati mkubwa.

Mhe. Spika, kupanga ni kuchagua, hiyo mvua ikinyesha kuna skuli ambazo ni chururu na nyengine ni ndondondo kwa hivyo tunatazama vile vipaumbele. Katika mabanda ambayo tulikusudia tuyamalize Mhe. Spika, mabanda 122 tayari tumemaliza. Pia skuli 6 zile ambazo tulisema tutazifanyia ukarabati mkubwa basi tukizungumza bajeti tayari skuli 4 tumezifanyia tumebakia skuli 2.

Mhe. Spika, skuli ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub hii ambayo anaizungumza haikuwepo katika bajeti hii ya mwaka huu kwa hivyo mpaka mwezi Julai hatutokuwa na uwezo wa kumtengenezea Mhe. Mwakilishi skuli hii. Lakini kwa bajeti mpya ambayo tunakuja nayo basi katika skuli ambazo tumekusudia kuzifanyia matengenezo makubwa ni skuli hii imo. Sasa Mhe. Mwakilishi akinieleza kama wazee, walimu, pamoja na yeye mwakilishi yuko tayari kusaidia gharama mimi nafurahi, lakini kwa mwaka huu mpaka mwezi Julai sitoweza kumuezekea kwa sababu sina hiyo bajeti ya kumuezekea. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwakilishi anikubalie kwa mwaka unaokuja basi nitakuwa tayari kumuezekea tusaidiane hizi gharama kwa sababu bajeti niliyonayo itakuwa inatosheleza na tayari tumeanza mchakato wa bajeti skuli hii imo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna skuli wanazipa vipaumbele katika kuzifanyia ukarabati.

(a) Je, ni vipaumbele gani wanavyotoa kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati.
(b) Skuli ya Msingi Potoa na Skuli ya Msingi Mkwajuni zina tatizo kama hilo la kuvuja. Je, ziko katika vipaumbele hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli nilizungumza kama kuna skuli ambazo tunatoa vipaumbele. Skuli ambazo tunatoa vipaumbele sio vipaumbele kwa ajili ya upendeleo, ni zile skuli ambazo tunaziona ziko katika hali mbaya zaidi. Kwa bajeti hii ambayo tunakuja nayo katika skuli ambazo

tumezitembelea na tukaziona ziko katika hali mbaya sana, basi katika skuli mbili ambazo amezitaja Mhe. Mwakilishi Skuli ya Msingi Potoa imo katika matengenezo hayo makubwa. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muyuni kwa kukubali kuchangia miti na misumari ya kuezekea jengo hili.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri ameomba kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub amstahamilie mpaka wakati wa bajeti basi skuli yake itaingizwa kwenye mpango wa uezekaji. Je, anakusudia kutwambia kwamba wanafunzi wasisome mpaka baada ya bajeti kwa sababu kipindi hichi ni cha mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sikusudii wanafunzi wasisome na ndio pale katika jibu langu mama nilipotoa rai kwa Mhe. Mwakilishi akishirikiana na wazee wa pale wafanye matengenezo madogo madogo ya kuweza kuziba japo kwa kuweka viraka zile tobo ambazo zinavuja, ili tustahamili mpaka wakati wa bajeti, tuweze kufanya hilo mheshimiwa.

Mhe. Spika, ninaamini Mhe. Jaku uwezo wa kufanya hivyo anao, kwa sababu ninazijua juhudi za Mhe. Jaku katika kuhakikisha kua elimu inakwenda mbele na wanafunzi wetu wanasoma. Yeye ni mjumbe katika kamati ya ustawi wa jamii, wizara ambazo anazitembelea, basi moja ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ninamuona katika skuli mbali mbali, kwa sababu anaijua bajeti yetu. Pia anajua uzito ambao tunao katika kutengeneza na kujenga majengo mapya, hua anatoa misaada katika skuli zetu mbali mbali, na tunamshukuru kwa hilo. Kwa hivyo, naomba na hili ashirikiane na wazee ili kuhakikisha tunatoa huduma ya kwanza pale, mpaka itakapofika wakati wa bajeti, basi namuahidi skuli hiyotutaifanyia matengenezo ya kutosha Mhe. Spika.

Nam. 157

Usumbufu wa Usafiri

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kutokana na kua wananchi wengi wanaoishi vijijini kwa Unguja na Pemba wanakabiliwa na usumbufu wa usafiri. Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hilo kama inavyofanywa katika sehemu nyingi zinazounganisha Mji wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 157 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali baada ya kuona wananchi wengi wanaishi vijijini kwa Unguja na Pemba, imeshaanza kutoa ruhusa ya njia inayounganisha vijiji baada ya kupata maombi kutoka kwa wananchi wa vijiji husika. Kwa hivyo, sasa ruhusa ya njia tatu zinazounganisha vijiji, tayari imeshatolewa. Njia zenyewe ni;

1. Tunguu hadi Kinyasini
2. Makunduchi hadi Jambiani na
3. Chwaka hadi Matemwe.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa bahati mbaya jibu sikulisikia vizuri. Kwa hivyo, naomba tena arudie kwa heshima yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, serikali baada ya kuona wananchi wengi wanaishi vijijini kwa Unguja na Pemba, imeshaanza kutoa ruhusa ya njia inayounganisha vijiji baada ya kupata maombi kutoka kwa wananchi wa vijiji husika. Kwa hivyo, sasa ruhusa ya njia tatu zinazounganisha vijiji, tayari imeshatolewa. Njia zenyewe ni;

1. Tunguu hadi Kinyasini
2. Makunduchi hadi Jambiani na
3. Chwaka hadi Matemwe.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sasa nimesikia vizuri. Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, swali la mwanzo, utaratibu huu wa kuwa wanavijiji wenyewe waombe unaanza mwaka gani.

Je, sisi wawakilishi tumeletwa hapa kwa kazi gani, ikiwa moja sio kuwatetea wananchi wetu na maendeleo au kauli yetu sisi haiaminiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Samahani Mhe. Spika, swali lake la pili sikulisikia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, swali la pili ni kua, sisi ni wawakilishi wa wananchi na wananchi tunawawakilisha hapa katika mambo yao yote, ikiwa ni pamoja na mambo ya maendeleo. Kwa hivyo, kuna sababu gani ikawa hii kauli yetu tunayoitoa hapa kwa niaba ya wananchi, ikawa haina nguvu mpaka wananchi waombe wenyewe. Lakini swali la mwanzo lilikuwa, mpango huu kwa wananchi waombe wenyewe unaanza lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu uliopo ni kwamba kuna tofauti ya mambo mawili. Kuna maeneo ambayo yana ruti, unapotaka kuengeza gari katika eneo lile kuna utaratibu wake mwengine na maeneo ambayo hayana ruti, ni lazima wale wanakijiji husika ndio wanaotakiwa waandae maombi, kwa sababu wao ndio wanaojua shida ya usafiri wa eneo lile.

Mhe. Spika, serikali inachoweza kukifanya ni kutengeneza ile ruti. Lakini kama hakuna maombi ya watu wanaohitaji kusafiri, basi serikali haiwezi kupeleka zaidi ya kujenga barabara, kuweka ruhusa ya njia. Utaratibu mwengine ni lazima wale wahusika wa maeneo yale ndio wanaotakiwa kufanya maombi na mimi sioni ubaya wake.

Mhe. Spika, kwa sababu mahitaji wanahitaji wale wanaokaa katika eneo husika, wanachokifanya wao kwa kupitia sheha na Halmashauri, kupeleka maombi katika idara husika ya kuomba kwamba tunahitaji ruti hii, kwa sababu tumekuwa wengi na kuna upungufu wa magari. Kwa hivyo, serikali inaruhusu kwa kupitia mamlaka iliyopewa idara. Sasa mimi sioni tatizo.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, sijajibiwa swali langu moja, nilisema huu utaratibu kuwa lazima wananchi waombe wenyewe ulianza mwaka gani, kwa sababu tumefanya mambo mengi tu na tuna wawakilisha wananchi halafu *Alhamdulillah* serikali inakubali na tunawaondolea shida chungu nzima.

Mhe. Spika, hata mimi nina barabara inatengenezwa na *millennium*, hajaja mwananchi kuomba nilizungumza mimi shida ya barabara tuliyonayo, maji nilizungumza mimi mwenyewe na kadhalika. Kwa hivyo, ikiwa mimi ni mwakilishi nimezungumza, halafu naambiwa wananchi waeleze wao wenyewe, ina maana gani sisi kuja hapa na kuwazungumzia wananchi matatizo yao.

Mhe. Spika: Swali lake ni kwamba mwaka gani utaratibu huu wa wananchi kuomba wenyewe umeanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, idara yetu ya usafiri na leseni hivi sasa inaendeshwa chini ya usimamizi wa sheria nambari 7 ya mwaka 2003, pamoja na kanuni zake ndogo ndogo ambazo zinaendelea katika kuungana katika uendeshaji na usimamizi wa sheria hii.

Mhe. Spika, kama itakua nimemuelewa vizuri swali lake Mhe. Mjumbe. Kama kuna maombi ambayo yeye Mhe. Mwakilishi ameyaleta basi tunaomba atukumbushe na sisi kama idara husika ya serikali tutayafanyia kazi na tutawapatia ruti hiyo wahusika wananchi wetu, ili kuwaondolea usumbufu unaojitokeza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kua Mhe. Naibu Waziri kasema kwamba utaratibu wa sasa ni kwamba wananchi waombe ndio watengenezewe barabara zao na kwa kua barabara zenye matatizo vijijini ni nyingi sana. Kwa kua Mhe. Naibu Waziri kaitoa ahadi hiyo, napenda kumuuliza je, wamefanya utaratibu gani wa kuwatangazia wananchi wakajua kwamba sasa mpaka waombe. Je, kwa kua barabara ni nyingi zinazoombwa ni utaratibu upi unaotumika na ni barabara ngapi zimeombwa kwa upande wa Pemba ili kutengenezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Subeit Khamis hakunifahamu vizuri. Tulichokua tukikizungumzia hapa ni suala la ruti za magari, sio masuala ya kutengeneza barabara. Sasa suala lake Mhe. Subeit ameeleza suala la kutaka kutengenezewa barabara, hilo ni jambo jengine kabisa.

Mhe. Spika, utaratibu wa kutaka kutengeneza barabara za ndani ni ule ule kwa kupitia halmashauri, kusaidiana na mfuko wa barabara na Idara yetu ya UUB tunaendelea kusaidiana.

Mhe. Spika, suala lililokua likizungumzwa hapa ni suala la kwamba kuna wananchi ambao wako vijijini wanashida za usafiri, namna ya kupata ruti ya kwenda magari kufanya huduma za usafiri wa wananchi wetu, ndicho kilichoulizwa. Sasa utaratibu wa kuomba ruti ni ule ule, kwamba wananchi husika kwa kupitia sheha wao au halmashauri zao, wanatuletea maombi na sisi tunayaratibu na kuwapatia ruti hizo.

Nam.143

Kukamilika kwa Barabara ya Mtoni Kidatu Amani

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kuna taarifa kupitia vyombo vya habari kua barabara itokayo Mtoni Kidatu kuelekea Amani (Mkapa Road), njia ambayo ujenzi wake unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari fedha za ujenzi huo kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania zimeshakabidhiwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Kuna ukweli wowote wa taarifa hizo.
(b) Kuna sababu zipi zilizopelekea kukwama kwa ujenzi wa barabara hiyo huku ikiendelea kuhatarisha maisha ya wananchi na watumiaji wa barabara hiyo kwa jumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe, Mjumbe swali lake nambari 143 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kua ni kweli fedha jumla ya Tsh. Bilioni 1.6 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimeshakabidhiwa na zimeshatumika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika ujenzi wa barabara husika.
(b) Ujenzi umekwema kutokana na kumalizika kwa fedha hizo za ujenzi, pamoja na upungufu wa fedha kwa ajili ya kufidia nyumba zitakazoathirika na ujenzi wa barabara hiyo hasa katika eneo la Mtopepo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishakabidhi fedha hizo Tsh. Bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Lakini barabara hiyo mpaka hivi leo haijakamilika. Pia amesema kwamba ni ukosefu wa fedha.

Mhe. Spika, nilikua nataka kujua makisio ya awali ya ujenzi wa barabara hiyo yalikua kiasi gani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutoa kiasi gani na kubakia kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tathmini ya awali iliyo kadiriwa Shs. Bilioni 1.6 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo. Barabara hiyo ina urefu wa kilomita 4. Kwa bahati mbaya fedha hizo zilichelewa kupatikana.

Mhe. Spika, wakati tunafanya tathmini hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikua ina akiba kubwa sana ya lami. Kwa kuchelewa kwa fedha zile, lami ile ikatumika kwenye maeneo mengine, zilipokuja kupatikana fedha zile ikawa lami haipo, ikabidi sasa fedha zile, Shs. Bilioni 1.6 baadhi yake zitumike katika kufidia lami, lakini pia mfumko wa bei na gharama, hasa suala la mafuta nalo lilikua limepanda. Sababu hizo ndizo zilizopelekea kwamba tathmini ile ya kwanza ikashindwa kukamilisha ujenzi ule kama ulivyokua umetarajiwa.

Baada ya kuliona hilo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea kufanya tathmini na kuona hivi sasa kwamba kuna haja kupatikana Shs. Milioni 400, ili kuweza kukamilisha kazi za ujenzi wa barabara ile kwa sehemu iliyobakia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri aliyojibu. Lakini Mhe. Spika,

kikwazo kikubwa cha barabara ile, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo ni kwamba imekwamishwa na kutolipwa watu fidia za nyumba zao.

Je, kwa sababu tatizo hilo na barabara hii ilianza kwa vishindo na kasi kubwa, na sasa hivi imekwama njiani. Je, serikali haioni ni kuzikwamisha juhudi zake wenyewe ilizozifanya. Kama ni hivyo, kwa sababu mvua za masika zinaanza na barabara ile itachimbuka tena kama mwanzo na wakati tumeshatengeneza. Je, ni lini hasa serikali itawalipa wananchi fidia zao ili barabara ile imalizike.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli miongoni mwa changamoto ambazo zinaikabili idara yetu ya UUB na wizara katika mradi ule ni suala la fidia. Tulifanya tathmini mara ya kwanza ikawa jumla ya Tsh. Milioni 800 zinahitajika, lakini serikali ikaendelea tena kufanya utafiti na kufanya tathmini ya mara ya pili, ikaonekana kwamba kuna haja na ulazima wa kulipwa fidia kwa Shs. Milioni 600 kama tulivyoeleza katika jibu mama kwa maeneo ya Mtopepo. Ni kweli kwamba kuna watu wanahitaji kulipwa fidia na kiasi kinachohitajika ni Shs. Milioni 600.

Kwa hivyo, serikali inaendelea na juhudi zake na jitihada zake na mradi huu utakamilika, kwani tumeshafanya mazungumzo na kupewa maelekezo na serikali kwa kupitia mfuko wetu wa barabara. Jambo hili tunaimani litakwamuka na barabara hii itajengwa chini ya ufadhili au fedha zitakazotoka katika mfuko wa barabara.

Nam. 156

Upatikanaji wa Maji Safi

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Spika, Upatikanaji wa maji safi na salama ni jambo la lazima kwa kila binadamu.

Ni sababu zipi hasa zilizopelekea wizara yako kushindwa kueneza maji ambayo yapo ya kutosha ardhini kwa wananchi wake na hasa wanaoishi vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 156 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba huduma ya maji ni jambo la lazima kwa mwanadamu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu, imechukua huduma kwa kiasi kikubwa cha kuwapatia wananchi wa mjini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Kwa kuendeleza huduma hiyo kuna miradi tofauti ikiwemo mradi wa *ADB, ACRA, TASAF*, mradi wa Maziwa Ng'ombe, mradi wa Kojani, Mradi wa Konde, mradi wa Chokocho na mradi wa Shumbaviamboni. Kumalizika kwa miradi hiyo yote kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo hilo la maji vijijini.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri kuhusu namna ya kusambaza maji vijijini. Mhe. Spika, naomba uniruhusu niulize swali langu moja la nyongeza, ambalo ni refu kidogo kama ifuatavyo. Mhe. Spika, katika jimbo langu kuna vijiji.

Mfano, Mitambuni, Kinazini, Makongeni, Chanjaani, Kiapaka, Kidundo, Chekea, Mtambwe mkuu, Tondooni, Kinazini, Letekofi na kadhalika. Mote humu hamna maji, na mimi katika kumbukumbu zangu kwenye hizo kampuni alizozitaja, hakuna moja ambayo itaelekea katika Jimbo la Mtambwe.

Je, kwa haya maeneo ambayo hao wafadhili aliowataja hawamo hawafanyikazi huko, ndio sisi tutakaa hivi hivi tu.

Vile vile Mhe. Spika, kuna tangi la maji pale Bahanasa, liliharibika na kusababisha eneo kubwa la Shehia ya Piki, Shehia ya Kisiwani na Mzambarauni kukosa maji. Je, tangi lile litajengwa lini tena upya ili wananchi waondokane na shida hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia mamlaka ya maji lengo kuu ni kuhakikisha, kwamba inasambaza maji mijini na vijijini kama nilivyoeleza mwanzo.

Kwa hivyo, vile vijiji ambavyo tumepeleka miradi hiyo ni kwamba tumeanzia tu, lakini tunategemea kumalizia katika vijiji vyote ambavyo havijapata huduma hiyo. Kwa hivyo, sio kwamba wizara yangu kwa kupitia mamlaka ya maji imevidharau hivyo vijiji vyake ambavyo bado havijapata huduma. Ninachomuomba Mhe. Mjumbe ni kwamba astahamili na huko tutaelekea, lakini mambo ni lazima yapelekwe kiutaratibu. Twende huku na kisha tumalizie huku.

Kuhusu tangi, tunajitahidi na tunajipanga ili fedha itakapoingia tu tutalishughulikia tangi hilo na *Inshaallah* watapata huduma hiyo wananchi kama vile inavyostahiki.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wananchi wa Jitenge Maziwani jimbo la Kojani, wanashida sana ya maji na Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi, ambaye ni mimi mwakilishi ninayezungumza hapa, tumejitahidi kuwapelekea paipu za maji na zimefika, lakini maji hayo mpaka leo hayatoki.

Je, ni sababu gani za msingi zilizofanya maji hayo yasitoke na wananchi hao kufaidika na maji safi na salama.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza kwa upande wake yeye mwenyewe katika kijiji chake nimpongeze kwamba huduma hiyo sasa hivi iko katika hatua nzuri. Ndio maana nikasema uko mradi wa Kojani, lakini huu mradi kwa upande wa Kojani umeshamalizika na tumeshauzindua. Ina maana Kojani kwako kuzuri.

Katika hivyo vijiji ambavyo vina matatizo na tayari bomba zimeshafika. Ni kweli nakubaliana na wewe kwamba kuna kasoro ya maji, lakini tutajitahidi kufanya matengenezo, tutapitia katika hizo sehemu tuangalie ni nini kinachosababisha, kisha tutayashughulikia na matengenezo ili na wao wafaidike.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, asubuhi hii kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, shemegi yangu, swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri je, ni sababu zipi zilizopelekea mpaka leo hii mradi wa *ACRA* kutomalizika katika vijiji vyetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kabla ya kumjibu hili swali Mhe. Mjumbe, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Makame Mshimba kwa kuliomba radhi Baraza lako tukufu kutokana na kitendo kilichotokea.

Vile vile nimpe pole sana kwa maumivu ya tumbo kali lililompata juzi na kutokuhudhuria katika Baraza hili.

Mhe. Spika, mradi wa *ACRA* umefikia katika hatua nzuri, lakini yaliyobakia ni matatizo madogo madogo. Kwa hivyo, tutajitahidi sana kuyafuatilia na kuyaweka sawa.

HOJA ZA KAMATI

Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyokubaliana jana tunaanza majadiliano, kuhusu ripoti ile *(Makofi)*

Nadhani sasa iko sawa. Nafikiri mjumbe anayehusika atajisawazisha na hilo. Kwa hivyo, tuanze kwa kumsikiliza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza leo hii kutia *fat-ha* hapa katika hii kamati teule. Kwanza niwapongeze sana Mwenyekiti na wajumbe wake wa kamati teule kwa kutuletea ripoti yao teule.

Vile vile Mhe. Spika, kabla sijaendelea, leo naomba unipe kama ikiwa tuna sheria ya dakika 30, basi ningeomba tutenge kando kanuni unipe mpaka dakika 60. Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kutokana na elimu, uzoefu, utu uzima wako na kwa sababu hiyo una busara nyingi. Mimi sina cha kukupa, lakini Mwenyezi Mungu ndiye atakayekupa fungu kubwa zuri la kukujaalia na kukutengenezea katika safari yako ya heri. Kwa sababu usione nakutakia ufe, hapana. Kwa sababu binadamu kufa ni wajibu. Hayo nimeona leo asubuhi nikwambie,

kutokana na muongozo wako mzuri na mimi kua muungwana kukubali kukiri kosa langu, ni kutokana na busara zako Mhe. Spika, nashukuru sana.

Pia nashukuru sana vyombo vya habari, mawio na wengine wote nawashukuru kwa kutekeleza wajibu wao, ili na mimi kuniweka katika hali nzuri na kuweza leo Zanzibar nzima natambulikana kwa heshima niliyoitoa katika Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nianze katika mswada huu. Mambo mengi tumeletewa na kamati teule, kuna mambo mengine wamesema ya kuwaaidhi watu, kuna mambo mengine yameelezwa humu ya kuwatia watu hatiani. Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo.

Mhe. Spika, kwanza mimi naanza na suala la kuuzwa kiwanja cha ofisi ya wizara hiyo ya mawasiliano kwa wakati ule. Hili ni jambo ambalo linasikitisha sana. Mhe. Spika, haliepukiki suala hili na kwa sababu haliepukiki, tunaambiwa viongozi tusishiriki katika masuala kama haya. Lakini leo tunafika kushiriki masuala kama haya kwa kuidhoofisha serikali yetu na hasa wafanyaji wenyewe wanakuwa ni watu wakubwa. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana.

Mhe. Spika, ni dhahiri inaonesha kutokana na kamati teule, kwa sababu hawa ni watu wamesoma sana, hawakufanya jambo kwa chusha, hawakufanya jambo kwa kumuhukumu mtu au kwa kumchukia mtu, sidhani hivyo. Wamefanya jambo ki*lillahi taala* ya amri ya Mwenyezi Mungu. Ndio walivyofanya hivyo.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, naamini binadamu ukiingia kwenye makosa, basi sheria ifuate mkondo wake, hilo nakubaliana nalo kabisa. Tusione tabu binadamu kufanya kosa, aidha, inategemea katika kosa lile kwa mujibu wa sheria lina mtazamo wa aina mbili, wanasheria wapo watanisaidia.

Kuna jambo la hapo kwa hapo sheria inakutizama na kuna jambo lililokua ni la muda mrefu. Kwa sababu kuna jambo ambalo hutengenezwa kwa misingi ambayo ya kutaka kufanya jambo, sheria nayo hiyo inakuangalia hukumu yake.

Mhe. Spika, suala hili halikuwa na ghafla, isipokuwa lilikuwa na muda mrefu. Kwa maana hiyo, ilikuwa na muda mrefu basi tayari mwenye kufanya jambo hili anaingia makosani moja kwa moja kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, inaeleza kuwa kimeuzwa kiwanja hicho kwa shilingi milioni 200. Kwa kweli shilingi milioni 200 hivi sasa wizara za serikali zimehamia kwenye majengo mabovu. Lengo hasa kwa sababu kitu kinachonifurahisha Mhe. Spika unapobadili buti basi hata na suti ubadili, kwani huwezi kubadili buti tu Mhe. Spika na suti ikawa nyengine na wala haiwezekani. Kwa mfano, ukiniangalia mimi nimevaa buti nzuri pamoja na suti nzuri na hivyo ndivyo inavyotakiwa Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa kweli tumeunda mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa maana hiyo, iendae na mazingira ya Serikali ya Umoja wa Kitafa, ndio maana yake. Kwa mfano, leo tunazo afisi za kurithi za Mji Mkongwe ni aibu, lakini kumbe tunapata viwanja na sisi tunauza maana yake nini Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana na serikali ndio muamuzi wa mwisho pamoja na kuangalia, kwa sababu Kamati kazi yake ni kuiwasilisha na kuchangiwa. Kwa hivyo, tunaichia serikali ikifuatiwa chini ya Mdhamana wa Mhe. Makamo wetu wa Pili wa Rais, tena Mhe. Makamo anaye Mhe. Waziri mzuri, yaani ni *centre forward* Mhe. Waziri wake, sasa tunawaachia wao jukumu hili wataamua wao kwenye safu yao. *(Makofi)*
Katika hili nadhani si vyema kumshirikisha Mhe. Rais, kwa sababu Mhe. Rais amemteua Mhe. Makamu wa Pili ambaye yumo ndani ya Baraza na yeye ndiye atakayeangalia je, hivi ni kweli au sikweli? *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu jengo la Wizara ya Fedha Pemba. Mhe. Spika, kwa kweli ni suala la kusikitisha sana, kwa sababu nakumbuka Mzee wangu Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) wakati ule tulikua kwenye Kamati ya Fedha ambapo Mhe. Salmin Awadh Salmin alikuwa ndiye Mwenyekiti wetu.

Mhe. Spika, tulikwenda kule kwa ajili ya kuliangalia lile jengo, basi wakati tunafika wale jamaa wanachukua mchanga kwa ajili ya kufukia michirizi, yaani wanafukia zile nyufa za chini kwenye sakafu ah! Mimi niliigundua ile hali na kuwauliza vipi, wakasema maana yake tunazuia maji yakitoka juu yasi-*block* hivi. Mhe. Spika, nikafanya kama nacheza muziki hivi kule vile nazifukua zile nyufa na kwa kweli ni nyufa kubwa sana, yaani chini ile sakafu imeanza kupasuka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazee wetu wakulima na wakwezi wanafanyakazi vizuri kwa ajili ya kututafutia fedha, ambazo tuzilipie kodi kwa *mintarafu* ya kupata kitu kiwe kizuri Mhe. Spika. Sasa leo tunakwenda kuzitokomeza, yaani kuziharibu na halafu Mhe. Spika tunyamaze kimya. Kwa kweli inauma sana hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo nataka niwaambie waandishi wa habari haya ndiyo mambo ambayo tunataka hivi sasa yatolewe kwenye Gazeti, Kipindi cha Mawio, *ITV* na Mhe. Waziri niangalie vizuri, lakini ndiyo mambo ambayo yanatakiwa yawe *published* kwa wananchi na waelewe kitu gani kinachotakiwa, kwa sababu mambo ya haki wenyewe ni wananchi ndio walioanza kuchangia masuala haya. *(Makofi)*

Kwa kweli wahusika hawa hatutokua radhi nao, isipokua wachukuliwe hatua haraka sana na fedha zirejeshwe na wala si kitu cha maskhara Mhe. Spika, tena inauma sana. Mhe. Spika, hivi jengo lile kama watu wangekuwemo mule ingekuwaje, kwa sababu alitakiwa baba, mama na kama ingetokezea ajali tungepata uzazi hapo, yaani mama na baba wote wangekosa mtoto na wote wangekuwa wameshakufa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hiyo ni hatari kubwa sana. Kwa kweli lengo la binadamu ni kuzaliwa na yeye baadaye aweze kuzaa. Lakini kuna mambo mengine tunayasababisha kwa makusudi. Sasa hilo moja ambalo nimesema wahusika wa jengo lile wachukuliwe hatua mara moja Mhe. Spika na wala sio kitu cha kuweka.
Kamati hii sijui ilikuwaje isiwe na askari pamoja na pingu kabisa, yaani ilikua wapewe kabisa. Mhe. Spika, kwa mfano wenzetu kule Uganda Kamati ya *PAC* wanatembea na askari pamoja na pingu, yaani ukigundulika tu, basi unatiwa pingu mkononi. Kwa hivyo, nadhani Kamati hii tungeipa meno na kuwapa askari, ili watakapokugundua basi wakukamate pale pale na kukutia pingu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana suala hili lifuatiliwe kwa haraka sana, ili wananchi waweze kuwa na imani na viongozi wao kutokana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Sasa wakati tunapotoa hoja Mhe. Spika huwa tunababaishwa hivi na vile, Kamati Teule hii imekwenda *in deep* na ikagundua. *(Makofi)*

Jengine nizungumzie kuhusu Mzee wangu Juma Kidawa. Kwa kweli mimi nakubaliana na ushauri wa Kamati kwa asilimia mia moja, kwa sababu kosa limepitikana na limeonekana kama ni udanganyifu umefanyika wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huu udanganyifu sisi Waheshimiwa Wawakilishi sio kazi yetu, kwa sababu sio muhimili wetu, isipokua muhimili wetu sisi ni kutunga sheria na kuwapelekea wahusika wa sheria, basi watajua wenyewe na wala sisi hatusemi hiki kitu.

Lakini nakubaliana nao kwamba yule mzee angalau naye kutokana na lile jasho lake na kufanyiwa udanganyifu kulipwa zile fedha. Kwa kweli nakubaliana nalo na lile suala kama walivyosema Kamati kua yule mama mhusika apewe hati na wala sipindi nakubaliana nalo. Kwa maana hiyo, yule mzee tayari tumeshamsaidia tena masuala ya mkono wa sheria watajua wao wenyewe. Mhe. Spika, hili nakubaliana nalo.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine nataka nitofautiane na Kamati, isipokua naomba Kamati munielewe nini ninachokizungumza, kwa sababu nimetembea nchi nyingi kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna nchi ambazo visiwa vyao ni vidogo, lakini katika ufanisi na utaalamu mkubwa hua wanavitanua visiwa kwa kutumia kujaza na kusogea mbele, ili wanaleta kitu ambacho kilichokua na msingi na kinatia tija kwenye serikali na baadhi ya wenzetu wamefanya Mhe. Spika.

Historia ya Maruhubi Mhe. Spika, miaka mingi iliyopita pale mimi nilikua nikihangaika sana, yaani kulikuwa na miembe wakati ule tulipokuwa tukicheza muziki, enzi zetu zile kulikuwa na Ukumbi wa *Dance* si kama unakumbuka wakati huo. Sasa ukiangalia mazingira ya wakati ule na hivi sasa, basi hivi sasa ni mazuri, yaani ni sehemu nzuri Mhe. Spika tuseme haya na yale, sasa utaratibu gani mwengine siwezi kujua.

Lakini nasema kwamba mazingira ya hivi sasa ni mazuri sana, hivyo niseme tu *well and good* kua hali kama ile imefanyika. Je, tujiulize masuala ya utendaji wa biashara unakwenda au vipi hapa naomba tungeliangalia na hili tuliseme ukweli kutokana na hali halisi.

Vile vile eneo jengine Kizingo wakati nilipokuwa kijana nilikuwa nikienda mbio na kuparamia yale mabonde ilikuwa ni kitu ambacho ni tofauti. Lakini leo tukiangalia mandhari ya pale, kwa mfano China kuna majengo ambayo yako juu ya milima kwa makusudi ya kutafuta makaazi pamoja na tija ya serikali.

Mhe. Spika, suala hili naomba nikubaliane nalo, kwa sababu Kamati na wao hawakuwa wakali sana kwa hili, basi hilo niseme ipo Haki ya Binadamu ya kuangalia kuibadilisha mandhari, kwa ajili ya kuleta tija kwa wananchi pamoja na serikali kwa jumla.

Katika hili kutokana na *science* yangu ilivyo basi ningeomba kabisa suala hili na mimi wala sina tatizo nalo hapa, kwa sababu kuna kitu ambacho kimeekezwa pale na kitaleta tija kwa faida ya kuwasaidia wanyonge, ili kuweza kupata dawa pamoja na mambo mengine.

Suala la kuharibu mazingira inategemea, kwa sababu kuharibu mazingira kuna namna nyingi Mhe. Spika. Kwa kweli suala ambalo ni baya zaidi mtu kuingia kwenye bahari na kwenda kujenga *jetty* hilo ndio kosa, kwa sababu *jetty* inakwenda kuharibu mazingira ndani ya bahari yenyewe. Suala hilo nalipinga vikali sana na wala sikubaliana nalo. Mhe. Spika, hilo niseme ukweli hali halisi ilivyojitokeza hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliomba muda mkubwa sana lakini kidogo hali yangu haijawa nzuri. Kwa hivyo, nakubaliana na Kamati hii pamoja na kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, naomba kukaa kitako tumbo linaniuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu kukushukuru kwa dhati kupata nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati Teule.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia ripoti hii nichukue angalau dakika mbili tatu kwa ajili ya kuelezea machache tu, kwa mnasaba wa hali halisi.
Mhe. Spika, kwa yale ambayo Mwenyezi Mungu alinipa mtihani na kipindi kirefu sijaweza kusimama. Lakini nichukue fursa hii kukurushu wewe Mhe. Spika kwa imani yako na jitihada zako pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika kunisaidia hali yangu na kuweza kurudi na leo hii nikiwa hapa imara katika kuchangia kwa ajili ya kuwawakilishi wananchi wa Jimbo la Kwahani. *(Makofi)*

Vile vile niwashukuru wananchi wangu kwa jitihada na dua kubwa ambazo walizokuwa wakiniombea wakati nilipokuwa kitandani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukue fursa hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati Teule. Kwanza kabisa napenda kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wa Kamati Teule kwa kazi kubwa walioifanya yenye ufanisi mkubwa, yenye upeo pamoja na malengo ya kusaidia nchi yetu katika mustakbali mzima wa kimaendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Serikali yetu ya Awamu ya Saba chini ya utaratibu wa Muundo wa Umoja wa Kitaifa, chini ya Kiongozi wetu Jamadari Rais wetu mpendwa, muadilifu, mwenye hekima na busara Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. Tunaimani kwamba jitihada zake anazozionesha, basi na sisi tutamuunga mkono, ili kuhakikisha hatma, haki za wananchi, maendeleo yao yanapatikana kwa haraka katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme kwamba taaluma mnazotupa, basi tunafikia pahala tuanze kuzitumia. Kwa kweli mumetupeleka shamba kwa muda mrefu sana na mkatupa zana nzito sana. Sasa nafikiri ni vyema sote kuzifanyiakazi zana hizi kwa uadilifu na haki kabisa.

Kwa kweli michango yangu mimi ni minne kwenye kitabu chote hiki. Mchango wangu wa kwanza nizungumzie kuhusu suala la ajira. Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar kifungu cha 21(4) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 21(4) kinaeleza hivi:-

> "Kila mtu, bila ya kuwepo kwa ubaguzi wa aina yoyote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na watu wote wafanyao kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi ya sifa ya kazi wanayoifanya".

Mhe. Spika, hii inaonesha masikitiko kabisa kwa baadhi ya viongozi kutokuitii Katiba na kuitendea haki, kwa kuanza kuiendea kinyume na kufanya mambo yasiyostahiki Mhe. Spika, kwa kweli suala hili litawapa unyonge wananchi wetu. Kwa hivyo, sisi kama watunga sheria, wasimamizi wa sheria hizi tunaanza kuzivunja kwa makusudi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kitabu kimeelezea namna ya ajira zilivyofanyika pasipo na utaratibu, ambazo zinaonesha kuwa na upendeleo wa dhati, yaani ajira ambazo zinaonesha kwamba wakulima na wakwezi hawana haki katika nchi, lakini wale watoto wa viongozi ndio wenye haki ya kuajiriwa. Kwa kweli haya yanatia unyonge tena yanatusikitisha sana. *(Makofi)*

Sasa wakati wananchi wetu wanapotufuata kwa sifa zao kutaka tuwasaidie na serikali inapotangaza mambo haya utasikia ajira hakuna, lakini hatimaye mambo ndio kama haya Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika hili waliohusika imani yangu, kwa sababu serikali hii ni sikivu Mhe. Rais wetu makini, mawaziri wake waadilifu, basi imani yangu kwamba Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora atalifanyiakazi kwa haraka sana suala hili. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu mambo yaliyozungumzwa ya mali ambazo hazikufuata uadilifu, mikataba ambayo haistahiki, kwa kweli ni mambo ambayo yanatusikitisha sana na tunapata tabu Mhe. Spika katika hili.

Kila tunapokuja katika Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika, tunawapigia kelele mawaziri wetu kuhusiana na hali halisi ya nchi yetu, yaani wananchi wa nchi hii wanasikitika sana kwamba hali ni duni, tunapokuja hapa majibu ndio hayo hayo, kwamba tutajitahidi, tutafuatilia.

Vile vile tunagipa kelele kwamba maji hakuna, dawa hospitali kupatikana kwake mashaka, barabara zetu zina matatizo. Lakini mali za nchi hii baadhi ya wachache wanaziharibu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nna imani kwamba zingekuwa zinafanyiwa uadilifu basi matatizo katika mawizara yetu yangepungua na wananchi wa nchi hii angalau wangepata afueni wa yale matatizo waliyonayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Katiba yetu narudia tena ukurasa wa 13 kifungu cha 23(3) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 13 kifungu cha 23(3) kinaeleza hivi:-

> "Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kuwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya Taifa lao". *(Makofi)*

Mhe. Spika, narudia tena kwamba Katiba tunazo zinaelekeza pamoja sheria pia tunazo, lakini tunapata unyonge kama kwamba haya yaliyoandikwa humu yana ukweli, basi hali inasikitisha sana katika nchi yetu Mhe. Spika. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika sheria ifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Sasa niende kwenye ukurasa wa 27 wa kitabu chetu cha Kamati Teule kuhusu ulipaji wa fidia kwa watu ambao mali zao zimeathiriwa kutokana na ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, tunayo haki ya kusimamia Katiba, Sheria pamoja na Kanuni zetu, pia naomba tena nirudi katika Katiba ya Zanzibar kwenye ukurasa wa 10 kifungu cha 17(c) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 10 kifungu cha 17 na 17(c) vinaeleza hivi:-

> 17 "Hakuna mali ya mtu yeyote itakayochukuliwa kwa nguvu
> Hakuna maslahi au haki yoyote inayotokana na mali hiyo itakayochukuliwa kwa nguvu isipokuwa pale ambapo masharti yafuatayo yametimizwa, yaani:
>
> (c) Sheria imewekwa kuhusiana na umilikaji au uchukuaji huo kwa kutoa fidia inayolingana".

Mhe. Spika, katika kitabu hiki kinaeleza jinsi ya matatizo yaliyojitokeza katika uchunguzi wa Kamati Teule hii, fidia kutokulipwa kwa haki, taratibu hazikufuatwa katika kuangalia mali halisi za watu.Vile vile baadhi ya watu mpaka leo wanaendelea kudai fidia bado hazijalipwa na fidia zenyewe zimekasimiwa tangu miaka mingi na hali ya kimazingira ya nchi yetu ya thamani ya fedha inabadilika. Kwa hivyo, hofu tu ni kwamba huenda kwamba ule mlingano wa fidia usije kupatikana.

Mhe. Spika, nasema kwamba nimeingia zaidi katika suala la Kikatiba kuna hali gani tunatekeleza Katiba hii pamoja na kuisimamia kama sisi ni wasimamizi wa wananchi ambao wanatutegemea. Kwa hivyo, imani yangu kwamba yalioandikwa humu Mhe. Spika kama yatakuwa na ukweli wa dhati na kwa sababu tumehitaji baadhi ya vitu ambavyo ni vielelezo tuvipate kwa ajili ya kujiridhisha nafsi zetu katika haya. Kwa maana hiyo, niwaombe wasimamizi wetu watende haki katika haya na wale wote ambao wamehusika katika namna moja au nyengine, basi sheria zifuate mkondo wake kwa haraka, ili kutoa matumaini kwa wananchi wetu ambao wametupa ridhaa ya kura zao.

Mhe. Spika, kuna suala la Maruhubi limezungumzwa na Mhe. Mjumbe aliyechangia hivi punde ameelezea sana kwamba ametembea nchi nyingi na kuona mambo mengi. *(Makofi)*

Kwa kweli kama kutembea na sisi tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatutembeza sana Mhe. Spika, mara nyingi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nalishukuru Baraza la Manispaa limenipeleka nchi nyingi na kutembea ulimwenguni na kuona mambo mbali mbali na wala hatukatai mambo mengi Mhe. Spika yanafanyika na hata pale tunapouliza maswali basi huwa tunatoa mifano baadhi ya nchi za wenzetu jinsi zilivyopiga hatua. *(Makofi)*

Ah! Lakini kinachotakiwa Mhe. Spika ni kufuata taratibu za nchi na hilo ndio tatizo, kwa sababu usipofuata taratibu za nchi Mhe. Spika unaweza kuja kufukia bahari. Matokeo yake kwa sababu wananchi wetu wengine wamejenga mpaka baharini. Kwa mfano, Mhe. Spika kama utakwenda Saateni ukiimaliza *Nursery School*, basi kuna nyumba ziko chini ya mikoko. *(Makofi)*

Sasa kama taratibu hazikufuatwa Mhe. Spika na hali hii ya mabadiliko ya kimazingira ya ulimwengu, basi tunaweza kuja kuua watu siku za baadaye. Kwa kweli hatukatai Mhe. Spika watu kujenga na kufukia bahari, lakini kinachoelezwa humu ni taratibu, kwa sababu kuna taratibu hazikufuatwa. Mhe. Spika, hata hao watu ambao waliofukia walikuwa hawapaswi kumiliki hiyo ardhi kwa mujibu wa mambo ambayo yameelezwa humu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama utasoma ukurasa wa 125 kifungu cha 8 kinaelezea hali halisi nani amepewa eneo lile na alitakiwa alitumie vipi. Kwa hivyo, matumizi yaliyoainishwa kwa mujibu wa kupewa ardhi ile sio matumizi yaliyotumika na hilo ndio tatizo Mhe. Spika. Kwa kweli tunawapenda sana wawekezaji Mhe. Spika na tunataka wawekeze kwa faidi ya nchi hii. Lakini jambo la kusikitisha hata huo utaratibu wa kulipa leseni zenyewe kama utakisoma hiki kitabu, basi pia ulikuwa hautekelezwi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, imani yangu kwamba wachangiaji katika ripoti hii ni wengi sana. Lakini niombe tu katika kutaka kurejesha imani za wananchi wetu katika hali hii tutawaomba sana viongozi wetu na kama nilivyosema mwanzo kwa sababu tunayo imani kwamba ni viongozi wenye busara, mahiri ambao wanataka mabadiliko ya nguvu. Vile vile wametuelezea jinsi ya matumaini ya mabadiliko na kutaka kuelekea nchi hii, ili iweze.

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassa Hija: Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati Teule, nakuomba Mhe. Spika kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano asitoe maneno kwa Wajumbe wa Kamati atulie. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, sijakufahamu hebu rudia kuhusu utaratibu.

Mhe. Hija Hassa Hija: Mhe. Spika, huu ni wakati wa kusikiliza Ripoti ya Kamati Teule na Wajumbe wanachangia ripoti hiyo. Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Spika kwamba umuombe Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano asitoe maneno kwa Wajumbe wa Kamati na sisi tumenyamaza kimya na kazi yetu imekwisha awache kutusakama. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, alichokuwa akisema Mhe. Mjumbe tujaribu kuwa watulivu na tusikilize Wajumbe wakichangia ripoti hii. Sasa kama kuna mikutano mingine kweli hiyo itakuwa inaingiliana na shughuli yetu hii na wala si jambo jema. Mhe. Mjumbe endelea.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kumalizia yale ambayo nimekusudia kuchangia katika siku hii ya leo. Mhe. Spika, niseme kwamba nilikuwa nikimalizia kwa kusema kwamba imani yangu kwa viongozi wetu wa nchi hii kuanzia Mhe. Rais wetu, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mawaziri ambao wameanza kutuonesha imani ya dhati katika kusimamia

haki. Kwa hivyo, imani yangu kwamba wale wote ambao wameguswa kwa namna moja au nyengine katika ripoti hii, basi hatua za serikali katika kuwapa imani wananchi wa nchi hii, nna imani kwamba zitatendeka tena kwa haraka sana.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo naomba kuunga mkono ripoti hii na kutaka waliohusika wachukuliwe hatua kwa mujibu wa utaratibu wa sheria za nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa fursa hii leo. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha hapa leo kwa ajili ya kuichangia Ripoti ya Kamati Teule.

Mhe. Spika, kwanza naipongeza Kamati yetu hii Teule kwa kutafuta ukweli na kutuletea ukweli ambao uliomo katika mawizara pamoja na maidara yetu. Mhe. Spika, Kamati hii mimi naiombea dua Mfunguo Tatu wote waweze kwenda Makka, kwa sababu ni watu ambao ni wa kweli na wala hawana woga kwa yale waliyoyakuta. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wangu utakuwa wa jumla. Kwa kweli hivi sasa lazima tubadilike, kwa sababu Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa inaangaliwa na wananchi wote nini tunafanya. Ukweli wa mambo ni kwamba Kamati Teule imetuletea watu ambao wanaohujumu uchumi wa nchi. Mhe. Spika, kilichobakia hivi sasa ni kuwa serikali iwajibike kwa watu hawa, kwa sababu uchumi wa nchi unanyang'anywa na watu ambao wanapenda madaraka kwa ubinafsi, kwa hivyo serikali naiomba iwachukue mara moja watu hawa na wahukumiwe.

Mhe. Spika, hapa tumeweka sheria ya mazingira ya bahari ili ndugu zetu wavuvi wanyonge leo tunawakamata kwa kuharibu mazingira, lakini tunashindwa kuwatia ndani na kuwahukumu wanaohujumu uchumi wa nchi katika mawizara yetu kwa nini. Mimi naiomba tena serikali iwajibike tena watu hawa wakamatwe mara moja.

Mhe. Spika, naiomba serikali wakati kamati zetu hizi mbili zinapokwenda kufanya kazi wapewe maaskari PAC na Kamati Teule wapewe maaskari ili wakihakikisha ushahidi upo mtu anatiwa pingu na anapelekwa Mahakamani, mnyonge muiba ndizi moja ya pukusa anakamatwa anapelekwa Mahakamani anasomewa sheria na jaji, kwa mujibu wa kifungu nambari sita mabano sita nakutia ndani, anafungwa miaka mitatu halafu anaambiwa kwamba fundisho kwa wenzako. Lakini katibu wa fedha anaiba fedha milioni thalathini hakamatwi anakwenda kubadilishwa Wizara badala ya kupelekwa fedha anapelekwa Uwanja wa Ndege maana yake ndio akahujumu zaidi, lakini mwizi wa ndizi anapigwa miaka mitano anaambiwa fundisho kwa wenzako.

Mhe. Spika, tunaiomba serikali iwajibike kwa watu wanaohujumu uchumi katika mawizara, tunawavunja moyo wananchi kwa kuwa wakubwa hawahukumiwi mimi sijasikia hata siku moja kuhukumiwa mkubwa aliyehujumu nchi hata siku moja hatujawahi kusikia, sijapata kusikia kwamba mkubwa kadhulumu uchumi wan chi akapelekwa katika Mahakama wanaopelekwa kwenye Mahakama ni wale wale waiba ndizi, kuku lakini aliyehujumu wizara au serikali hapelekwi katika Mahakama kwa nini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi kwa kuchangia kwangu katika ripoti hii imeelezwa wazi na bila ya wasi wasi wowote na haikuficha kitu, waliouza viwanja, waliopewa mishahara hewa wamo, wote hawa wamehujumu uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, serikali iweke mazingira ndani ya mawizara, kama tulivyofanya mazingira ndani ya bahari, misitu na ndani ya wizara yaweko mazingira uletwe mswada hasa, wa kuweka mazingira safi katika mawizara kwa sababu uchumi wa nchi unahujumiwa sana na tunaohujumu uchumi ni sisi wakubwa, wakubwa hatuhukumiwi kwa nini wanahukumiwa wadogo tu. Kwa sababu dasturi ya jiti kubwa likikatwa haliangukii kwenye mti mkubwa huangukia kwenye mti mdogo.

Sasa na sheria zetu zote tunazozitunga haziwakamati wakubwa na wakubwa ndio wanaohujumu nchi, kwa hivyo Mhe. Spika, mimi sina maneno makubwa kutokana na ripoti yetu hii ya kamati teule, nasisitiza tena Mhe. Spika, kamati teule inapopewa kazi wapewe na maaskari wanapohakikisha kwamba huyu mtu ushahidi tayari upo pale pale atiwe pingu apelekwe Mahakamani tumsikie. Kwa hivyo, bila ya kwenda mbali naunga mkono ripoti hii mia kwa mia ahsate sana. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pili pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema hii leo asubuhi. Niwapongeze kamati teule kwa dhati ya moyo wangu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa kweli kwa kuwa ni utaratibu tu kuchangiwa ripoti hii

lakini ilikuwa haina haja ya kuchangiwa, kwa sababu kila kitu kinajionyesha wazi katika yale ambayo yamezungumzwa humu basi mengi yao yamo humu na wala hamna vificho.

Lakini pia niwapongeze kwa dhati baadhi ya mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa mara ya kwanza jana kuunga mkono juu ya uundwaji wa kamati teule ya Baraza la Wawakilishim, kwa ajili ya kuchunguza Baraza la Manispaa ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijazungumza chochote kwanza nitoe tahadhari kwa serikali yetu hii ikiwa hatiokuwa makini kuna hatari kubwa ya kila kikao kuundwa kamati teule ya Baraza, na madhara makubwa ya kamati teule ni kama haya, lakini pia kamati teule zinapelekea kupotea kwa pesa nyingi sana kwa serikali kwa hivyo natoa tahadhari ama wito kwa serikali ijitahidi kufanya kazi zake kwa uadilifu, ama si hivyo serikali hii itazidi kufilisika iwe haina pesa kwa sababu ya kamati teule za Baraza la Wawakilishi hilo la kwanza.

Mhe. Spika, kabla ya kuingia katika ripoti yetu naomba ruhusa yako niinukuu katika baadhi tu ya vipengele vya katiba tu ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha tisa mbili (b) kinazungumzia hivi .”Usalama wa hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali ya Mapinduzi “.

Kifungu cha 10 kinazungumzia malengo ya kisiasa Kifungu (c) hapa kinazungumza hivi. “ Itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuondosha kabisa vitendo vya rushwa, utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wele wote walio na madaraka”.

Kifungu cha 12 kinazungumzia usawa mbele ya sheria na hii watu wote ni sawa mbele ya sheria.

Kifungu cha 10(h) kinazungumzia “vyeo vyote na madaraka ni dhamana kwa manufaa ya umma”.

Kifungu cha 17 kinazungumzia “ hakuna mali ya mtu yoyote itakayochukuliwa kwa nguvu na ikiwa hakuna maslahi yoyote yanatokana na mali hiyo itachukuliwa kwa nguvu”.

Lakini vile vile Kifungu cha 21 kinasema “Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii sheria za nchi za Zanzibar”. Kifungu cha 23 kinasema “ wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa taifa”.

Kifungu cha 23(ii) kinasema “Wajibu wa kutii sheria za nchi kulinda mali ya umma”.

Kifungu cha 23 (2) Kila mtu ana wajibu kwa kulinda maliasili ya Zanzibar, mali ya wananchi, mali ya nchi na mali inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi pia kuheshimu mali ya mtu mwengine.

Mhe. Spika, vifungu hivyo vinatosha kabisa tukiwacha vyengine vingi ambavyo vimo kwenye katiba hii kuweza kumtia hatiyani mtu moja kwa moja, yeye mwenyewe bila ya kuambiwa fanya hivi sasa hivi ama vipi, kwa sababu hii katika katika vifungu hivi mimi naamini viko wazi na vinafahamika Mhe,Spika.

Baada ya kusema hayo sasa niingie moja kwa moja katika ripoti ya kamati, mimi nitachangia mambo matatu manne tu, la kwanza kuhusu uuzaji wa mali za serikali kinyume na utaratibu hapa kuna viwanja viwili vimeuzwa, kiwanja cha Mawasiliano na kiwanja kimoja ambacho kipo Mbuyu Taifa pale kinyume kabisa na utaratibu kwa mujibu wa kamati teule, kwamba mtu mwenyewe binafsi serikali haikuuza hapa lakini mtu mwenyewe binafsi kwa matamanio yake tu anachukua mamlaka ya kuuza kitu cha umma au cha watu wote wa Zanzibar ukweli hii ni hatari kubwa sana.

Kwa hivyo yeye mwenyewe asisubiri kuwajibishwa mtu kama yeye mwenyewe anaweza kuwajibika mwenyewe mimi nahisi moja kwa moja awajibike yeye mwenyewe asisubiri kuwajibishwa na mtu, kwa sababu sheria na taratibu ziko wazi katiba hii iko wazi moja kwa moja na inaonyesha ubaya ambao umefanyika katika suala hili.

Suala la pili kwa haraka haraka Mhe. Spika, ni suala la ajira sisi kama vijana huku nje tunao vijana wengi wamemaliza degiree ya kwanza, wamemaliza Masters wana diploma na wana sifa nyengine nyingi tu ambazo wao wapo hapa kwa ajili ya kungoja foleni ya kuajiriwa, cha kusikitisha Mhe. Spika, katika awamu hii juzi sheria ya utumishi wa umma tumepitisha hapa katika baraza lako tukufu kwa makofi na vigelegele, kwamba tunaweka utaratibu mwengine mpya sasa wa kuweza kuajiri watu. Kitu cha kushangaza ajira hazikufuata utaratibu likiwemo moja upendeleo au ubinafsi uliofanywa na baadhi ya watendaji wetu na viongozi wa juu wa Wizara, jambo hili hatuwezi kulivumilia kwa sababu watu wengi wako huko na wana sifa na wanataka ajira katika nchi hii hii.

Mhe. Spika, nchi hii imefanya Mapinduzi mwaka 1964 kwa ajili ya kuwakomboa wakwezi na wakulima ndio wenyewe hasa nchi hii, kwa wakati ule watu wengi walikuwa hawajasoma lakini hii wamesoma na wana sifa za kufanya kazi, hili Mhe. Spika, hatutoweza kulivumilia taratibu za sheria zifuatwe katika masuala haya.

Mhe. Spika, jengine suala la ulipwaji fidia kwa watu ambao wamepata madhara katika ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege pale, hii ni hatari huu muda umekuwa mkubwa watu hawa wana rizki lakini kwa maslahi ya watu binafsi wao wenyewe wameamua kutokuwalipa watu hawa haki yao, wanaiachia serikali kulaumiwa na kuonekana serikali hii ni ya kudhulumu watu na hina sifa hizo serikali hii, serikali hii tokea awamu ya kwanza inajulikana wazi kwamba ni serikali moja adilifu kama serikali. Ikiwa mtu mwenyewe binafsi anafanya hayo hili hatutolifumbia macho Mhe. Spika, hatua zinazofaa zichukuliwe.

Mhe. Spika, la mwisho ujenzi wa jengo jipya la wizara ya Fedha kwa maelezo ya ripoti ya kamati hii taratibu za ujenzi huu hazikufuatwa, mmezungumzwa kuhusu ununuzi wa vifaa haukufuata taratibu na watu ambao wanahusishwa humu ni waziri pamoja na watendaji wake wengine, kwa hivyo Mhe. Spika, tunaomba sana ikiwa waziri aliyekuwepo wakati huo alikuwemo humu leo hapa anatusikia na ripoti anayo ameshaisoma, kwa hivyo yeye mwenyewe kama yeye aamue kwa hiyari yake mtu asisubiri Mhe. Rais afanye hivyo tutakuwa tunamuongezea kazi. Lakini sheria ziko wazi mtu awajibike yeye mwenyewe kwa mujibu wa utaratibu.
Mhe. Spika, nakushukuru sana baada ya hayo mimi naomba nikae kitako niwapishe wenzangu waendelee na mchangio huu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia kamati teule ya Baraza la Wawakilishi, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu subuhana llahu wataala aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema na kuweza kusimama katika baraza lako tukufu hili kuweza kuchangia kamati teule hii.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuipongeza kamati teule ya Baraza la Wawakilishi iliyofanya kazi zake kwa uadilifu sana, kamati hii imefanya kazi kwa muda mfupi sana lakini imefanya kazi nzuri na imeleta ripoti yake hapa bila ya wasi wasi wowote kwa hivyo tuwapongezeni sana wana kamati wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mwenyekiti wa kamati hii aliyewasilisha amewasilisha kwa umakini kabisa bila ya woga na bila ya kujali kama ni nani aliyefanya makosa, Mhe. Mwenyekiti nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kuipongeza kamati hii naipongeza kwa mambo ya misingi kabisa, kamati hii imeona mambo na haikuwaficha imeyatoa baana katika chombo hiki kitukufu cha baraza lako tukufu, kazi ya kamati ilikuwa ngumu kuna kwengine walipata mashirikiano na kwengine walikosa ushirikiano kwa kutoelezwa bayana. Lakini walijitahidi na Mwenyezi Mungu kawajaalia wamefanikisha azma yao hii ya kuchunguza nawapongeza sana kamati.

Mhe. Spika, baada ya kuwapongeza kamati niseme tu katika nchi yetu hii ya Zanzibar na serikali yetu ya Mapinduzi yenye sura ya umoja wa kitaifa wananchi wanaitegemea sana na wanaiamini, lakini niseme haya yanayayozungumzwa na waheshimiwa wawakilishi tukiwa hapa barazani na yale yanayoletwa na kamati basi ni lazima yafanyiwe kazi, tunaishauri serikali kama maoni yaliyotolewa na kamati na mapendekezo yaliyoletwa pale yafanyiwe kazi. Kwa sababu hiki ndicho kipimo cha wananchi wetu tunapokuta mambo maovu ndani ya mawizara na Maidara kama tutafanya kazi kama alivyozungumza Mhe. Mosi pale kama mtu anaiba kuku anakwenda kufungwa miezi sita au mwaka na anaambiwa ni fundisho kwa wengine.

Lakini mtu anaiba mamilioni ya fedha anaachiliwa anaendelea kuiba tu hili sio jambo jema tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu ambao tunawaongoza, na serikali hii inaongozwa kwa mujibu wa katiba na sheria.

Mhe. Spika, kumekuwa na dhambi kubwa ya upendeleano na ubaguzi hivi sasa katika mawizara yetu na maidara tunafanyakazi kwa upendeleano ikiwa huna mtu ndani ya idara zetu basi huwezi kufanikisha jambo lolote utabaki kule kuja, msifikirie kama wakulima wanaolima hawana elimu wale wana elimu ya kutosha lakini hawana ile ajira. Wasifikirie wavuvi wanaovua ukafikiria hawana elimu wana elimu ya kutosha lakini hawana ajira.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 202 mwanafunzi aliyeajiriwa akiwa mwanafunzi na kuna watu wenye elimu ya degree eti hawajapata kuajiriwa hata siku moja jambo hili linawavunja moyo wananchiwetu, ni jambo la kutizama kwa kina. Sasa Mheshimiwa tunasema maoni yote yaliyotolewa na kamati ukipatikana ushahidi basi

naiomba serikali iwafanyie kazi, kwa sababu hiyo ndio itakuwa serikali makini na yenye kujali wananchi ambao watakuwa na matumaini makubwa katika nchi yao.

Mhe. Spika, kwa kweli dhambi hii ya upendeleo na kujuana imo katika Mawizara na Maidara na hii itaendelea kuwepo kama haijafanyiwa kazi, haya yanafanywa kila pahala hapa iliyolengwa ni Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Ardhi na Makaazi lakini nafikiri kama wizara zote kama zitachunguzwa basi kutakuwa na zaidi kuliko haya. Naiomba serikali ifike pahali ifanye kazi kwa makini ili kuwapa moyo wananchi wake, nathubutu kusema ndani ya baraza hili tukufu kuwa nchi yetu haitafikia maendeleo kama tutawaonea aibu hawa waliofanya ubadhirifu huu hata siku moja, na kama tutawafanyia kazi hawa basi baada ya muda mfupi nchi yetu itakuwa na maendeleo kwa sababu sasa hivi kila mtu anayewekwa sehemu yake anajikidhi haya yake yeye na jamii yake.

Kwa nini hununui gari la kwako ukawa dereva wewe mwenyewe na mtoto wako akawa tingo na mpokea fedha akawa mjukuu wako, lakini katika mambo ya umma basi watu wote wapate haki zao za kimsingi, hapo tutakuwa na jambo ambalo kuwa limetujenga kwa dhati kabisa na wananchi watakuwa na moyo na watafikia pale tulipokusudia. Mambo haya yote yamakuja kutokana na mambo ya kisiasa tu.

Nasema namnukuu Mhe. Asha Bakari makame alivyosema kama ni siasa tumeshaicheza zamani uliobakia ni mshikamano wa pamoja Wazanzibar kuweza kufanya kazi kwa pamoja na kuiletea nchi yetu maendeleo, isiwe kila siku tunaanza tu lakini hatufiki na kama tutakuwa tunaanza hatufiki tunakuwa tunatwanga maji katika kinu, tutakuja hapa barazani kuzungumza hatima yake hakuna hata moja linalokuwa. Hili ni jambo la aibu na fedheha imefikia wakati hawa waliofanya mambo kama haya kuitwa mafisadi na sio kuitwa mafisadi tu wakishaitwa mafisadi wachukuliwe hatua za kisheria na wawajibike, bihairi ya hivyo tutakuwa hatufiki tunakokwenda.

Mhe. Spika, elimu haina thamani kwa nini niseme hivyo, elimu haina thamani kama nilivyotoa mfano hapa kama watu wanafanya kazi kwa kujuana na kama wanafanya kazi kwa kujuana mnyonge siku zote atakuwa hana haki, na nchi hii ni ya wanyonge ya wakulima na wakwezi. Lakini mpaka leo hatuwajali iko siku itafika ndani ya ofisi yetu kutatokea msiba basi ofisi itafungwa kutokana na watu kuajiriana kwa kujuana, kwamba wote watahusika na msiba ule na ukenda ofisini hakuna matu kwa sababu kumetokea msiba.

Mhe. Spika, naomba tuangalie na kulipa kipaumbele jambo hili kamati hii mimi niipongeze sana, Mheshimiwa kaiombea dua kwamba wajumbe wa kamati hiyo wote waende Makka katika msimu huu, nami nasema Mwenyezi Mungu awajaalie waende Makka kwa sababu wamefanya mambo kwa uadilfu kabisa kabisa bila ya kujali huyu ni nani na huyu ni nani, huyu ana wadhifa gani na huyu ana wadhifa gani wametoa ripoti yao kwa ukamilifu kabisa. Na sisi tipori hiyo tunaiunga mkono kwa moyo mkunjufu kabisa.

Sasa tukienda katika ajira kunakuwepo ajira hewa jambo hili linasikitisha sana na linakatisha tamaa wananchi wetu, mtoto wa masikini anasoma mpaka anafikia malengo lakini hatima yake anabakia pale pale anakuwa hana kazi lakini watu wenye uwezo ndio wanaopewa kazi hizo, hili ni jambo la aibu kweli kweli.

Halafu sasa Mhe. Spika, misaada hewa nayo kuwepo unaweza kuambiwa hapa tumetoa misaada kwa kikundi hiki na hiki lakini mtu akawa anayetoa misaada ile ikawa na yeye yumo katika hisa pale, walengwa haiwafikii misaada hii. Imefika wakati kufanya jambo linaloeleweka na wananchi wetu wakapata msada na serikali ikapata tija na kuweza kuendesha serikali iliyo makini.

Mhe. Spika, kama atulivyozungumzia katika mambo ya huduma ya afya mnyonge anaweza kwenda kupanga foleni mpaka akashindwa kupata kwa sababu hajuani na mtu yoyote, hamjui daktari hamjui mpimaji, unaweza kumuuliza mtu vipi mtoto huyo anaumwa vipi unampeleka hospitali hata ukimpeleka hapati dawa ni kukata tamaa kwa sababu kila aneyekuja pale anapewa huduma kwa kujuana hili ni jambo la aibu na fedheha katika nchi yetu. Tumefika wakati Wazanzibari tumeshikamana tufanye kazi kwa pamoja, siku zote mimi nazungumzia jeshi likigawanyika halishindi vita hata siku moja lakini tukiwa wamoja hakuna tusiloweza kulifanyia kazi na kupata tija na maendeleo yanayokubalika.

Mhe. Spika, yapo mengi ya kuzungumza lakini mwisho niseme tu ukitaka kumuuwa nyani usimuonee haya, usimuangalia usoni ukimuangalia usoni jinsi alivyo atakutia huzuni na hutoweza kufanya kazi yako uliyokusudia. Kwa hivyo nasema na natoa wito kwa serikali yetu hii watu wote waliokutwa na mambo machafu basi wachukuliwa hatua za kisheria na nidhamu ili iwe fundisho kwa watu wengine na wizara zote ziwe zinafundisha hayo. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia neema zake za uhai na uzima asubuhi hii tukakutana hapa tukiwa tunajadili ripoti ya kamati teule ya baraza lako tukufu, iliyoundwa kuchunguza mambo mbali mbali ambayo yamejitokeza wakati wa kikao au wakati wa Mkutano wa bajeti wa mwaka jana.

Mhe. Spika, hatua iliyofikiwa ni hatua kubwa sana kwa sababu chombo hiki ni chombo ambacho kina wajumbe waliochaguliwa na wananchi ili kusimamia serikali, kwa hivyo ni jukumu lake kabisa la kikatiba pale inapoona kwamba kuna harufu ya ukiukwaji wa taratibu za kisheria au za kiutawala kuingilia kati kwa niaba ya wananchi na kuchunguza masuala yale na baadae kuleta mapendekezo yake hapa katika chombo hichi.

Mhe. Spika, kwanza mimi niungane na wenzangu kuwapongeza sana wajumbe wa kamati teule kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, ilipokuwa inawasilishwa jana hapa ripoti hii ulikuwa unajua tu kwa ule muhutasari kwamba kazi kubwa imefanyika, baadae ukipitia hichi kitabu chenye ripoti hii ambacho kina maelezo ya kina juu ya kila kadhia katika zile kadhia jumla yake nadhani ni nane (8) zilizochunguzwa naambiwa tisa, lakini unajua kwamba kazi kubwa imefanyika.

Lakini pia jana Mhe. Spika, nilinyanyuka kuomba kwamba tupatiwe vile vielelezo mbali mbali ambavyo walivitaja katika muhtasari wao ili tuweze kujiridhisha kabla ya kujadili, bahati mbaya naona hilo limekuwa gumu lakini nilibahatika kutoka kwa mmoja wao kupata sehemu ya vielelezo hivyo na vimenisaidia angalau kuweza kupitia baadhi yao.

Mhe. Spika, sasa baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, nilikuwa na mimi nizungumze machache yaliyojitokeza katika ripoti hii, katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 69 (iv)(a) kinazungumza "ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo, au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na ilivyokusudiwa madaraka hayo".

Mhe. Spika, kifungu hichi kinaweka wazi au kinatafsiri ile dhana ambayo tumezoeya kuizungumza sana kwamba cheo ni dhamana, kama cheo ni dhamana maana yake ni kwamba tukitumie kwa yale makusudio ambayo yametolewa, sasa uchunguzi uliofanyika Mhe. Spika, unaonyesha katika maeneo mengi kwamba baadhi ya watu ambao tumewakabidhi dhamana ya uongozi walishindwa kusimamia uadilifu wenywe dhamana ambayo tumewapa. Jambo hili kama walivyosema wenzangu linaleta athari mbaya katika nchi, viongozi katika nchi yoyote ni kioo cha jamii, viongozi ni taathira ya nchi kwa nchi nyengine katika ulimwengu na mara nyingi wananchi wetu au wananchi wan chi hii huwa wanatazama viongozi wao.

Viongozi wanapokuwa safi Mhe. Spika, basi na wananchi mara nyingi nao utawakuta wako safi, lakini viongozi wanapokuwa wachafu hawafuati taratibu zilizowekwa na wananchi hawapati moyo na wao kuzifuata taratibu zilizowekwa. Kuna usemi wa wanasalsafa mara nyingi wanasema jamii siku zote inapata viongozi kwa mujibu wa ile jamii yenyewe ilivyo, sasa hili ni funzo kwentu Zanzibar tujitizame tumeteleza wapi kama jamii hata kufika pahala tumepata viongozi ambao wanashindwa kusimamia yale ambayo nimeyataja ndani ya katiba.

Mhe. Spika, katika ripoti hii tukisema tujadili moja moja muda hautotutosha lakini mimi kuna baadhi ya mambo machache nilikuwa nataka niyatolee maoni.

Mhe. Spika, kwanza nimejifunza katika hili naomba sana viongozi wetu hasa Mawaziri, wanapokuja katika chombo kikubwa kama hichi, zile taarifa ambazo wanatutolea hapa wawe na uhakika nazo.

Mimi naelewa kwamba sisi sote ni binaadamu hatuwezi tukawatabiria mawaziri kuwa na nguvu kubwa ambayo hata sisi hatuna. Huwezi ukajua kila kitu lakini nadhani si dhambi wala si kosa, wala si aibu kuulizwa jambo ukasema hili sina taarifa nalo, nalifatilia halafu nitakuja kuleta taarifa Barazani. Ninachokiona hapa mara nyengine unakuja utaratibu kwamba unakuwa na jawabu la kila unaloulizwa au utetee kile kinachofanywa na watendaji wako. Matokeo yake kwa sababu wewe ndiye unayewajibika katika Baraza hili utapobeba mzigo ule na madhara yake yatakuja kukuta wewe.

Mhe. Spika, kule Mjimkongwe kuna Shekhe mmoja wamembadilisha jina mpaka wanamwita Shekhe Kuba kwa sababu kila analoulizwa yeye ana jawabu hapo hapo. Hakuna hata siku moja alosema kwamba hili hebu niachieni nikafungue vitabu kidogo. Sasa Mhe. Spika, isijekuwa na Mawaziri wetu ikawa kama Shekhe huyu.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo yametajwa humu ukiyatizama ni mambo ambayo yalikuwa madogo tu mengine, lakini yamekuja kwa sababu mwuheshimiwa alipoulizwa alijibu bila ya kulifanyia utafiti. Leo kamati inafika kusema kwamba umelidanganya Baraza ni kwa sababu ungekuweza kujibu kwamba hili nalichukua

ngojea nikalifanyie utafiti. Kwa hiyo nasema hilo moja nimeligundua nilikuwa naomba sana tujirekebishe Mhe. Spika.

Pili nimejifunza kwamba na imezungumzwa hapa katika muhtasari kwamba kuna matumizi yanakuwa yameidhinishwa na Baraza hili kwa mujibu wa Katiba hii, ndilo pekee lililopewa dhamana ya kusimamia fedha za walipakodi na matumizi yake. Madhumuni ya kuwa na vikao virefu vya bajeti, tunapokuja hapa tukakaa tukaumisha vichwa, tukapigishana kelele katika vifungu, tukapigishana mabuti katika vifungu humu mpaka wengine wakataka wakataka kuanguka ni kwamba tunataka tupate usahihi wa matumizi ya fedha za wananchi.

Sasa tukifika baada ya kazi yote ile kuwa tumefika pale yale mambo ambayo yameidhinishwa na Baraza hili basi tuyaheshimu. Najua kunatokea taratibu mara nyengine inapelekea kuhaulisha vifungu na ndio maana hata ile sheria tunayoipitisha mwisho pale ya *appropriation bill* inatoa nafasi kwa Waziri wa Fedha kuhaulisha vifungu. Lakini ikifanyika hivyo zile dhamira ambazo zimekusudiwa sio kwa mambo mengine madogo madogo ambayo matokeo yake yanakuja kuonesha aibu kama ambayo imeone katika ripoti hii iliyotajwa kadhia yake.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima lililojitokeza katika ripoti hii ni juu ya kuheshimu sheria na kanuni za matumizi ya serikali au matumizi ya umma. Hili limejitokeza kila pahala. Mimi naomba sana kwamba hili tujifunze. Napata wasi wasi kwamba watendaji wetu, haya mengine mimi siwabebeshi Mawaziri ingawa mawaziri ndio wanaowajibika hapa. Hasa mawaziri wanapokuwa hawasimamii watendaji wao wabeba mzigo uliokuwa si wao.

Mhe. Spika, kuna kitu nilikuwa sijawahi kukisema lakini leo nitakisema. Nilivunjika moyo sana mwaka jana, tulikaa humu ndani mmoja mimi niliyezungumza sana juu ya mitambo ya televishen kuletwa kwa jina la mtu binafsi. Utadhani baada ya kulisema katika chombo hichi kwamba itakuwa fundisho sasa mtindo kama ule uwachwe, lile tuseme limeshatokezea tumedai maelezo tumepewa. Lakini nakuhakikishia Mhe. Spika, baada ya kile kikao cha Bajeti siku moja niko Uwanja wa Ndege na mimi naeleweka huwa sisafirii huku nipo huku huku kwa wananchi maana yake huku ndio unakoona mambo Mhe. Spika.

Niko pale kulikuwa na malalamiko mengi ambayo yaliyokuwa yakitolewa humu ndani kwamba lile eneo la wasafiri wanaosubiri kuondoka limekuwa na joto sana kutokana na kuwa halina *AC* nikakuta katika yale makelele yetu nafikiri kuletwa *AC* kubwa sio ma – *AC* yanayopaswa kuwepo katika maeneo kama yale lakini ndio katika hali ya kuchukua hatua ya kwanza kabla yatua zaidi hazijachukuliwa limeletwa pale, linafunguliwa nipo pale, nasubiri kuondoka. Lile plastiki lililofungiwa *AC* kubwa sana juu lina jina la mtu binafsi kwamba hii ni mali ya mtu binafsi, jina la mwanamke fulani mfanyabiashara. *Niaka-comment* pale pale nikaawaambia eeeh! hamjakoma tu. Wale watendaji wakacheka. Nimekwenda kidogo pembeni sasa narudi nakuta plastiki limeshachanwa. Sasa unachana wakati nimeshaona.

Sasa ninachosema tumefika pahala ya pa ile *impunity* kwamba Mhe. Spika, watendaji hata ule woga hawana kwamba limeshazungumzwa suala kama hilo basi tunategemea lisifanywe tena lakini baada ya muda unakuja kushuhudia suala kama lile. Utaratibu huu wa kutokuheshimu sheria hizi na kanuni tunazopitisha hapa za manunuzi ya umma unavunja moyo sana. Katika hili viongozi wetu watendaji hasa Wizara ya Fedha wachukue hatua za kujirekebisha.

Mhe. Spika, tunapiga kelele hapa kwamba leo imekuwa kila manunuzi lazima wasimamie Wizara ya Fedha. Usifikiri ni kwa sababu ya kutaka kulinda fedha za wananchi, kwa sababu ya kutafuta kamishen na kwa sababu ya kutafuta mapato yao binafsi mfukoni. Kamishen zinaruhusika katika biashara binafsi huko, huwezi kutumia cheo chako tulichokupa kwa mujibu wa katiba hii ukataka kutafuta kamishen kwa migongo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hili limetajwa mwahala mwingi lakni sitaki kulirejea mara moja moja bali nataka tuone tunachukua hatua ya kuzisimamia sheria hizi na watendaji wajifunze. Kwa sababu wasipochukua hatua hizo Mawaziri wanabeba kazi kubwa sana kubeba mizigo yao humu ndani. Mawaziri nao pia wawasimamie watendaji wao katika hili.

Mhe. Spika, katika hilo nililolisema limejitokeza katika ripoti hii, kuna watu wanaongoza nafasi fulani, halafu wanazitumia kujinufaisha wao. Imetajwa kesi humu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Unachukua eneo unakodi kwa US$ 200, halfau wewe unalikodisha kwa US$ 1000 moja. Hii si haki, kwa sababu pale pana *direct convince of interest*, hata kama ulikuwa unapo kabla hujawa Mkurugenzi basi tararibu ni kwamba ukishakupewa nafasi basi mambo mengine uyaachie au uchague moja, uwe mfanyabiashara au uwe mtumishi wa umma. Ukiwe mfanyabiashara tena wa sekta ile ile ambayo wewe umepewa kusimamia

lazima patatokea mgongano wa maslahi. Mhe. Spika, hili pia watendaji wajifunze, Baraza hili halitokubali tena sasa mambo kama haya.

Mhe. Spika, jengine lilojitokeza ni suala la uajiri, kama alivyosema Mhe. Hamadi. Baraza hili hili ndio lilopitisha sheria ya Utumishi wa Umma mwaka jana. Tukasifiwa sana humu ndani kwamba kuanzia sasa na tangu miaka ya nyuma hapajakuwepo nchi hii sheria ya khusu Utumishi wa Umma, sasa tunaanzisha sheria ya Utumishi wa Umma. Tulizani kwamba tutaanzisha sheria ile, ambayo wengine tulipiga kelele kwamba inanyang'anya madaraka ya baadhi ya taasisi zetu. Tukaambiwa unawekwa utaratibu mzuri sana. Tukadhani tuliowapa dhamana ya kusimamia suala hili watalisimia vizuri. Leo Mheshimiwa humu kuna majina zaidi ya 70 nadhani kama siku zile 32 Unguja, 37 Pemba, watu walioajiriwa kinyume na taratibu.

Mhe. Spika, imefika kutajwa mpaka Mawaziri Wakubwa inafika pahala mpaka tunaingilia taratibu za kuajiri. Matokeo yake ndio unakuja kumuacha mtu mwenye sifa unachukua jamaa yako unampeleka kwenye nafasi. Hawa tunaowasomesha kila siku, watapata lini ajira. Kila siku tunalalamika hapa jinsi utandaji wetu unavyoshuka kwa kuwa na watendaji ambao hawana sifa, watendaji wabovu. Tukiendekeza uajiri wa namna hii Mhe. Spika, nchi hii haitosongambele maisha.

Mhe. Spika, wakati fulani Zanzibar ilikuwa ni mfano katika Bara la Afrika katika *professionalism* ya *public service*, kuna tendaji tumewatoa kutokana na misukosuka ya kisiasa wamekwenda katika nchi za watu wanatumika katika nafasi kubwa kubwa. Wamekwenda kuwa ma- *Vice Chancellor*, wamekwenda kuwa Wakurugenzi. Nchi hii imetoa mtu Dokta Abdulrazak Gurna ni Mzanzibari, yeye ndio Mkuu wa Kitivo cha Kiingereza katika *University of Kent*, nchini Uingereza. Kwamba yeye kawazidi kaweza kuwapita wao kwa somo la kiingereza wakati wao ndio lugha yao, ndivyo ilivyokuwa Mheshimiwa. Leo kwa sababu ya uwajiri wa holela holela kama huu halafu tunalalamika hapa tunapitisha maamuzi hapa hayendi, utendaji haufanyiki, kwa sababu ya mambo kama haya. Mhe. Spika, hili ni suala baya sana tunataka likomeshwe na likome mara moja.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine tunaitia hasara bure Serikali. Katika kikao cha Bajeti kilichopita Mhe. Hamza alizungumza hapa suala la Mwanakombo Vuai, alilizungumza hapa kwamba Katibu Mkuu kamuajiri mwanawe, tena kamuajiri akiwa ni *graduate*, wakati si *graduate* ndio kwanza anasoma. Analipwa mshahara wa *graduate*. Ingekuwa siku ile Waziri kakubali kufatilia yangekwisha. Pengine mambo mengine ingekuwa Mawaziri wanakubali kuambiwa yasingefika hatua hii iliyofikia kama wangechukua hatua mapema. Leo yanakuja humu ndani na maelezo chungumzima. Waheshimiwa cheo ni dhamana, tusitumie kwa maslahi binafsi kama katiba yetu ilivyokataza. Hili ni muhimu sana kujifunza.

Mhe. Spika, pia nimeona kitu muhumu mimi kimenikera na hili nataka liwe ni fundisho kwa wengine, iwe kweli iwe si kweli. Kwa sababu hata wajumbe wa Kamati Teule na wao pia ni binaadamu wanaweza wakawa wamefanya makosa ya hapa na pale. Lakini wamefanya kazi kwa niaba yetu. Sasa wanapotoka wafanyakazi wakenda wakatoa ripoti au taarifa zinazotakiwa kwa Kamati halafu ikatajwa kwamba wanasimbuliwa, hili Mhe. Spika, halikubaliki hata kidogo. Kwa sababu hii ni kuwambia watu kwamba wakiona uwoza wanyamaze, kwamba ukenda ukiuripoti unachukuliwa hatua, hili hakubaliki hata kidogo. Nadhani tutoe onyo kali kwa matendo kama hayo.

Mhe. Spika, jengine limeonekana kwamba nalo ni mazoea. Katika jumla ya ripoti hizi kuna baadhi ya mambo yametajwa hapa. Waziri ana wizara fulani, una suala lako binafsi huko unatumia idara iliyokuwepo katika wizara yako na unaipa maelekezo ikafanye kazi yako ya binafsi. Haya yamezoeleka sana kwa miaka nenda miaka rudi. Hili si haki, hatuwezi kutumia taasisi ambazo ni za serikali, zinaendeshwa kwa pesa za walipa kodi kuendesha mambo ya binafsi ya mtu.

Mhe. Spika, hili niwe mkweli tusije tukam- *point* mtu mmoja tu kwa sababu yumo kwenye ripoti hii. Hili limekuwa mazoea miaka nenda miaka rudi. Serikali ya awamu ya saba ijufunze katika hili, ioneshe mfano katika hili. Limetajwa hili katika ukurasa wa 162 kwamba Idara ya *UUB* kutumika kufanya shughuli binafsi za mtu. Leo tunaitumia Idara ya Serikali inakuwa inavunja sheria za nchi. Ingekuwa kila mtu anafanya kazi yake, kama una mambo yako binafsi ungetumia huduma binafsi, yasingefika hapa.

Mhe. Spika, katika yaliyokuwemo humu naomba pia nizungumzie suala moja kabla sijafunga maelezo yangu. Kuna suala humu limetajwa mimi hili naomba niseme kabisa, hili kidogo natofautiana na Kamati katika ukurasa wa 123 pametajwa suala la mzozo uliokuwepo katika utoaji huduma Uwanja wa Ndege. Katika mapendekezo yao mimi nilikuwa najiuliza kwamba hii ni sahihi kwa chombo kama hichi. Imesemwa pamoja na viongozi waandamizi wa ushirika wa *ZAN* na ndugu Khamis Juma kushindwa kununua hisa katika Kampuni hiyo

kutokana na umasikini wao. Ingawaje ndugu Khamis amenunua kwa asilimia 5. Serikali kupitia Mamlaka zinazohusika ziwasaidie kununua sheha hizo kwa asilimia 50.

Mhe. Spika, hili mimi siliungi mkono kwa sababu tukifika hapa tutajiuliza kwamba kwa nini wasaidiwe hawa tu. Mimi nadhani suala la biashara ni la mtu binafsi. Serikali ni muwezeshaji wa wananchi wote. Panapotokezea ushindani kila mtu aingie kwa ushindani sawa, lakini tukitoa pendekezo kwamba Serikali imuwezeshe fulani kununua hisa itakuja kuwa na mwengine akasema kwamba mimi nataka hisa kwa nini nisiwezeshwe na serikali yangu, tutawawezesha wangapi. Hili kidogo natofautiana na hili.

Mhe. Spika, ya jumla nataka kuyazungumza katika umoja wa uzuri wa kazi hii ni kwamba katika kila kifungu ulivyowapa hadidu rejea wametoa mapendekezo mahsusi ya hatua za kuchukuliwa. Nilikuwa naomba katika haya utakapokujakuwa unatuongoza mwisho Mhe. Spika, tuende kifungu kwa kifungu badala ya kuipitia na kutohoji kwa kamati kwa pamoja. Nasema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya mambo nahofu kwamba Baraza hili lisije likachukua hatua ambazo baadaye zikaja zikaigharimu nchi zaidi kuliko ile hasara iliyokuwa imeshapatikana.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo humu yanahusu mikataba baina yetu na kampuni ambazo nyengine za kimataifa. Unaweza ukaja ukashtakiwa kwa sababu kama taratibu kusema hivyo simaanishi kwamba hakuna taratibu zilizokiukwa ndani inawezekana taratibu zimekiukwa ndani lakini zile zitabakia zetu sisi za ndani. Yule aliyepewa *beneficial* kwa hili yeye hayamuhusu. Kwa hivyo yeye atakapokuwa umevunja mkataba wa maagizo ya Baraza ambayo yeye ni mnufaika, akenda Mahakamani tunaweza tukajikuta nchi tumeitia katika matatizo makubwa zaidi.

Mhe. Spika, tujifunze katika hili kwa yaliyotokezea Bungeni. Kamati ile iliyoundwa kuchunguza suala la Richmond, hakuna asiyejua kama taratibu zilikiukwa katika suala lile. Ndio maana nikasema katika hili sisemi kama Kamati imefanya makosa. Baadhi na inawezekana uchungu na shauku yao ya kutaka kuchukua hatua, wamependekeza kwamba mahala fulani mkataba uvunjwe na mali irejeshwe, tutizame athari zake.

Mhe. Spika, katika suala lile la Richmond ilifika pahala serikali imekuja kudaiwa fidia kubwa zaidi. Matokeo yake tumepata hasara zaidi kuliko ile Serikali au nchi ilipata kwa kuingia ule mkataba. Tukifika hapa pia Baraza itakuwa hatuwatendei haki walipa kodi. Ikiwa itabidi kuja kulipa fidia ni wale wananchi ambao tunawakamua kulipa fidia. Ningependekeza kwamba hili kwa ujumla tuje tulitizame moja baada ya moja.

Mhe. Spika, jengine katika hatua zilizotajwa humu kuna baadhi ya maeneo yamependekezwa kuchukuliwa hatua za kisheria na nyengine wameambiwa wawajibike kiutendaji. Mimi nilikuwa nina fikra hili tuje tulitizame kwa umakini. Mimi nadhani ni fikra zangu kwamba kwa viongozi wa kisiasa waliotajwa humu na hasa wale ambao wamekuwa *directly implicated* na katika kila kifungu wametajwa mimi nilikuwa nadhani *level* ya mawaziri wao wangewajika kisiasa. *Level* ya watendaji, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wengine nilikuwa nadhani kwa wale ambao *directly implicated*, basi Serikali ibebe dhamana ya kuchukua hatua za kuwawajibisha. Katika vitu hivyo, mimi nawaomba kabisa wakubali kuwajibika kwa heshima kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika uongozi wa kisiasa una gharama zake mara nyengine hata ukenda Mahakamani huwezi ukathibitishwa rasmi. Lakini kisiasa unakuwa umeshachafuka. Kuna kisa maarufi cha mke wa Julias Siza alituhumiwa, lakini baadaye ilipofanywa uchunguzi ikagundulikana zile tuhuma alizoambiwa hazikuwa za kweli. Lakini bado Julias *Caeser* akamuacha. Akamwambia kwamba wewe kwa kutuhumiwa tu huna sifa tena za kuwa mke wa Julias Siza. Hayo kwa uongozi wa kisiasa ukifika pahala ukiwa umetwajwa hasa Mhe. Spika, ni vizuri ukawajibika.

Kama kuna masuala ambayo ni ya kijinai hasa ambayo yameigharimu nchi nadhani sisi Baraza letu tusije tukafika pahala tukasema kwamba huyu achukuliwe hatua kadhaa kwa sababu na sisi tutakuwa tunaingilia kazi ambayo sio yetu. Katiba yetu nimeweka utaratibu wa uchunguzi, tungesema yale maelezo ya ushahidi ulipatikana ungelekwa kwa *DPP* yeye akatizama kisheria kwamba je, hapa pana kosa au hapa kuna kosa la kwenda Mahakamani. Tukifanya hivyo tutakuwa tumejiweka *safe* na Baraza hili halitokuja kutumiwa baadaye kwamba limechukua hatua kama ulivyotutahadharisha jana. Jana ulitutahadharisha sana tusije tukaonekana Baraza hili linachukua maamuzi ambayo sio sahihi, itakuwa tunalitia dosara katika jamii.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni kwamba kadhia yote hii kama nilivyosema mwanzo, imetufundisha jambo moja kubwa sana juu ya haja ya uadilifu, nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Nilisema kwamba Zanzibar wakati fulani ilikuwa inasifika, nadhani kwa Baraza hili kuchukua hatua kama hizi itakuwa linatoa

fundisho kwa wengine na watendaji wote wa serikali kwamba sasa zile zama za Mfaki ridhia zimekwisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lazima wanapofanya kazi wahakikishe kwamba kuna chombo cha wananchi. Mzee Jumbe aliita hii ni ngome ya wananchi kwa hivyo itakuwa na inawatizama. Kama tunavyosema sisi ni binaadamu tukikosea tunapo pahala pa kurekebishwa, lakini kama ni chombo cha wananchi tutakuwa tunawasimamia. Ile tabia yao wa kukaa watendaji na wengine wamejenga mpaka *empire*. Nasema watendaji nataka nieleweke vizuri, kwamba wamefika pahala kila wakikaa kazi yao kukisema chombo hichi, kuwasema wajumbe wa Baraza hili wakiona kama vile hawana kazi ya kufanya. Mimi nadhani Mhe. Spika, wajue kwamba chombo hiki kimepewa kazi. Hichi ni tofauti, wao wameteuliwa na mtu sisi tumechaguliwa na watu. Sisi tuna mamlaka kwa niaba ya wananchi kuwasimamia wao. Kama walivyosema wenzangu tusifike pahala ikawa mtu anapata huduma kwa sababu ya *know who* sio *know how*. Isifike pahala mtu ikawa anapata huduma kwa sababu anamjua nani sio anajua nini, itakuwa hatari Mhe. Spika, au kama ana haki au hana haki, tusifike hapo.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kunukuu hichi kitabu Mhe. Spika, niwaomba viongozi wetu wengi wangekisoma. Hiki kitabu kimeandikwa kutokana na kadhia za ufisadi na rushwa Kenya. Kina mafunzo makubwa sana kwa nchi za Kiafrika, kinaitwa *"IT'S OUR TURN TO EAT THE STORY OF A KENYAN WHISTLE BLOWE,* kimeandikwa na *MICHELA WRONG*. Yaliyokuwemo humu yanaonesha kwa nini nchi za Kiafrika hatwendi mbele, tunalalamika sana na kila wakati kazi yetu kukumbushwa mambo ya kihistori kama vile historia hayendi mbele kwamba tunakwama. Si kweli historia imekuja imepita, imeacha athari zake lakini mengi tumeyachangia sisi wenyewe. Kwa sababu ya hili lililoandikwa katika gamba la kitabu. Kila anayekuja anaona ni zamu yetu ya kula.

Mhe. Spika, katika hichi kwenye hitimisho lake kuna mafunzo makubwa sana nataka nisome hayo halafu nikae kitako. Mhe. Spika, hapa Baraza la Wawakilishi tumeshatunga sheria nyingi sana, juzi tumepitisha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, tuna sheria tele kila siku tunapitisha, lakini hali bado ni hii hii. Sasa Mhe. Michela Wrong anasemaje Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 327 wa kitabu chake anasema hivi:

"One of the many lessons of John Githongo's story is that the key to fighting graft in Africa does not lie in fresh legislation or new institutions. To use the seemingly counter intuitive phrase of Danny Kaufmann, expert on sleaze: 'You don't fight corruption by fighting corruption'. Most African states already have the gamut of tools required to do the job. A Prevention of Corruption Act has actually been on the Kenyan statute books since 1956. 'You don't need any more bodies, you don't need any more laws, you just need good people and the will'.

Mhe. Spika anasema moja katika mafunzo ya kisa cha John Dethong ambaye kama tunamkumbu sote alikuwa Katibu MKuu katika Afisi ya Rais aliyepewa kazi ya kusimamia maadili na kupambana na ufisadi, ambaye baada ya kuufichua yalimkuta madhara ikabidi aikimbie Kenya akenda uhamishoni Uingereza anaeleza humu kwamba kisa chake kinaonesha kupambana na ufisadi au rushwa Afrika, hakutopatikana kwa kutunga sheria mpya au kuunda taasisi mpya. Akasema hupambani na rushwa kwa kupambana na rushwa. Lakini anasema nchi nyingi za Kiafrika tayari zina zana za kutosha za kupambana na rushwa. Anasema kwa Kenya sheria ya kupambana na rushwa imekuwepo katika vitabu vya Sheria vya Kenya tangu mwaka 1956. Kwa hivyo anasema huhitaji vyombo au taasisi mpya, huhitaji sheria mpya, unahitaji wetu wema na nia njema ya kutekeleza yale ambayo tumeyapanga.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kama nilivyosema naunga mkono hoja hii, ninazo reservation zangu katika baadhi ya maeneo nimesema hapa. Kwa sababu kawaida yangu mnanijua sizungumzii kitu kwa ujumla wake nakwenda hatua kwa hatua, palipo kuwa sahihi kamati tutaunga mkono, palipokuwa panahitaji marekebisho kwa faida ya kukiwekea heshma chombo hichi tutakuja jarekebisho ndio nilikuwa nakwenda hoja kwa hoja.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii angalau niweze kueleza chochote kuhusu hii taarifa waliyotuletea wenzetu hapa. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku hii ya leo tukiwa hai huku tukiweza kuangalia ripoti ambayo kwa kweli Mhe. Spika, wasifu wake nitautoa muda mfupi ujao. Kabla ya kutoa wasifu huu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikukushukuru wewe binafsi.

Mhe. Spika, chombo cha Mamlaka kilichoteuwa hii Kamati kwanza nikishukuru nafikiri ulikiongoza wewe Mhe. Spika. Kwa kweli kama kuna kitu kilichosibu katika uteuzi basi ni pale mlipowateuwa hawa wajumbe wa

hii Kamati Teule. Kwa kweli ni watu makini, mahiri na wanaofanya kazi zao katika misingi ya uwadilifu mkubwa. Kwanza nakipongeza hichi chombo.

Pili nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuwashukuru na kuwapongeza hii Kamati yenyewe. Majukumu waliyopewa na Baraza wameyatekeleza vilivyo, wamefanya kile tulichowatuma. Wametuonesha utumishi uliomakini na wenye kutukuka mno. Kwa hivyo nawapongeza sana.

Mhe. Spika, sasa niende katika hoja na nianze katika ukurasa huu wa 5 wa ripoti hii ya Kamati Teule juu ya uhaulishaji wa kiwanja cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kilichopo Mtoni. Kwa masikitiko makubwa napenda nichukue fursa hii kwanza kutoa lawama kubwa kwa hawa mawaziri ambao na naibu wake pale ambapo Baraza hili linataka taarifa kuhusu kiwanja kile wakatupa taarifa za kupotosha. Wajumbe wa Baraza walidai juu ya kiwanja kile uhaulishaji wake uko wapi, pesa zikowapi. Kwa kweli taarifa tulizopewa na Waziri na Naibu Waziri wa Wizara husika kwa kweli zilipotosha Baraza.

Na si tu ilipotosha Baraza Mhe. Spika, lakini hata kukiuka kanuni zetu. Kama ukiangalia kanuni ya 58 kifungu kidogo cha tatu ya kanuni zetu mtu anatakiwa awe na uhakika na lile analolisema humu Barazani. Leo anasimama Waziri anaulizwa swali anazungumza kauli ambayo hana uhakika nayo, jambo ambalo nashukuru Kamati imekwenda kutoa ukweli na kutuletea hapa, naipongeza kamati. Katika hili nadhani haitokuwa sahihi tu kwa sababu jana Mhe. Mshimba aliandika barua nzuri hapa baada ya kupata ugonjwa wa tumbo na kushindwa kuhudhuria kutoa taarifa hapa ya Kamati yake, hivyo aliandika barua nzuri yenye mantiki kuliomba radhi Baraza. Lakini hapa tusiishie kuomba radhi sisi tu lakini waombwe radhi wananchi kutokana na ubabaishaji wa mali yao iliyofanywa na wachache.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe *tanbihi* ndogo kwamba hawa mawaziri na watendaji wa serikali wasijifikirie kwamba wao ni Mitume, wasijifikirie kwamba wao wana uwezo wa kila kitu. Mhe. Spika, hii ni fursa tu wamepata hivyo watutumikie vizuri sisi wananchi wao. Mhe. Spika, jambo la kusikitisha inaonekana wenzetu hawa ndio wanajifanya kama vile steringi tena Wakihindi hapigwi yeye, yeye kazi yake apige tu. Mhe. Spika, wasifikiri kwamba wao hawa ndio wenye akili na kila kitu, wamepewa fursa Mzee Karume aliwaweka mawaziri hapa wala hawana taaluma, lakini wakafanya mambo mazuri tu. Mhe. Spika, walizitumia hizi *public assets* kwa ajili ya maslahi ya wananchi, leo hapa kuna watu wana ma-*degree* Bwana Shaaban Robert naomba nimnukuu kidogo Mhe. Spika, kwa idhini yako alisema: “Busara kubwa na elimu kubwa kichwani haina faida ikiwa moyoni huna tembe ya wema”.

Mhe. Spika, hawa wenzetu wana vichwa vilivyoelimishwa lakini mioyo iliyosahauliwa. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba leo unachukua *public assets* unaiuza kama ni mali yako binafsi hilo ni tatizo. Mhe. Spika, hapa alikuwepo Mzee Kassim Ali Masego alikuwa anaongoza wizara hii hii, alituibia *public assets* kwa maslahi yetu badala ya kuziuza ardhi yeye ndio ametujengea majumba ya Michenzani yale mpaka sasa watu wanaishi. Mhe. Spika, pia badala ya kuziuza ardhi amejenga nyumba za vijiji huko tunakaa wakwezi na wakulima wa nchi hii. Mhe. Spika, inasikitisha leo mali za walipakodi wa nchi hii mtu anazichukua kama za kwake, hilo ni aibu tena sana. Kwa mnasaba huo sasa katika hili naunga mkono mapendekezo ya kamati kwamba Baraza na wananchi wa Zanzibar waombwe radhi, hilo moja. Mhe. Spika, la pili hiki kiwanja chetu kirejeshwe ili kirudi kwa wananchi na wote wanaohusika na kadhia hii wawe waungwana wawajibike.

Mhe. Spika, naomba niende na utaratibu wa ajira, utaratibu wa ajira ilikuwa katika Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu katika ukurasa wa 83. Mhe. Spika, sisi tunadhima kubwa kwani tuna wajibu wa kuisimamia serikali kuona kwamba haki inatolewa kwa wananchi wote wa Zanzibar. Ni kwamba hakuna makundi kunakuwa na *unity* na hili ndio lengo la Mzee Karume na Afro Shirazi kuleta mapinduzi ya nchi hii ili tuwe wa moja na tushikamane katika nchi. Vile vile ni lengo la hii *GNU* ku-*create Government of National Unit* ilinde nchi hii.

Kwa hivyo, inasikitisha kwamba unawaajiri watu kwa kua ni rafiki zako, familia yako, ndugu zako unawapiga mapande Wazanzibari hili ni tatizo na ni ubaguzi mkubwa. Mhe. Spika, sisi tumo katika *elected government* hatuko katika *monarchy* ingelikua tuko katika *monarchy* tungewaachia wao kama wafalme na familia zao wakafanya mambo yao sisi ikawa kazi yetu ni *hewalla* bwana. Lakini tuko katika hizi *elected government* hivyo, kila mtu ana haki katika nchi hii, hivyo inakua ni tatizo unamuajiri mwanafunzi anasoma wewe unamlipa mshahara wa kitaalamu. Mhe. Spika, hii inasikitisha tena sana na inavunja moyo.

Mhe. Spika, mimi hivi ninavyokwambia kuna vijana zaidi ya 20 ambao tayari wana digrii huu ni mwaka wa nne wamekaa tu wanasubiri ajira, leo unamuajiri mtoto wa kidato cha nne au cha sita unamuachia *degree holder* hao ndio wanaotukimbia katika nchi hii. Mhe. Spika, wakulaumiwa ni nani, mimi nadhani wakulaumiwa ni sisi

tunaooneana haya, hili limeshajuulikana kwamba kuna ubaguzi katika ajira za SMZ. Mhe. Spika, hapa tutapiga kelele sisi ni sawa sawa na mabunge mengine ya *Commonwealth* kwamba sisi tuna *work as a watching dog for public funds*. Mhe. Spika, ingawa kuna msemo unaosema *barking dog never bites*, lakini ijuilikane kwamba tumepiga kelele basi serikali isimamie hilo baada ya kusema. Lakini leo nakuhakikishia sijui lakini ni kwamba yule anayeonekana na maovu na akasemwa na Baraza hapa kwamba anaonekana na maovu lazima awajibishwe ili heshima ipatikane katika nchi.

Mhe. Spika, sio labda unamuondosha katika deski hili unampeleka katika dawati jengine, hivyo utakuwa hujafanya kitu. Kwa hivyo, mimi naomba sisi ni wamoja katika nchi hii hivi sasa tumetulia kabisa lakini kwa utaratibu huu tunaondoka katika matatizo ya kisiasa, basi tusipojikaza serikali itatuingiza katika matatizo ya kiuchumi.

Mhe. Spika, kwa sababu vijana hawa waliokosa ajira wataandamana, wataingia barabarani wewe una digrii yako anaajiriwa mtoto wa kidato cha nne, hivyo kweli unafikiri watakubali tu, hilo mheshimiwa ni tatizo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba katika hili basi mapendekezo waliotoa kamati yafuatwe moja baada ya jengine kwa sababu hawa ndio waangalizi wa wananchi na wameshaliona tatizo, kwa hivyo moja kwa moja maagizo yao serikali iyafuate.

Mhe. Spika, kwanza ajira yote ile isimamishwe halafu itangazwe upya na kwa mujibu wa sifa, na isiwe tu kwamba mtu ana mtoto wake, ana baba yake mdogo, ana ndugu yake kumpeleka pale sisi huku tukaendelea kuwalipa mishahara kupitia kodi zetu kumbe tunalipa familia za watu, kumbe tunalipa rafiki zao hatuwezi hilo na huo ni unyonyaji na ni ukoloni. Mhe. Spika, isiwe tumeondoka katika ukoloni halafu tukaingia katika ukoloni mambo leo, hivyo wameajiriana wao halafu mishahara tulipe sisi walipa kodi. Mhe. Spika, ajira hizi zisimamishwe zote zilizotiliwa mashaka na kamati hii na halafu zitangazwe upya halafu kila mwenye sifa ndio aweze kuajiriwa.

Mhe. Spika, nimalizie kwa sababu Mhe. Jussa amemaliza kila kitu, lakini niendelee kutiatia nyalio kwa mara ya mwisho kuhusu suala zima la kuhusiana na hadudi rejea Nam.124 juu ya uvamizi wa fukwe na uharibifu wa mazingira. Mhe. Spika, niipongeze taarifa hii kwa kweli wamefanya *feasibility study* hawa waheshimiwa kuweza kuibua mambo.

Mhe. Spika, hoteli hizi zilizotajwa kwa kiasi kikubwa sana zimekiuka mazingira na halafu zimekiuka mpaka sheria ya nchi. Mhe. Spika, sheria inasema katika *coral beach* zile za mawe ujenge mita 10 nje ya ufukwe wa mawe, halafu na ufukwe wa mchanga mita 23. Kwa hivyo, wao wamekwenda kuziguwika maana ya kuguwika ni kuzichovywa zile hoteli ndani ya bahari.

Mhe. Spika, sheria tumeitunga wenyewe na leo wasimamizi wa sheria hii wanatupa macho na wanaangalia. Mhe. Spika, sisi kazi yetu ni kutunga tu hapa wasimamizi ni wao hivyo ikiwa wameshindwa kusimamia hizi sheria watwambie kwani wako watu makini huku nyuma nnawaona wanaweza kusimamia sheria hizi. Mhe. Spika, leo watu wanakiuka sheria zetu halafu tunawaangalia tu, wapo kina Dk. Hija wanaweza kusimamia sheria zetu.

Mhe. Spika, mimi namshauri Mhe. Rais katika mambo kama haya basi aache muhali na sisi tumetunga sheria na tumekaa hapa kulipwa fedha za walipa kodi tukawekwa kwenye Baraza hili, tukatunga sheria ya mazingira halafu leo inakiukwa mtu anaitolea macho tu. Mhe. Spika, ni kwamba watu wako wameshindwa hao kusimamia sheria tafuta wengine huku wapo kuna Mhe. Jaku yupo, Mhe. Nassor hao watasimamia sheria zetu.

Mhe. Spika, jengine inaonekana serikali ina *double standard* katika suala zima la kusimamia sheria za nchi. Mhe. Spika, hii ni aibu nchi tulioingia katika uhuru tangu 1964 tunahimizwa umoja, mshikamano na mpaka leo tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, leo aliyekuwa na nyavu yenye tundu ndogo akenda kuvua kule anaambiwa anaharibu mazingira, anatafuta rizki huyo eti kwa kua katumia nyavu yenye tundu ndogo. Lakini huyu aliyevunja sheria kwa kujenga hoteli ndani ya bahari yeye haharibu mazingira, hili ni tatizo. Mhe. Spika, nadhani katika hili tumshauri Mhe. Rais atusaidie Baraza, aisaidie nchi wale wote wanaohusika na hoteli zote zilizokiuka sheria basi zichukuliwe hatua mara moja.

Mhe. Spika, kwa sababu ikiwa sisi sheria zinavunjwa leo tunaziangalia basi kesho mambo yatazidi zaidi. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi jimbo ambalo ni muhimu sana katika siasa za nchi hii naunga mkono taarifa hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba niseme neno moja au mawili. Mhe. Spika, nchi yetu au serikali yetu ina utajiri mkubwa wa mali na rasilimali, lakini kuna baadhi ya watendaji wanaturudisha nyuma na kutuletea umasikini mkubwa wa mawazo na huruma.

Mhe. Spika, moja kwa moja niende katika upotevu wa fedha katika Uwanja wa Ndege wa Unguja. Mhe. Spika, kuna ununuzi wa jenereta katika ripoti hii umeonesha kwamba jenereta hili lililonunuliwa kwa pesa nyingi sana, chakusikitisha na kibaya zaidi kwamba jenereta hilo zaidi ya mwaka sasa limeshindwa kufungwa au kujaribiwa lipo tu.

Mhe. Spika, hizo ni pesa za wafadhili sisi wenyewe tunakaa ndani ya nchi yetu tunapiga kelele, tunaomba pesa kwa wafadhili na wafadhili wanatusaidia kwa nia safi kwa kuiendesha nchi yetu, lakini baya sisi wenyewe hatuzijali zile nguvu za wafadhili wetu wala nguvu za nchi yetu wenyewe. Hili ni lakusikitisha sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, ukenda kwenye ukodishwaji wa maeneo *air port* ni kwamba watendaji wa *air port* wamelidanganya Baraza la Wawakilishi kwa sababu wamedanganya kamati na kamati ni za Baraza la Wawakilishi, na Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa mihimili mitatu mikuu ya serikali. Mhe. Spika, katika kamati hii ilipokwenda kule *air port* baada ya kutaka kuelezwa ni maeneo mangapi yaliyokodishwa waliambiwa ni maeneo arobaini, lakini kulikua na zaidi ya mengine nane hawakuyaorodhesha katika *list* ile ya watu ambao tayari wameshakodisha.

Mhe. Spika, kibaya zaidi ni kwamba kuna mtu amejitokeza yeye amekodi lile eneo, lakini yeye amekodi kwa bei ndogo lakini yeye zaidi amechukua juhudi ya kukodisha kwa mtu mwengine kwa bei kubwa zaidi. Pia chakusikitisha zaidi ni kua yeye aliyekodi mwanzo na kumkodisha mtu zaidi ya miaka mitatu ilipopita kamati hajalipa. Kwa kweli Mhe. Spika, tunakwenda wapi sisi ndani ya nchi hii. Mhe. Spika, utajiri tunao sana ndani ya nchi yetu na serikali yetu kwa jumla, lakini watendaji wetu ni dhaifu na wanatabia mbaya yakuirudisha nyuma serikali yetu na itakua maisha hatwendi mbele kwa hali kama hii yakutokuwa na imani.

Mhe. Spika, twende kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika suala la ajira. Mhe. Spika, Rais wetu wa mwanzo wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume miongoni mwa adhma zake ilikuwa ni kutoa elimu bure, lakini nataka niseme mbele ya Baraza hili tukufu ni tofauti na hivyo alivyokuwa yeye. Mhe. Spika, sasa hivi elimu imekuwa ni mali kuanzia nasari skuli mpaka kufikia chuo kikuu na kuendelea. Lakini yote hiyo haitoshi ni kwamba wazazi tunajitahidi kuwasomesha watoto wetu kwa gharama kubwa, mtu analala na njaa hana uwezo, lakini watoto wetu tunawasomesha kwa lengo la baadae waje wasaidie wazazi wao. Mhe. Spika, chakusikitisha kama huna mkubwa fulani juu basi mtoto wako haajiriwi hata akafika Chuo Kikuu, hata akawa na digrii, hata akawa na diploma, hata akawa na master haajiriwi mpaka uwe na mtu fulani.

Mhe. Spika, wizara inapokwenda kuomba kazi katika taasisi husika utumishi, wanaomba kazi kwa vigezo maalumu kama wanataka dereva, kama wanataka karani na kwa sifa maalumu. Lakini kibaya kwamba yule mwenye sifa hachukuliwi anachukuliwa mtu ambaye hana sifa ya nafasi ile kwa sababu tu yakujuulikana ni mtoto wa mkubwa fulani. Mhe. Spika, hilo linaturudisha nyuma na katika hili kama hatukulizingatia vilivyo basi watoto wetu tusiwalaumu baadae wakiwa wavuta unga, wakiwa wasafirisha unga, wakiwa wavuta bangi itakua sisi ndio tuliolisababisha hilo. Mhe. Spika, mtoto anamaliza kidato cha sita anaajiriwa hajaripoti hata siku tatu kazini anakwenda zake chuoni kusoma na analipwa mshahara ambao kua sio fani yake. Mhe. Spika, huko nje kuna vijana wetu wengi tu waliosoma na wana elimu ya kutosha na lakini wanashindwa kuajiriwa katika nafasi za kazi na wao wakajiendesha katika maslahi ya nchi hii.

Mhe. Spika, kama hatujalizingatia hili basi tutakwenda pabaya, sasa hivi tumefikia pahala pazuri, tunakwenda vizuri ndani ya nchi yetu, siasa tumeiweka upande, tunajadili maslahi kwa wananchi wetu kwa jumla, lakini tunataka kurudishwa nyuma kiasi fulani.

Mhe. Spika, naiomba serikali ilisimamie hili na iangalie vizuri ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi wale wote ambao wanahusika na kadhia hii kwa njia moja au nyengine serikali iwachukulie hatua inayofaa ili iwe funzo kwa wengine. Mhe. Spika, kinyume na kuwachukulia hatua hawa wanaohusika na haya itakua ni uzoefu na kila atakayekuja ataona na mimi niendelee, ataona madhali huyu hajafanyiwa na mimi niendelee na kufanya hivyo hivyo na itakua nchi yetu kila siku inakwenda kwenye umasikini na omba omba, jambo ambalo nchi yetu ni tajiri kuliko nchi tajiri zote za dunia hii. Mhe. Spika, kwa kumalizia hayo naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa siku ya leo ambayo ni siku ya Alkhamis, siku ambayo ni miongoni mwa siku tukufu. Mhe. Spika, na mimi basi niwapongeze wale wote Wajumbe wa Kamati Teule kwa kazi yao nzuri walioifanya. Pia Mhe. Spika, nikupongeze wewe kwa umahiri wako pamoja na Baraza hili kwa kupata fursa yakupata idhini ya kuundwa hizi kamati teule huenda ikawa ni *solution* yakuondokewa na matatizo mengi ambayo yaliyokuwepo kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, mimi tangu jana iliposomwa ripoti hii basi nimejiuliza kwenye kichwa changu, nikasema kwamba serikali wangelisema kwamba sisi tumeshaipokea hii ripoti kilichobakia tunakwenda kufanya kazi juu ya yale yote yaliyoelezwa kwenye ripoti hii. Nadhani ilikua hapana haja yakukaa hapa tukazungumza mengine kwa sababu ripoti kueleza imeshaeleza, imeweka bayana kila kitu ambacho wajumbe wa Kamati Teule walivyofanya kazi zao kwa makini.

Mhe. Spika, wakati tumepata fursa yakuichangia basi ipo haja ya kutoa sauti zetu na wananchi wanasikiliza tangu jana baada ya kusomwa ripoti hii, wanachi wengi wamesikiliza kwenye vyombo vya habari na wamefurahika sana na ripoti hii. Mhe. Spika, hata madereva waliokuwepo nje baada ya kutoka tu suala kubwa walilokua wakijiuliza wanasema ikiwa serikali itachukua hatua kwa hali kama hii ambayo imejitokeza, basi nadhani patakua na serikali madhubuti muda wa mwaka mmoja ujao. Lakini kinachowasikitisha sana wanahisi kwamba Baraza litapiga kelele, wawakilishi waseme ikiwa hapakuchukuliwa hatua kutokana na kadhia hizi basi mimi nadhani wananchi wengi watavunjika moyo mara mbili zaidi na Serikali yao makini ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, basi na mimi niseme kwamba suala zima ambalo mengi ambayo wameshayachangia wenzangu na mimi nizungumzie lile ambalo tunapata masuala mengi kama ni wawakilishi wa wananchi tunaulizwa, tunapata hoja nyingi lakini ufafanuzi wake hatujui tuufikie wapi, ni suala zima la ajira. Mhe. Spika, suala la ajira ambalo lilojitokeza katika uajiri wa Mawasiliano, hili ni suala ambalo linatia uchungu katika nafsi, tena linaumiza sana kwa sababu wewe kama mwakilishi ukitoka nje unaulizwa vipi ajira, watoto wetu wengi wamesoma wamemaliza vyuo mbali mbali. Lakini ukenda hivi sasa wako mitaani wamekaa kitako hawajui wafanye nini na wameemewa, leo kutokea hali kama hii kwa kweli inauma na inatia uchungu. Mhe. Spika, mimi naipongeza kamati tena kwa mara ya pili kwa jitihada yao hii waliyoifanya na mimi naungana na yale maamuzi waliyoyatoa kamati juu ya hatua ambazo zichuliwe juu ya kadhia hii.

Mhe. Spika, naomba sana suala hili lichukulie hatua mara moja au tuone kwamba zile sheria zetu tunazozipitisha hapa kama hazitekelezeki tuzichomeni moto. Kwa hivyo, haina haja kuwa na sheria ambazo hatuwezi kuzitekeleza, kama sheria zetu hazitelekezeki bora tuzichome moto tujue kwamba hatuna sheria. Lakini chamsingi wakati nchi hii inaongozwa kwa sheria, basi twende kwa sheria ambazo tunakaa katika Baraza hili kuzipitisha kwa makofi mengi hatimae sheria hizi zinapewa mgongo.

Mhe. Spika, nadhani sheria zetu tulizozipitisha hapa ni sheria za nchi na wakati sheria tunazipitisha hakuna uzito wowote. Kwa hivyo, mimi nahisi sheria ambazo zinavunjwa zichukuliwe hatua. Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wa Fedha alisema hapa kinachotufanya hivi ni kuoneana haya, tunaoneana haya, tunafumbiana macho hili ndio linalotukwaza kwamba sheria zetu zisitekelezeke. Lakini tutizame wanaoumia nani wananchi wetu tunawaumiza na wananchi wetu tunawatoa imani katika nafsi zao hata baadae tutakapowahitaji wananchi hawa kwa jambo ambalo la uamuzi wa nchi yetu wenyewe watashindwa na watahisi kila mtu aishi anavyotaka yeye mwenyewe. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Spika, kwa hali yoyote hatua zichukuliwe.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lilizungumzwa katika ripoti hii. Mhe. Spika, sisi ni wawakilishi wa wananchi, wakati sisi ni wawakilishi wa wananchi basi tunasema hatuko tayari kuona mali za umma zinauzwa kwa kujinufaisha mtu kwa nafsi yake yeye mwenyewe, hili sisi hatuko tayari kabisa. Mhe. Spika, sisi sote ni viongozi kwa hivyo tunasema kwamba mwenye kufuata kundi na yeye yumo, kwa hivyo wakati jina la viongozi na sisi tunaitwa viongozi, sisi hatutofata kundi hilo na tutakemea vya kutosha kuona kwamba mali za umma ambazo za wananchi wavuja jasho zinauzwa kiholela. Mhe. Spika, sisi hatuko tayari na tunaomba sheria zichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, kumdhulumu mtu mmoja bora sana kuliko kuudhulumu umma. Kwa hivyo, tuchukue hadhari kubwa ya kuogopa kudhulumu umma, ni bora kumdhulumu mtu mmoja unaweza ukamuendea nyumbani kwake ukazungumza nae na ukamtaka radhi na akaridhika yule mtu mmoja na akaondoka pale hali yakuwa ameridhika. Lakini umma mzima sijui hali hii itakuwaje. Kwahivo tunaomba sheria zichukuliwe Mhe. Spika, kwa kila aliyehusika.

Mhe. Ismail Jussa ameeleza vizuri hapa, ustaarabu mzuri sana mtu kujitia kwenye mizani mwenyewe, nikajihisi mimi nimekosa basi singoji nimatiwa kwenye mizani nitajipima mimi mwenyewe kipimo changu nina kosa gani nililolifanya, nina kitendo gani nilichokifanya. Kwa hivyo nina uwezo wa kujiwekea hadhari mimi mwenyewe, najua nijiwekee hadhari vipi na njia gani itakuwa bora kwangu. Sasa ni suala zima la binadamu kujitia katika mizani mwenyewe, kama mtu anaona yumo katika mkumbo huo basi ajiweke kando mapema na wale ambao wanahisi kwamba wao kuna wawajibishaji ambao watawawajibisha basi wawe na nguvu hii ya kuona umma unawatizama.

Mhe. Spika, katika ripoti hii kadhia zote hizi zilizojitokeza endapo hatua hazikuchukuliwa basi tutakuwa tuko katika hali ngumu na ya hatari kuona kwamba serikali hii kila mmoja afanye anavyotaka yeye mwenyewe. Kila mtu ataona hivi ndio ndivyo wakati kutakuwa hakuna hukumu yoyote itakayochukuliwa.

Tuchukue kigezo kidogo tu nyumbani, una mtoto wako mkubwa mmoja kafanya jambo halikukuridhisha ikiwa hukumrudi na waliobakia watafanya watasema mbona yule kafanya hakugombwa, mbona dada kafanya hakurudiwa, hakukemewa, kwa hivyo hii ndio hali iliyopo katika nchi yetu.

Sasa ikiwa tunataka tufanikiwe, ikiwa tunataka tuweke nchi yetu katika hali ambayo wanaokuja waione ni ya mfano, basi panapotokea tatizo kama hili hatua zichukuliwe haraka haraka. Kwa hivyo, sisi kama ni wawakilishi wa wananchi tunaunga mkono ripoti hii pamoja na hatua hizi ambazo kamati wameziagiza zichukuliwe katika kadhia zote ambazo zimejitokeza katika ripoti hii.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba ripoti hii imemaliza kila kitu cha msingi ilikuwa serikali iseme tu kwamba tunachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi yote na utekelezaji wa hukumu zilizotolewa na kamati tuone kwamba serikali inafanya kazi na kuchukuliwa moja kwa moja hatua hizi. Kwa hivyo Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hi kwa asilimia mia moja pamoja na mapendekezo yote yaliyotolewa na hatua zilizotolewa kuwa zichukuliwe, basi naunga mkono cha msingi tunaiomba serikali hatua hizi au kadhia hizi zilizojitokeza hawa wahusika wote wachukuliwe hatua. Tunaomba tena tunaomba kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, nami adhuhuri hii kunipatia fursa ya kusema machache katika ripoti iliyopo mbele yetu. Mengi yameshazungumzwa na ripoti kwa ujumla inajitosheleza na ningewaomba wenzangu wa Kamati ya *PAC* mara nyengine watakapotuletea ripoti basi wangekwenda chini zaidi kama ilivyokuja hii Ripoti ya Kamati Teule.

Mhe. Spika, ripoti hii imeeleza mengi sana na kila anayejua kusoma atakapochukua kitabu hiki ataona mengi, humu mna mambo ya uzembe, ufisadi, ubadhirifu na mambo ya ubaguzi, mimi sitaki niende huko nitakwenda kuchache sana. Haya yote Mhe. Spika, yanatuonesha au yametupelekea kuona kwamba serikali yetu iliyopita na hata hii iliyopo hivi sasa zina mambo mengi ambayo hayafai kuendelea nayo katika awamu yetu tuliyonayo.

Hivyo sasa, ni wajibu wetu sisi kama yalifanyika awamu ya sita sisi awamu ya saba tusiendelee nayo tena, lakini kunahitaji kitu ambacho kitayalinda haya na kujua kwamba kuna mambo yanahitajika yafanyike ili yasiendelee.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna dalili na kuna sababu za kuwa kila mara tunakuwa na Kamati Teule ili kupitia mambo kama haya. Hii mimi inanipa fikra na mawazo kwamba hata Mhe. Spika wewe mwenyewe kutokana na busara uliyotumia jana umeshaona kwamba upo umuhimu sasa wa kuwa na kamati teule, kwa hivyo mara kwa mara tunatakiwa tuwe nazo kamati hizi. Aidha, tuwe na kamati teule au zile kamati zetu ambazo ni za kudumu za Baraza tuziwezeshe, tuzipe nyezo za kufanya ripoti kama hizi ili zitusaidie katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa hilo nakushukuru na Mhe. Sale Nassor Juma yeye alimsifia mwandishi huyu lakini jana na mimi baada ya muda mfupi kukaa na wewe nilidhihirisha kwamba ni kiongozi mwenye busara. Wale waandishi wa vitabu walisema kwamba, “palipokuwa hapana elimu kama imekosekana, basi hata mvi hutumika kuwa ni dalili ya hekima”.

Mhe. Spika, ripoti hii ni kama vile tulikuwa tuna mgonjwa na mgonjwa huyu tukampeleka hospitali kufanyiwa vipimo akapata vipimo tofauti, *X- ray, CT-Scan, Ultrasound* na mengineyo. Lakini kinachojitokeza ni kwamba yule daktari ambaye anafanya hivi vipimo yeye siye mwenye kutoa dawa, yeye anakuonesha tu kwamba dalili zako ni hizi, tatizo lako ni hili, anayetoa dawa anakuwa ni *physician* yaani daktari mwengine. Sasa uwezo huo sisi hatunao uko katika mamlaka nyengine.

Sasa ninachokiomba ni kwamba huyu daktari ambaye ni *physician* mwanzo tu alipoingia katika madaraka alituambia kwamba sisi sasa ule wakati wa kuwa na ile *formula* ya *business as usually* hatutaki tena ameanza kuikemea. Sasa kwa maana hiyo kama yeye ni muumini wa suala hili kwamba sasa katia *notes* katika ile *business not usually* basi yeye awe ni mtu wa mwanzo kabisa kuona kwamba kalitekeleza kwa vitendo, yaliyotokea katika ripoti hii ni mengi sana na katika nchi yetu ambayo inaelekea katika kujenga demokrasia ya ukweli basi masuala kama haya hayawezi kuvumilika tena. Tunaomba ile *business as usually* iondoke na yeye ni mtu wa mwanzo aliyetwambia sisi kama ni watendaji tuondokane nayo. Kwa hivyo, tunataka kumuona sasa kaitekeleza yeye mwenyewe kwa vitendo.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia mimi sitaki niseme mengi, pia ripoti hii inatupeleka mana nataka nikumbushe kitu kimoja muhimu sana, kwamba hivi sasa sisi ni kama vile tumefikia hatua ya kufanya hukumu tuko Mahakamani. *PP* ameshafanya uchunguzi, uchunguzi umeshamalizika na sasa tunasubiri hukumu na hukumu hiyo wenye kuitoa sio sisi, sisi tunasubiri nini atafanya, lakini kuchelea kwamba sisi tusije tukaona kwamba tumenyongeka katika yale basi tunaomba hukumu itakayotoka iambatane na vielelezo ambavyo tayari tumeshavitoa na nafikiri vimeshathibitika.

Mhe. Spika, katika hili mimi naomba nithibitishe moja, naomba uniruhusu ninukuu tu, mwanzo baada ya uhuru kuna kiongozi mmoja wan chi hii hivi sasa ni marehemu anaitwa Nyerere. Yeye huyu alinukuu akasema kwamba, "*our judiciary at any level must be independent of the executive arm of the state, real freedom because of that, any citizens feels confidence that his case will be impartially judged even if it is a case against Prime Minister himself*".

Kwa maana hiyo hii inasisitiza kwamba, unapokuwa unahukumu kesi hutakiwi umtizame hata kama ni kiongozi mkuu wa nchi ile, wakati huu aliyeyasema haya alikuwa ni Mwalimu Nyerere mwenyewe. Lakini alisema kwamba hata kama kesi inahusu raia na raia huyo akawa anahisi kwamba haki yake ipo basi usiogope kuleta hukumu.

Sasa kwa maana hiyo, na mimi natoa kauli hii mwanzo tu baada ya uhuru ndio iliyotumika tunatakiwa sasa tufuate maadili haya.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sitaki niende sana isipokuwa tu, wenzangu waligusia lile suala la uajiri ubaguzi umekuwa ni wa hali ya juu. Unasikia kuna *interview* lakini ikimalizika *interview* hiyo waliopata ni wale wale. Mimi haliniumi sana kwamba mtu kapata ajira kwa sababu sawa kapata pengine ana cheti, lakini linaloumiza zaidi ni kwamba huyu anayeajiriwa anakuwa hana sifa za kufanya kazi, sasa kama hana sifa za kufanya kazi ina maana ubora wa kazi haupatikani. Kwa maana hiyo taifa letu siku zote litakuwa linasuasua, tunahitaji watu *right person* tuta *right post* ili tuweze kufanya maendeleo yetu kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Spika, sitaki nitumie muda wako mkubwa mimi nawaunga mkono walioleta hoja hii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa na mimi fursa kuchangia mawili matatu. Mhe. Spika, mimi nitasema kidogo tu sitaki kusema sana. Kwana mimi niseme kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na uwezo wake na kutujaalia leo tukawepo hapa wazima na kujadili hoja hii ya Kamati Teule.

Pili, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati Teule kwa jinsi walivyofanya kazi zao kwa ustadi mkubwa, jitihada kubwa, kwa sababu kama si jitihada kubwa waliyoifanya basi yasingeweza kupatikana yote haya ambayo yamepatikana. Kwa hivyo, niwasifu sana kwa jitihada yao na kazi kubwa waliyoifanya.

Pia nataka nitoe kama ushauri au nasaha. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo katika sura hii ya Umoja wa Kitaifa. Jambo la pili nataka niseme kwamba serikali hii ya Umoja wa Kitaifa iliyopo wananchi wa Zanzibar wanaiangalia kwa macho mawili au matatu zaidi, na wao wananchi wana matumaini makubwa na serikali yao, wamejenga matumaini makubwa na wana imani na serikali yao kama sasa umefika wakati wa kuleta maendeleo katika nchi yetu. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wetu tuna imani kubwa ya kuwa sasa umefika wakati wa kuijenga nchi yetu na kuleta maendeleo katika nchi.

Mhe. Spika, kama ni hivyo basi, ndio maana serikali imepanua demokrasia ya kweli na tukaweza kuthubutu katika Baraza hili sasa hivi tunaweza kuunda kamati teule na kuona kama yanayoletwa. Kwa kweli wananchi wa Zanzibar wamefumbua macho sasa hivi na pia niwashukuru Waandishi wa Habari kwa kuwaelimisha wananchi wetu juu ya Baraza la Wawakilishi na maendeleo yanayofikiwa na Baraza hili.

Mhe. Spika, tahadhari yangu sasa nataka niitoe kwa serikali. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema kabisa naomba ichukue tahadhari kubwa kutokana na suala hili liliopo mbele yetu, kwa sababu wananchi wa Zanzibar wote wanatuangalia kwa mambo mawili na wanasikiliza matokeo yanayotokea. Kwa maana hiyo, wazee wa kale wana msemo wao wanaosema kwamba, "Ukicha mwana kulia mara utalia wewe". Kwa maana hiyo ni kwamba serikali imepata matope makubwa kutokana na masuala yanayozungumzwa. Kwa hivyo, naiomba serikali iangalie kwa kina na ione kwamba itachukua jitihada gani kwa sababu iyo ndio yenye maamuzi ya mwisho. Sisi tunazungumza hapa lakini *finally* ni serikali.

Mhe. Spika, wazee wanasema "Maji yakishamwagika hayazoleki". Kwa maana hiyo hili suala lishakuwa wazi kila mmoja keshasikia linalozungumzwa hivyo serikali lililobakia sasa ni kusimamia utekelezaji wake. Mhe. Spika, mimi nasema kuwa Kamati Teule imeundwa kwa kuangalia sasa hivu wizara ambazo naweza kusema zimefanyiwa kazi ni wizara mbili, humo mwengine inagusa gusa tu, kama Wizara ya Fedha, lakini wizara hasa zilizofanyiwa kazi ni mbili ambazo ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na huku imegusa gusa kwenye Wizara ya Fedha.

Lakini ninachotaka kusema kwa serikali lau kama kamati teule zinaweza kuundwa kwa wizara nyengine tunaweza tukagundua mambo mengi zaidi ya haya mara kumi na tunaweza kulia sote na wananchi wetu na tukasema kwamba bora tukose kutokana na yaliyomo. Kwa maana hiyo basi, naomba serikali ijifundishe kwa makosa yaliokwishatokea na ikishajifundisha sasa isawazishe. Jamani nawaomba watendaji wa serikali wote muone kwamba sasa wakati umefika wa ukweli na uwazi, kama si wakati wa ukweli na uwazi yasingegundulikana. Kwa hivyo mujifunze kutokana na makosa mnayoyafanya.

Mhe. Spika, inasikitisha inahuzunisha, mimi naumia katika nafsi yangu nasema nikiwa naumia, kwa sababu wizara zote zinazoguswa ni wizara ninazozifanyia kazi kwenye kamati yangu. Nahuzunika kweli kweli nasema hali ya kuwa naumia kabisa, kwa sababu nimeguswa mimi mwenyewe ndani kabisa, lakini sasa mwenzangu kasema ukitaka kumpiga nyani usimtizame usoni na ukificha maradhi basi mwisho yatakutoa roho.

Mhe. Spika, kwa kweli nchi yetu si masikini lakini tunaitia umasikini sisi wenyewe. Zanzibar ni nchi ndogo kweli kweli, ni kweli kuna nyezo ndogo za kupatia uchumi wetu wa fedha lakini kutokana na udogo na watu wetu waliomo kwenye vianzio vya fedha hivi hivi vinaweza kuendesha nchi na tukatulia na tukajua kama tumekaa katika nchi yetu na tunaiendesha vizuri. Lakini tatizo ni kwamba tunachumia kwenye pakacha, maji ukitia kwenye pakacha yanavuja.

Mhe. Spika, imetosha, tulipofika panatosha jamani kwa maana hiyo naisihi serikali ifanye kazi kwa mujibu wa sheria inayojiwekea. Mhe. Spika, sasa hivi katika nchi yetu hii kuna watendaji wana mali haziwezi kuhesabika, kuna watu wana majumba hawawezi hata kuyatumia na kweli wameyapata katika njia za udanganyifu. Kwa maana hiyo nataka kukwambia Mheshimiwa kama inaweza kuundwa kamati teule nyengine basi tunaweza tukakuta mambo zaidi ya hayo.

Kwa hivyo naiomba serikali ichukue mkondo wake ione yule aliyehusika imchukulie hatua kwa anaehusika isimuonee, mtu achukuliwe hatua kwa lile alilolifanya mwenyewe isimuonee. Wenzetu Wakiristo wana msemo wao wanasema kwamba, "kila mtu ataubeba mzigo wake mwenyewe". Kwa hivyo, kila mtu abebe mzigo wake mwenyewe, ndivyo wanavyozungumza wenzetu kuwa siku hiyo ikifika kila mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi nasema hii inatosha kuijadili, sisi hata hatuna haja ya kuijadili ni kwamba ni sheria tu na ni wajibu, lakini hii inajitosheleza na sisi hatuna nyongeza ya kuongeza wenzetu wamefanya kazi ya ziada. Lakini kazi hii inayofanywa isije ikawa inamalizia hapo ukutani tu ikawa kelele zetu zote ndio mwisho wake, naiomba serikali iangalie kwa kina kabisa ili itoe fundisho kwa wengine watakaokuja wowote wale ili tuendeshe nchi yetu kwa amani na utulivu na twende kwa mustakabali wa nchi yetu. Naunga mkono hoja Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi hii kutoa machache juu ya ripoti hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kuendesha shughuli zetu hizi. Aidha, nikushukuru wewe binafsi kwa busara zako, hekma na uwezo wako uliokaa kuiteuwa kamati hii teule ambayo mimi binafsi ninapotazama kila mmoja namuona ni bora kuliko mwengine, kila mmoja naona bora angekuwa mwenyekiti huyu kuliko huyu kwa hivyo hawa ni watu wenye uwezo.

Mwalimu Nyerere baada ya kuongoza vita vya Kagera akawaambia wapiganaji sina cha kuwapa lakini cha kuwapa ni ahsante. Kwa hivyo na kamati hii teule nawambia ahsante sana kwa kazi waliyoifanya na pia Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuwateuwa watu hawa kuwa wajumbe wa kamati hii teule.

Mhe. Spika, tulipokuwa watoto sisi tukicheza kuna msemo tulikuwa tunambiana, kwa nini mwanadamu hamuoni jini, lakini jini anamuona mwanadamu? Tukawa tunaambiana majini waliambiwa fumbeni macho mwanadamu apite, wao hawakufumba waliweka mkono tu kwenye uso wakatuona tulipopita, lakini mwanadamu alipoambiwa fumba macho jini apite yeye aliyafumba kweli. Kwa hivyo, majini wakapita bila ya mwanadamu kumuona jini na ndivyo ilivyo leo kuwa sisi ni bahati mbaya tu jini kumuona, lakini wakati wote jini anaomuona mwanadamu.

Lakini sasa, sisi Wawakilishi humu ndani tumo wa aina mbili wa serikali na *backbenchers* lakini sote ni Wawakilishi. Sasa serikali iliambiwa fumbeni macho Wawakilishi wapite, hawakufumba tukipita wanatuona, na sisi tuliambiwa fumbeni macho serikali ipite, hatukufumba na wao wakipita tunawaona. Kwa hivyo, sisi na serikali tunaonana kwa sababu sote hakuna aliyekubali kufumba macho mwenzake apite, kwa hivyo serikali tunaiona na serikali inatuona. Kwa hivyo basi, kwa kuwa tunaonana kila upande baina yetu tufanye uadilifu katika kutekeleza majukumu yetu, serikali iwe na uadilifu, uaminifu kadhalika na sisi kwa sababu sote tunaonana hakuna aliyekuwa hamuoni mwenzake.

Mhe. Spika, ripoti hii kwa kweli inajitosheleza kabisa lakini mimi nitazungumza machache sana kuliko wote. Huko nyuma mimi nilikuwa ni mfanyakazi wa serikali na nilianzia ualimu, baadae nikenda Wizara ya Habari pahala fulani hivi. Siku moja ilitokea nafasi ya kutaka kuajiriwa mtu *typist* akatakiwa Afisa Mdhamini kwa kipindi hicho atafute watu awafanyie *interview* ili mmoja wapo aajiriwe na kwa kipindi hicho walitakiwa wenye sifa ya *Form IV* lakini waliopasi kwenye *credit* zaidi ya mbili.

Kafanya hivyo, kawaita watoto kama sita wakafanya *interview* na mmoja kawazidi wenzake na yeye dhamira yake ilikuwa huyo ndio amuajiri, lakini kipindi hicho mkubwa wake alileta mtu ambaye hajafanya *interview* lakini ni wake akamwambia muajiri huyu na huyo aliajiriwa. Kwa hiyo dhana hii ya kuajiri kwa upendeleo na bila ya sifa haikuanza leo na jana bado ni mzizi ambao unaendelea jambo ambalo si zuri hata kidogo.

Mhe. spika, baya kuliko yote hayo ni kumuajiri mtoto ambaye bado anasoma hata awe na umri kama wangu, kama bado hajaajiriwa yuko masomoni akaajiriwa bado ni mtoto ambaye yuko masomoni. Hii Mhe. Spika, ni mbaya tena mbaya sana, kwa kazi gani aajiriwe, kwa kazi gani apatiwe ajira wakati yuko masomoni, kwa sifa gani za ziada alizonazo wakati ambapo kuna mamia ya wanafunzi au vijana ambao wamemaliza masomo yao wa viwango mbali mbali wamekaa hawana ajira hizo.

Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunahangaika hapa na pale serikalini kuwatafutia baadhi ya vijana ajira tunaambiwa ajira hakuna, lakini hatimaye siku ya pili utakuta mtoto wa bwana mimi kaajiriwa pengine mwenye sifa chini ya yule ambaye nimemtafutia mimi. Kwa kweli Mhe. Spika, hili ni tatizo na kama ni ugonjwa basi kila ugonjwa una dawa, kwa hivyo ugonjwa huu lazima utibiwe, ugonjwa huu lazima uondoke.

Mhe. Spika, watu sote tuko kama kinyonga kwa upande mmoja, kinyonga ni mnyama ambaye macho yake yamekaa hivi, anaposikia zogo nyuma hageuki anaangusha macho tu pooo anaona nyuma, zogo liko huku na huku macho yanakwenda hivi. Kwa hivyo, tujue kuwa tunaonana sana na tunajuana sana kwa sababu ni wachache. Mhe. Spika, mimi nina bahati moja nzuri nikitoka hapa wengi hawanijui na hupenda makundi mbali mbali ya jamii jinsi wanavyotulaani watu baadhi ya wakati pale ambapo kumetokea jambo ambalo wao haliwafurahishi na vile wanavyotupongeza panapotokea jambo ambalo limo katika *interest* yao.

Mhe. Spika, mimi sikemei kuhusu hili tatizo mtu kumuajiri mwanawe ikiwa ana sifa za kuajiriwa kwa sababu mwanawe nae ni Mzanzibari na ana haki kama ile haki ya mtu mwengine. Lakini je, anakubalika, hapana ni upendeleo na ni dhambi, kama anazo ni haki na hatuna haja ya kumsema.

Mhe. Spika, mimi niko katika Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Madawa ya Kulevya, mambo ya Ukimwi na mengineyo. Kwa hivyo, tunapotembelea sehemu mbali mbali tunagundua uchafuzi na uharibifu wa mazingira mkubwa mno uliomo katika sehemu zetu mbali mbali. Kwa kuwa kuna sheria mbali mbali za kusimamia mazingira, mazingira kila uchao yanachafuliwa na yanaharibiwa, ni nani, ni sisi tulio na dhamana ya kusimamia mazingira.

Mhe. Spika, kama hatukuwa na hadhari ya kutosha visiwa vyetu hivi siku moja vitakuja kutoweka. Kama sijasahau jiografia vyema kisiwa cha Pemba nadhani kilikuwa kina upana wakati huo wa maili 14 lakini

ninahakika leo upana huu hautimii tena umeliwa na bahari kutokana na shughuli za kibinadamu tunazozifanya. Tunakata miti ovyo, mti unapoondoka maji yanachukua nafasi yake. Kwa hivyo, iko siku tutakuja kukifanya kisiwa hichi kijibane pande moja libakie kusini pande moja libakie kaskazini hatimae lizame chini lakini nadhani sisi tutakuwa hatuko tena.

Mhe. Spika, kama yuko anayechangia hilo litokee hatua gani ichukuliwe dhidi yake. Mhe. Spika, lazima tuwe wakweli, waaminifu, waadilifu ili tuwatumikie watu wetu kama tulivyoahidi kuwatumikia, wala tusifanye chochote kile ambacho kitawaangamiza. Si vyema, si vizuri, si busara, wala si uadilifu kuona mtu anatumia madaraka yake kwa kujinufaisha yeye binafsi kinyume na vile alivyokula kiapo.

Mhe. Spika, kile kiapo cha pale ni kiapo cha kweli kweli. Tunasema naapa kwamba aaaa lakini je, naapa kwamba unakusudia kitu gani, maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu muumba wetu. Kwa hivyo, nadhani tunapoapa pale hatuapi kumdanganya Mwenyezi Mungu kwa sababu hadanganyiki, lakini tunaapa kuwa tutakuwa waaminifu, wakweli na tutawatumikia watu wetu ili kuwakwamua katika hii hali waliyo.

Mhe. Spika, sisi hatuna sababu yoyote saa hizi ya kuomba misaada kama ingelikuwa rasilimali tulizonazo tunazitumia vilivyo kwa maslahi ya watu wetu. Mhe. Spika, kuna kipindi Zanzibar ilitoa msaada kuipa nchi nyengine wakati wa marehemu Mzee Abeid Amani Karume mimi nafahamu si mdogo sana sisi tulichangia. Leo Zanzibar kazi yetu ni kuomba, kwa nini tuombe, ina maana baada ya watu kwenda mbele sisi tunarudi nyuma. Lakini kuna watu wametufunga kamba ya kiuno tukenda hatua mbili kidogo ile kamba wanaivuta, ukivutwa kamba ya kiuno unaanguka kwa sababu unapoteza *balance*. Kwa hivyo, ili tuendelee sisi tuliomo humu tuwe wakweli, waaminifu na tuwatumikie wananchi wa Zanzibar kama vile tulivyowaahidi kuwatumikia.

Mhe. Spika, kwa kuwa nimesema ripoti hii inajitosheleza sina haja ya kusema chochote kwa sababu itakuwa kama ni kupoteza muda. Kwa hivyo, niseme tu kuwa naiunga mkono ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi na ningeiomba serikali pale ambapo pana hatua ya kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa ichukuliwe lakini bila ya kumuonea mtu yeyote.

Tuliwahi kufanya *debate motion* ilikuwa *Mmasi should be settle a fight so as to maintain justice*. Kwa hivyo, ningeomba na hapa *motion* hii itumike. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa kuendeleza majukumu yetu ambayo tumetumwa na wananchi wetu. Lakini pia Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza kwa dhati kabisa kunipa nafasi hii ya kuweza na mimi kuchangia mawili matatu juu ya ripoti ya Kamati Teule ambayo umeiunda kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Lakini pia nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuipongeza kamati kwa jumla chini ya mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi na shukrani hizo nataka nianze maneno yangu kwa ku-*refer* maneno ya Mhe. Subeit Khamis Faki aliyesema kwamba wakristo wanasema kila mmoja atabeba mzigo wake. Mimi nasema kwamba waislam wanasema hivi kwa kauli ya Mwenyezi Mungu *Walaa kafir waadhiratun hushra uqra. Sadaqallah laadhim.* Kwamba hatobeba mbebaji mzigo wa mwenzake, sasa yale maneno ni yale yale kwamba kila mmoja atabeba mzigo wake. Kwa hivyo, aliye na mzigo wake abebeshwe mwenyewe asimbebeshe mwengine.

Mhe. Spika, jengine nataka ni-*refer* kidogo maneno ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliposema kwamba umefika wakati wa yule ambaye mwenyewe anaona kwamba ameingia katika hatua hii mwanasiasa awajibike. Kwa hivyo, kuna maneno ya wataalam wanasema *hasibu kabla al tuhasab*, jihesabuni kabla ya kuhesabiwa. Kwa hivyo, tunapaswa mtu kujiweka katika *balance* kuangalia mwenyewe kwamba niko wapi na nafanya nini.

Mhe. Spika, jana katika kuchangia ripoti ya Kamati ya *PAC* nilisema hivi, kwa nini Mabunge yametakiwa kuunda kamati, nikaeleza umuhimu mkubwa wa Mabunge kutakiwa kuunda kamati ni kuhakikisha kwamba wanafuatilia yale mambo ambayo yamo katika mawizara mbali mbali mapungufu pamoja na faida ya kwenda kuyaangalia. Moja katika kamati ambayo inafanya kazi ya uchunguzi wa hayo ni Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, kwa kweli Kamati Teule imetuletea waraka huu ambao umebeba sura nzima ya kuihakiki serikali pamoja na wizara zote za Zanzibar. Mhe. Spika, kwa kweli kamati hii inastahiki kupewa pongezi za pekee kwa sababu wamefichua mambo ambayo ni kuikwamisha na kuirudisha Serikali ya Zanzibar, serikali ambayo tunaposema kwamba serikali yetu ni changa inasikitisha jamani, serikali changa, mtu anazaliwa akiwa na miaka

30 tu ana wajukuu, serikali hii ina zaidi ya miaka 40 ni changa tu. Bali uchanga wa serikali hii ni uchanga wa mawazo ya baadhi ya watendaji kujinyakulia mafao binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, umefika wakati sasa wa kuwahurumia wananchi wetu wa Zanzibar ambao hawana uhakika wa maisha yao ya chakula kwa siku moja. Kumbe Mhe. Spika, nchi yetu ni nchi ndogo ambayo ina uwezo wa wananchi wake kumiliki milo mitatu kwa siku. Lakini kitu gani kinachofanya kwamba wananchi wetu washindwe kula milo mitatu, ni hawa wanaojilimbikizia mali za umma kwa maslahi yao binafsi.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe mfano kwa sababu sote tunaishi hapa Unguja na Pemba wengine tuko vijijini, tuangalieni nchi yetu inapoingia neema ndogo mashelisheli tu yanakushinda yanaozeana kwa sababu ya wingi wake na uhaba wetu sisi watu wa Zanzibar. Unapofika msimu wa maembe tuangalieni maembe yanakushinda yanaozeana kwa sababu ya uhaba wetu sisi na wingi wa maembe. Leo vyanzo vyetu vya uchumi, vyanzo vyetu vya mapato tulivyonavyo tumeviwekea mawe. Mhe. Spika, watu hawa kwa kweli mimi nasema kwamba ipo haja serikali kuchukua nafasi yake ya kuwawajibisha ili kuwaonea huruma wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nataka niuokoe muda ili na Mhe. Mwakilishi aliyetangaziwa sasa hivi apate nafasi kabla ya kukiahirisha kikao hichi. Lakini niende kidogo katika masikitiko yangu makubwa kwenye ripoti nambari 189 katika ujenzi wa Wizara ya Afya kule kisiwani Pemba. Mimi nataka ninukuu katika maelezo machache. "Mkataba kati ya muajiri na mjenzi haukuzingatiwa." Kwamba katika ukurasa wa kwanza na wa pili mkataba unamtaka mkandarasi awe na uwezo wa kiufundi, vifaa na wataalam wa kutosha. Mambo yote haya hana na mtu huyu anapewa.

Halafu jengine katika maelezo yenyewe ya sifa za kampuni zilizoelezwa kuwa ni pamoja na uzoefu wa miaka mitano kampuni hii ya ujenzi ilisajiliwa Zanzibar mnamo mwaka 2007 kwa hivyo haikuwa na sifa zilizohitajika. Mhe. Spika, inaonesha dhahiri kwamba watendaji wetu wengi wanafanya maamuzi binafsi kwa ajili ya maslahi yao binafsi.

Mhe. Spika, napenda kwa busara kubwa kutokana na busara na hekima zako ili Zanzibar tuiweke katika *standard* nzuri ianpohitajika kuunda Kamati Teule kuzichunguza wizara nyengine ziundwe. Wananchi wetu wapo katika hali ngumu, wapo katika madhila magumu sababu ni watendaji ambao wanaangalia maslahi yao binafsi.

Mhe. Spika, katika kitu ambacho kinatudhoofisha mno kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo jana kwamba muhali, kuoneana haya, kuoneana aibu. Jamani umefika wakati wa kusema muhali basi.Mhe. Spika, moja katika sifa ya kiongozi lazima awe muadilifu, awe mkweli, awe mpenda wananchi wake.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe kisa kimoja hapa, ulitokea wizi wakati wa bwana Mtume (SAW) kuna mwanamke mmoja kaiba, sasa Mtume alikuwa ni miongoni mwa mahakimu waadilifu na tunatakiwa na sisi tufuate kigezo hichi. Sasa watu wakaamini kwamba yule bibi atakatwa mkono katika Mahkama, ikabidi kwamba yule bibi hukumu yake ni kukatwa mkono. Sasa watu wengi wakaleta shauri kwamba jamani nani ambaye tumchague aende kwa Mtume akamuombee bibi huyu asikatwe mkono. Kuna sahaba anaitwa Usama si Osama bin Laden, bwana Usama huyu akaendewa kwamba aende kwa Mtume akamuombe kwamba huyu bibi asikatwe mkono. Katika kwenda Usama kumueleza Mtume kumuombea yule bibi, Mtume alionesha uchungu mkali sana kwa Usama akamwambia "Ewe Usama unataka kumuombea huyu katika hukumu aliyoitangaza Mwenyezi Mungu. Laiti angekuwa mtoto wangu Fatma ningemkata mkono."

Jamani tuna wajibu kwa mnasaba wa maneno haya aliye na kesi aachiwe kesi yake, aliyekuwa anapaswa kuwajibishwa basi awajibishwe. Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi angalau kuchangia. Kwa niaba ya wananchi wangu wanyonge wa Jimbo la Chambani basi naiunga mkono ripoti hii pamoja na mapendekezo ya hatua ambazo zichukuliwe kwa wale ambao wanashutumiwa juu ya kadhia ambazo wamezifanya. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuchangia ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ripoti yake nzuri tu aliyoisoma jana hapa na sisi wajumbe sote ikawa tunaisikiliza pamoja na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, pili niwapongeze wajumbe wote wa kamati hii kwa kazi ngumu waliyoifanya walipokuwa wakitafuta shughuli hizi ambazo ni matatizo kwa wananchi wetu na serikali kwa ujumla. Mhe. Spika, wajumbe

hawa hawakujali jua, mvua, malipo, wala lolote alimradi walifanya kazi hii, lakini nawaambia Mwenyezi Mungu atawalipa kwa haya waliyoyafanya.

Mhe. Spika, naamini kufanya kazi hii ni kwa sababu ya uchungu wa nchi yetu. Mhe. Spika, sisi hatutokubali kuona jinsi ya mali za serikali zinavyopotea kiholela. Mhe. Spika, hili hatutokubali kabisa kwa kuona wananchi wanadhulumiwa haki zao pale ambapo hapana tatizo la kuwa wadhulumiwe haki zao.

Mhe. Spika, sitaki niende katika ripoti kwa sababu Mhe. Mwenyekiti jana kaisoma vizuri na tumeyafahamu, tumeyaelewa yote yale ambayo yanadhuru serikali yetu hii tuliyonayo hivi sasa. Hii ripoti Mhe. Spika, itakuwa ni ripoti ya historia na kwa mara ya mwanzo katika Baraza hili.

Lakini Mhe. Spika, mimi ningesisitiza tu kwamba isiwe ni mwisho, huu uwe ni mwanzo wa kufichua maovu yote yale ambayo yanatendwa na wale ambao hawaitakii mema nchi hii, wala hawaitakii mema serikali hii, wala hawawatakii mema wananchi wao.
Mhe. Spika, naomba waovu hawa wafichuliwe mara moja ili wananchi wajue nini kinachotendewa katika Baraza la Wawakilishi na nini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanavyowatetea wananchi wao kwa kudai haki zao.

Mhe. Spika, serikali kila siku inasema kwamba haina pesa. Mhe. Spika, kweli serikali itakuwa na pesa wakati ya kuwa waovu hawa tunawaacha tu ambao wanadhulumu nchi hii, wanaidhulumu serikali yetu, wanawadhulumu wananchi wetu. Kweli Mhe. Spika, serikali itakuwa na pesa na kweli uchumi utakuwepo. Itakuwa uchumi hapana, serikali kila siku itasema kwamba haina pesa jinsi ya maovu wanayoyafanya wenzetu.

Mhe. Spika, mwisho ningesema kwamba Mhe.Rais ningemuomba hawa *backbenchers* ambao wamo katika Kamati Teule asije akawachukua akawaweka viti vya mbele atuachie huku huku tushirikiane nao ili kuyafichua yale maovu ambayo yanatendeka katika nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuijadili ripoti hii na nafikiri muda umefika sasa tukapumzike ili tukutane jioni. Kwa maana hiyo basi, sasa naahirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza katika jioni hii ya leo, na mimi angalau niseme machache sana kuhusu ripoti hii ya kamati teule ambayo kwa kweli wenzetu wamefanyakazi kubwa sana inafaa kuwaunga mkono.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kukubali kwako kuunda kamati hii teule, ambayo katika historia yangu ya Baraza katika kipindi cha miaka 20 hii nafikiri ni kamati ya pili kuundwa. Waheshimiwa Wajumbe mara nyingi walikua wakidai kuundwa kwa kamati teule, lakini kulikua kuna vizingiti vya hapa na pale na mara nyingi wameshindwa kupata kamati teule.

Nadhani Mhe. Spika, unaweza kuthibitisha sasa kwamba kamati teule kumbe hata wajumbe wakiamua iundwe kamati teule basi kuna mambo muhimu sana ya msingi yanafaa kuchunguzwa.

Mhe. Spika, nataka nitumie fursa hii pia kuwapongeza sana wajumbe wa kamati hii, ambao walifanya kazi mpaka kwenye muda wao wa *private* na hatimaye kufanikisha kutoa ripoti moja safi sana.

Mhe. Spika, wenzangu wamesema mengi, nadhani haitakua jambo jema sana kuyarudia yale kwa yale, kwa sababu kuna wajumbe wengi wanataka kusema. Kadiri nilivyoiangalia hii ripoti nimeibua mambo humu ambayo naomba niyataje.

Kwanza Mhe. Spika, nilichokiona mimi kwa kupitia ripoti hii, katika taasisi nyingi za serikali kuna ukiukwaji mkubwa wa sheria. Hii inasikitisha sana kwa sababu tunatumia pesa nyingi za wananchi, tunatumia muda wetu mwingi tunakaa hapa, tunatengeneza sheria Mhe. Spika, na sheria tunazozitengeneza hapa ni nzuri sana, ambapo sheria kama hizi wenzetu katika nchi nyingine basi wamepiga hatua kubwa sana ya maendeleo kwa sababu ya sheria zao. sheria zetu nzuri.

Lakini tatizo Mhe. Spika, tukishatengeneza sheria zinafungiwa kwenye makabati na watendaji wanafanya vile wanavyoona wao wafanye. Ndio maana tunadumaa siku hadi siku.

Jambo jengine Mhe. Spika, nililoliona kwenye ripoti hii ya kamati, nimegundua kwamba tunaendesha nchi kwa misingi ya kujuana. Huyu mwanangu, huyu mtoto wa ndugu yangu, alimradi mtu wako wa karibu ndiye anayestahiki kupata fursa katika nchi hii. Hili Mhe. Spika, ni hatari sana, kwa mawazo yangu mimi naona ni jambo hatari sana, maana yake unasababisha sasa chuki kati ya mtu na mtu, unasababisha wengine wasiridhike na tukifika hapo basi tunatishia hata amani ya nchi.

Mhe. Spika, ripoti hii inatoa taswira ya mambo yanavyokwenda huko katika taasisi za serikali, maana ni taasisi chache sana zilizochunguzwa na hii kamati teule. Lakini yaliyogunduliwa ni haya ambayo kwa kweli sidhani kama kuna mtu atabisha kwamba haya sio mazuri hata kidogo.

Mhe Subeit Khamis Faki alisema hapa asubuhi kwamba ikiwa kila taasisi itakwenda kuchunguzwa, basi yatagundulikana, mwenyewe Mhe. Subeit kaita magurunguti. Yatagundulikana magurunguti mengi na kwa kweli Mhe. Spika, huo ndio ukweli. Hata juzi Mhe. Hija Hassan alipokua anawasilisha hoja yake binafsi kataja baadhi ya mambo kama haya.

Mimi nadhani Mhe. Spika, wajumbe wako wakikuambia tuunde kamati teule, basi naomba sana kwa busara zako usiwe mzito, kwa sababu sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sio Manabii wala sio Mitume sisi. Maana Mtume huwa anateremshiwa *wahyi* na Mwenyezi Mungu mwenyewe, lakini sisi hata tukifikiria kusema pahala fulani kuna jambo fulani, basi lile jambo tumelipata kutoka pale pale. Kuna watu hawaridhiki na mambo yanavyokwenda, hawana pa kutolea ndio wanakuja kutuambia sisi, tukiyapata sisi ndio tunakua na ile shauku ya kusema sasa pale pahala bora pakachunguzwe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ili kuifanya nchi hii iondokane na mazowea haya tuliyonayo, ni lazima tuwe na utamaduni huu wa kuchunguzana mara kwa mara. Mimi nafikiri kwa kupitia kwenye kamati hii teule tuliyoiunda, serikali ichukuwe kama hili ni tukio la kujitathmini utendaji wa serikali unavyokwenda.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nimeliona mimi ni kwamba kuna wakuu wa taasisi za serikali, wanatumia madaraka yao kwa maslahi yao binafsi. Hili limeonekana katika hadidu rejea nyingi zilizosomwa hapa imeliona hili, jambo ambalo kwa kweli Mhe. Spika, mimi nadhani linasikitisha kwa sababu waheshimiwa wengi tunakula kiapo hapa cha uaminifu. Sifa moja kubwa sana ya kiongozi ni kuwa muadilifu na unapokuwa muadilifu basi na ubinafsi uuache kando. Maana uadilifu na ubinafsi ni mambo mawili ambayo hayakutani.

Mhe. Spika, mimi sioni tatizo hata kidogo, mtu kumuajiri mwanawe kazi, sio tatizo, kwa sababu kila raia wa nchi hii ana haki ya kuajiriwa, huo ndio ukweli. Kama ametimiza sifa zilizotakiwa basi aajiriwe. Sasa kama mtu anamuajiri mwanawe madhali ana sifa sio tatizo, lakini unapofika pahala
Mhe. Spika, unamuajiri mwanao pale kazini hayupo wala watu hawamjui, yuko masomoni huko wewe unamuajiri huku na unamlipa mshahara mkubwa kweli kweli, aah! Sasa hapa uadilifu uko wapi jamani, wakati pengine nafasi hiyo imeombwa na watu wenye sifa wapo wamekaa-*bench* wameshasoma, hapewi mtu anaajiriwa mtu yuko pahali anasoma huko. Hii inasikitisha sana. Kwa kweli sijui hata niseme vipi.

Mhe. Spika, kuna mshairi mmoja alisema, kwa maneno ya Kiarabu naomba niyanukuu kidogo. Alisema, '*Dhahabtu ila uroba waraaitu Islama Wamaraaitul Muslimina'* yaani nimesafiri mimi nikenda Europe, kule nikaukuta Uislam, lakini Waislamu wenyewe sikuwakuta, maana yake kuna *practice* ya kisheria. Kile ambacho kiko ndani ya mkataba ndiocho unachokifanya huo ndio Uislamu na ndio uadilifu.

Hata kama wale Waislamu wenyewe hawapo. Halafu akasema, *'Thuma dhahabtu Ilabiladil Islam'*, kisha nikaja katika miji ya Kiislamu, *'Waraaitul Muslimina'*, nikawakuta Waislamu, '*Wamaraaitul Islama*', lakini sikuukuta Uislamu. Maana yake Uislamu ni kutimiza ahadi. Sifa ni kutimiza ahadi tumeikiuka sisi viongozi. Hatuko waadilifu, hatutekelezi mambo kwa mujibu wa sheria. Lile ambalo mnakubaliana basi unalifanya.

Mhe. Spika, alama moja ya mnafiki ni kukiuka ahadi. Ile ahadi uliyochukua kwamba mimi nitafanya kazi kwa mujibu wa sheria hii, halafu ukenda kinyume na hiyo sheria. Mhe. Spika, kwa kauli ya Mtume hiyo ni alama ya kinafiki. Sasa je, tuitane wanafiki humu. Mimi nadhani sio jambo jema na lazima tuondokane na mazoea haya, turudi tufanye kazi kwa sheria.

Mhe. Spika, tulikua tuna siasa chafu kwa miaka mingi iliyopita, nchi yetu ilidhalilika kiuchumi sana, lakini tumerudi kwenye umoja tukaunda serikali ya umoja wa kitaifa, wananchi walikua wana matumaini makubwa

kwamba sasa tunaanza hapa kwenda mbele. Lakini Mhe. Spika, ikiwa hatutekelezi ahadi zetu, hatutimizi yale ambayo tumekula kiapo kwa ajili ya mambo hayo, nadhani tatuwavunja moyo sana wananchi. Nawaomba sana viongozi wa serikali wajitahidi sana kutekeleza ahadi zao. Athari ya haya Mhe. Spika, yaliyoandikwa humu, athari yake kwanza ni kuudidimiza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi sitaki kusema moja kwa moja kua ni ufisadi, lakini inawezekana kukawa kuna dalili za ufisadi, maana mtu mara anapokua anatumia madaraka yake kwa kujinufaisha yeye binafsi, hapo itakua kawasahau wanyonge na uchumi utakua unakamatwa na watu fulani fulani.

Mhe. Spika, kuna haja kubwa sasa ya kupitisha ile sheria ya kuhakikiana humu, kila mtu mali aliyonayo na *income* yake inayokuja. Je, *income* yake huyu inamfanya kweli awe na mali hii. Mimi nina wasi wasi kuna watu wana mali kibao.

Athari ya pili Mhe. Spika, ikiwezekana haya yatiwe kwenye mtandao ili watu duniani wayaone. Mhe. Spika, hii sio dalili nzuri ya utawala bora. Utawala bora hauendani na mambo haya. Kwa hivyo, hapa tutakua na kazi kubwa sana ya kusema, yaani wenzetu watufahamu kwamba hapa pana utawala bora kwa mambo haya, hayuko atakaye tufahamu.

Jambo jengine baya zaidi ambalo litatokea Mhe. Spika, ni ule mmoja na mshikamano wetu utatetereka, kwa sababu watoto wawili waliosoma darasa moja miaka 14, lakini wakafika pahali mtoto wa mkubwa kaajiriwa yeye kaachwa, basi wale watoto wawili uhusiano wao unachafuka, kwamba kumbe yule sio mwenzangu. Mimi nadhani tufuate sheria.

Mhe. Spika, tukifuata sheria basi kila mtu ataajiriwa kwa sifa zake, hataajiriwa kwa misingi kwamba huyu ni mwanangu au huyu ni mtoto wa kaka yangu hapana. Utamuacha mwanao ukamuajiri mtu mwengine mwenye sifa.

Mhe. Spika, mimi sina maneno mengi, lakini nasema tumechoka kila siku kuhubiri unyonge, umaskini na upungufu wa bajeti, nataka tuondoke hapa. Kama hatujasema na nafsi zetu, basi hapa patakua pazito kuondoka Mhe. Spika, tukitaka tupige hatua ya maendeleo, lakini itatushinda kwa sababu ya mambo kama haya. Nadhani sasa tuondoleane muhali, mtu akifanya kosa tumuambie bwana mkubwa umefanya kosa na sasa wajibika. Nadhani tukifanya hivyo basi tunaweza tukenda vizuri.

Mhe. Spika, narudia kusema kwamba wenzetu wameendelea kwa sababu ya kuheshimu mipango yao wanayojipangia. Kuna nchi hivi majuzi tu zilikua na hali mbaya ya kiuchumi. Siku zote wajumbe wenzangu wanapiga mfano nchi ya Rwanda, juzi walikua na vita, janga kubwa sana, wakauwana na hali yao ya uchumi ikawa mbaya. Lakini kwa sababu walipanga na wakaheshimu walichokipanga, sasa hivi wako mbele.

Mimi nilishawahi kupigiwa mfano kwa Afrika ya Mashariki hapa. Kwa hivyo, na sisi hakuna kisichowezekana, lakini tuwe *serious* tufuate sheria, tuondoe ubinafsi tuwe waadilifu. Nadhani Mhe. Spika, tukifanya hivyo tutakwenda vizuri. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na *taufiq* ya kuzungumza. Pili naomba nipongeze kazi ya kamati na hasa Mwenyekiti, namna alivyowasilisha muhtasari wa ripoti ya kamati.

Mhe. Spika, kilichofanyika ni kuitia maabara serikali kwenda kufanyiwa uchunguzi wa maradhi iliyonayo.

Sasa kazi ya kamati ni sawa sawa na kazi ya wale wachunguzi katika maabara. Ni kutoa hali ilivyo katika yale mambo ambayo walitakiwa wayafanyie uchunguzi. Bahati nzuri walitoa na baadhi ya mapendekezo, lakini kuna taratibu za kisheria na kanuni mbali mbali ambazo serikali itaizingatia na kuona, kutokana na mapendekezo waliyotoa, basi lipi ambalo lifanyike litakalokua na maslahi kwa Zanzibar. Wale walioonekana kwamba wamejitokeza wazi wazi kuvunja sheria, basi hakuna wasi wasi uwajibikaji upatikane, wawajibike mara moja. Ukija kwenye sehemu ya pili, baada ya kuwawajibisha kuna mawaziri kama wawili au watatu hivi watakua wameongezewa kazi katika ripoti hii.

Kwanza itakua ni mawaziri wote kwa ujumla, lakini Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naona kama kaongezewa kazi katika ripoti hii. Kwa sababu taratibu zilizotumika katika kuwaajiri watu mbali mbali ambao sio mahali pao kuajiriwa kwa wakati ule, zilitokana zaidi na iliyokua Idara ya Utumishi wa Umma. Sasa

katika haya mabadiliko ya sheria yaliyopita, utungaji wa sheria mpya, kupata wizara mpya bado wafanyakazi ni wale wale na mambo ni yale yale yaliyokua yamezoeleka.

Kwa hivyo, ili kuona kwamba ripoti hii inafanyakazi, Mhe. Waziri huyu inabidi afanyekazi ya ziada na wizara nyengine kuona kwamba ile kazi iliyofanywa na kamati basi inafanywa kwa wizara zote, kuona kwamba watu walioajiriwa wana husiana au wanalingana na kazi walizopewa.

Mhe. Spika, mimi nina mifano miwili katika hapa. Kama kuna mtu amejenga nyumba kubwa nzuri, kwa jina la zamani inaitwa *kasri* akaona aajiri wafanyakazi watano. Mmoja ni mtu wa bustani, wa pili ni mpishi, wa tatu ni mtu wa kazi za ndani za kusafisha, mtumishi wa nne ni yule anayeshughulikia gari za mabosi kuziosha na mengineyo na mtumishi wa tano yeye kazi yake kupeleka maagizo pahala popote pale, kama kununua au kitu chochote kinachotakiwa nyumbani.

Lakini yule aliyewaajiri akaona kama ambavyo yanafanyika, akaona achukuwe jamaa zake wapate kazi ile. Mpishi akapelekwa kwenye bustani, mfanya bustani akapelekwa kununua vitu na mambo kama hayo, ile nyumba itakwenda kwa siku ngapi. Ndio yaliopo sasa. Sisi tunaona mbona mambo hayaendi katika mawizara, pengine pesa zinatumika lakini wafanyakazi wengi wao kama ilivyobainika humu hawakuajiriwa kwa zile *profession* zao. Kwa hivyo, kufanya uchunguzi wa *postmortem* ya serikali nzima na utumishi wake ni jambo la lazima, kwa sababu hii imefanyiwa moja tu kutokana na tuhuma zilizokuwepo, lakini hatuna uhakika kwamba na kwengine ni hivyo hivyo. Hilo la kwanza.

Mfano wa pili Mhe. Spika, mimi nilisikia kesi moja iliyotokea mwaka jana. Kulikua na mtu anatafuta ajira, kazi yake yeye ni *engineer*. Kwa hivyo, katika kuhangaika akawa tayari keshapeleka maombi yake na alikua anafanyiwa *interview*. Lakini jambo la kustaajabisha siku ile ya *interview* ikawa badala ya mmoja wakawa wawili, lakini yule wa pili ana *public administration* na kazi inayotakiwa ni *engineer*. Sasa yule aliyepelekewa yule mtu anatetemeka mikono, aah wewe hiki cheti chako hata hakilingani na hii *post* inayotakiwa, ulitoka wapi lakini hana budi na yeye akamwingiza, kazi inayotakiwa ni *engineer*, yeye ana mambo ya utawala wa umma. Kwa hivyo, inaonekana haya mambo yapo.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na wengi waliochangia kwamba ipo njia mtu ya kumsaidia mwanawe au ndugu yake, lakini awe na *qualification*, yeye ni binadamu sio kwa njia hizi ambazo zimetumika. Kwa hivyo, hizi zinaonesha kwamba ubinafsi umetawala sana katika uongozi, mpaka wizara nyengine unaona hasa baba yupo chini yake mwanawe.

Mhe. Spika, sisemi kwamba ni jambo la kupita, mimi sikubaliani kwamba pachukuliwe hatua za ghafla halafu basi, lazima madhali tunafanya marekebisho basi twende kwa utaratibu wa marekebisho ya muda wote kwamba, sasa wafanyakazi wetu wanalingana na zile nafasi ambazo wamepewa.

Mhe. Spika, suala la asilimia 10 *commission* pia inatufikisha pabaya. Siku moja katika mchango niliokua natoa humu Barazani, nilisema ziko nchi zimeamua katika sera na sheria zake kwamba mfanyakazi yeyote hana ruhusa ya kuchukua asilimia 10, inarudi huku katika mfuko wa taifa. Sisi bado hatujafikia huko, lakini kutokana na uzito wa asilimia 10 inabidi sasa hata wizara haziachiwi kununua mambo yake wenyewe, inunuliwe na mtu binafsi halafu ndio wakabidhiwe wizara.

Hii imeshatokezea kuchelewa sana kwa *TV* Pemba kupatikana kwake, mashine zilizoagizwa zilikuja kwa jina la mtu binafsi. Sasa hivi kuna kesi hiyo hapo iliyotajwa katika ripoti hii, *generator* lililonunuliwa limeshindwa kujaribiwa limekuja kwa jina la mtu binafsi. Sasa nauliza mimi, katika zile sheria mbili ambazo Mhe. Waziri wa Fedha jana alizitaja wakati wa ku-*sum up* ripoti ya *PAC*. *Public Finance Act* na *Procurement Act*, ni pahala gani ilipoelekeza kwamba vitu sasa vya serikali vinunuliwe kwa jina mtu binafsi.

Kwa hivyo, wizara hii ya fedha iwajibishwe basi na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye anayeshughulikia mambo ya Baraza, kwa sababu wao wenyewe ni vichwa lakini hawakutaka kujirekebisha. Ununuzi wa vifaa vya serikali vinunuliwe kwa jina la taasisi na sio kwa jina la mtu binafsi.

Mhe. Spika, kinachojitokeza kwenye ripoti hii ni mikataba mibovu inayofanywa na serikali na kutojali masharti ya mikataba. Sasa ikija tena kesi nyengine mpya kwamba kuna mkataba mbovu baada ya ripoti hii, basi itaonekana hasa yule aliyefanya amekusudia kweli. Kwa hivyo, lazima uchukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati tulipofuatilia mpaka tukagundua kwa huko kwamba huyo aliyepewa ile *tender* ya kujenga jengo la Wizara ya Fedha kule Pemba, yeye kazi yake ni fundi mirejeji si *contractor* na wala si mjenzi, yaani ni

fundi mifereji pamoja na mambo ya *pipe system*. Kwa hivyo, ikavungwa vungwa na kampuni ikatengenezwa basi, ndio maana mpaka hii leo ikashindikana hata kulitatua. *(Makofi)*

Jambo jengine lililotajwa kwenye ripoti hii Mhe. Spika ni uhaulishwaji wa majengo ya Mambo Msiige. Mhe. Spika, mimi binafsi nimeshazungumza sana humu kwamba huu uuzaji utatufikisha wapi? Kuna baadhi ya mambo hayauziki, kwa sababu inapofika wakati ukaambiwa uuze sura yako wakati ndio inayokupa hiba mbele ya watu kwamba huyu fulani, halafu ukaiuza haifahamiki, yaani Zanzibar tunauza mpaka sura yetu. *(Makofi)*

Sasa nani atakayetufahamu kama ni Zanzibar, kwa sababu kuna mambo ni yetu Zanzibar tu, lakini mambo yale yanauzwa, sasa ni sawa na mtu kumwambia niuzie sura yako. Kwa hivyo, Mambo Msiige pamoja na majengo mengine ni sura ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunapofika wakati tukauza majengo haya Beit-el-Ajab tukaliuza, Mambo Msiige likauzwa, sasa hiyo Zanzibar ya utalii iko wapi? Kwa kweli itakuwa haipo tena. Kwa hivyo, kuna mambo mengine Mhe. Spika pamoja na umasikini hayauziki. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, sisi tuliuliza, kwa sababu hivi sasa wizara ilikuwa ikihangaika kwenda na kurudi *UNESCO*, basi tuliuliza hii haraka ya kuuza ilikuwaje na musiende kwanza huku na kupata uthibitisho, kwamba *UNESCO* hawana matatizo na ubadilishaji wa jengo hili, ikawa sasa ndio mnahangaika. Mhe. Spika, ndipo pale niliposema kwamba kuna baadhi ya mambo hayauziki ni yake mwenyewe mtu ukiuza maana yake ndio umeshajimaliza. *(Makofi)*

Kwa hivyo, serikali itanabahi sasa na mambo yote ya kuuza. Mhe. Spika, leo Chumbe ndio ufunguo wa Zanzibar kutoka Tanzania Bara tena upo na mnara. Sasa leo akitokezea mtu kuinunua na kumuuzia hiyo Zanzibar tena iko wapi? Mhe. Spika, ndio maana nikasema kwamba kuna mambo hayauziki. *(Makofi)*

Nadhani kama kuna kitu ambacho kinakosekana, basi tukiangalia katika mambo ya mikataba. Mhe. Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia serikali iwe ni lazima ithibitishe kama kuuza au kufunga mkataba wowote, lakini ikiwa hapana budi mambo hayendi, basi mikataba mikubwa ipitie katika Baraza la Wawakilishi, mikataba midogo midogo sawa, lakini mikataba mikubwa ambayo italeta mabadiliko katika picha ya Zanzibar ipitie katika Baraza la Wawakilishi na wananchi waisikie. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mwisho kabisa nasema kama haikutekelezwa ripoti hii kwa kiwango kikubwa kama ilivyopendekezwa na sheria zinazoruhusu, basi itakuwa hatukufanya chochote na wala hatukuwafanyia wema wananchi wetu. Kwa kweli suala la uajiri hivi sasa halijulikani liko sehemu gani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba serikali iwajibike kikamilifu kuhusiana na yaliyotajwa katika ripoti hii, ili tuweze kwenda mbele. Kwa upande wa wale mawaziri ambao wamepewa wizara mbali mbali kuzisimamia wao wenyewe kabla ya kuchunguzwa na ripoti kama hii, basi wazichunguze zile wizara zao. Kwa mfano, hivi kweli *staff* wao wanastahiki kuweza kufanyakazi zile zinazojulikana na ikiwa ipo, pengine hawana la kufanya kwa wakati ule, lakini wanajua kwamba ikitokezea nafasi anafanya mabadiliko.

Mhe. Spika, sisi tunakwenda katika kamati ukirudi mambo yako vile vile, kuna taasisi kidogo sana unazokwenda na ukirudi wakati mwengine mambo yamebadilika, kumbe wafanyakazi wetu hawana uwezo, yaani baadhi yao hawana uwezo wa kufanya na wengine ndio hivyo fedha zinatumika ovyo.

Baada ya hayo, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani, ambao wamekereka sana na upotevu wa fedha, kwa sababu ni jimbo ambalo halitizamwi sana na serikali kwenye barabara zake. Kwa mfano, nilisema siku moja hapa Mhe. Spika kwamba njia ya Jimbo la Ziwani ni kama ukuti, yaani wakubwa hawendi. Sasa mimi nikisikia na kila nikienda kudai njia fedha hakuna na ukija huku fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya kununulia *generator* bovu, ambalo haliwezi hata kuwashwa, kwa sababu fedha hizi zikiwa huku zimetumika ovyo ndio wananchi wanakosa kule. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi waliokosa huduma za serikali kwa wingi Jimbo la Ziwani, naomba niunge mkono ripoti hii na niseme kwamba serikali iwajibike, ili mambo yaweze kwenda. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu japo kidogo katika Kamati Teule ya Baraza.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu sisi tuliomo ndani ya Baraza hili tukufu tunao wajibu mkubwa katika kuisimamia serikali, yaani moja katika kazi yetu ni kuisimamia serikali katika shughuli zake zote. Sasa kama moja ya kazi yetu ni hiyo, basi pia katika Baraza letu hili tukasema tuunde Kamati Teule ya Baraza.

Kwa mfano, zamani kipindi kilichopita ilikuwa kuunda Kamati Teule katika Baraza ilikuwa ni vigumu sana. Lakini *Alhamdulillah* hivi sasa suala la kuunda kamati kwa ajili ya kufuatilia mambo fulani haijawa tabu na tumekubaliana na tayari Kamati Teule zipo na tunategemea si hiyo tu, lakini zitakuwepo nyingi Kamati Teule mbali mbali za kuweza kufuatilia shughuli za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali haiwezi kujikosoa wenyewe, hivyo ni lazima kuwepo na watu wa kufuatilia mwenendo wa serikali. Kwa hivyo, kwa jitihada ya Baraza lako tukufu ndio maana ikaundwa hii Kamati Teule kwa ajili ya kufuatilia majukumu ya serikali yanakwenda vipi? Mhe. Spika, kuna ubaya hapo? Mimi sioni ubaya, kwa sababu bila ya kufuatilia majukumu ya serikali, basi serikali hii itakuwa inayumba.

Mhe. Spika, niipe pongezi kubwa sana Kamati Teule hii ya Baraza kwa kazi zake kubwa ambazo ni ngumu na wamefanya ustahamilivu mkubwa na kuweza kuandika ripoti kama hii ambayo ni kubwa na inafaa serikali iangalie kwa makini ripoti hii.

Kwa kweli ripoti ni nzuri, yenye kutupa muelekeo tunatoka na tunakwenda wapi, haiwezekani serikali kuachiwa hivi ikaenda inavyotaka. Kwa maana hiyo, ni lazima kuwepo na watu wa kuikosoa pamoja na kuishauri serikali. Sasa huu ndio ushauri tulioupata na wenzetu wamejitahidi kuweka mtandiko mzima na mimi sioni ubaya ndani yake. *(Makofi)*

Lakini niseme moja kati ya mambo ya Kamati ambalo imelifanya na mimi limenifurahisha, kwamba hii Kamati haifanyi mambo kiholela, yaani haiendi tu ovyo na badala yake imefuatilia kwa kina mambo yake. Kwa mfano, katika suala zima la Kiwanja cha Mtoni, kiwanja hiki ni cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, yaani kilikuwa ni kiwanja chao na vyenginevyo vingi walikuwa navyo.

Sasa Kamati wanaposema kitu kama hiki kimeuzwa ni wajibu wa Kamati hii kukifuatilia kile kiwanja chenyewe, waone kwamba je kiwanja hiki kweli kimeuzwa au hakikuuzwa. Kwa hivyo, ikiwa kimeuzwa, basi kama kimeuzwa Kamati ina wajibu wa kupata taarifa kwamba kiwanja kile kimeuzwa. Je, Kamati pia inataka kujua katika mauzaji haya zimefuatwa taratibu maalum za uuzaji na hiyo ndio kazi ya Kamati Teule. Mhe. Spika, hapa kuna ubaya gani wa Kamati hii, si kazi yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamati hii naipa hongera sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kuweza kutoa taarifa. Kwa hivyo, Kamati inataka ijue sababu za kuuzwa kwa kiwanja hicho, kulikuwa na sababu gani? Kwa sababu ukisema kiwanja kinataka kuuzwa lazima kutakuwa na sababu kwa nini kiwanja hiki kiuzwe kwa maslahi ya nani, maslahi ya umma au kuna mtu binafsi, kazi hiyo ndio waliifanya hao.

Kwa hivyo, baadaye walijua kwamba kiwanja kile kimeuzwa na pengine wao walivyotegemea sio ilivyokuwa, kwa sababu kiwanja kimeuzwa kwa mtu mwengine, lakini hata hivyo wanataka waona katika mauzaji ya kiwanja hiki mkataba wake umekwenda vipi, hivi kuna ubaya gani ndani yake, basi walifuatilia na kuona hali halisi.

Sasa baada ya kufanya uchunguzi huo na kuona vile walivyotegemea kwamba kiwanja kile kiuzwe kwa maslahi ya umma na badala yake hakikuuzwa kwa maslahi ya umma, yaani ameuziwa mtu tu.

Mhe. Spika, dhamira ya ripoti za mauzaji inaonekana kwamba ilikuwa inataka ijengwe Ofisi ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo, dhamira au lengo lilikuwa ni hilo, lakini hakikufanyiwa dhamira yake iliyokusudiwa na badala yake kimeuzwa kwa mtu mwengine. Sasa hawa wamefanyakazi yao kuna ubaya gani.

Mhe. Spika, nafikiri serikali ilikuwa sasa iendelee baada ya mtandiko ambao wao wameuandaa, basi serikali sasa ifuatie kwa sababu hii ni kazi kubwa ambayo wameifanya kwa uangalifu sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, jambo jengine ambalo wamelifanya wenzetu nalo ni muhimu pia katika suala zima la ujenzi wa uzio ulioko katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume. Kamati Teule hii moja katika kazi zake kubwa ilikuwa inataka kujua ulipaji wa fidia ya hawa ambao katika kujengwa huo uzio wenyewe, kwa sababu uzio ulitaka kujengwa kwa kupitia sehemu za wananchi. Sasa bila ya shaka Kamati Teule hii lazima iende ikajue utaratibu mzima wa uzio huo, mali iliyokuwo ambayo itaathirika kwenye uzio huo na bila ya shaka mulikuwa na mambo mengi katika eneo hilo. Kwa maana hiyo, uzio uliathiri nyumba za wananchi na katika

kuathiri nyumba za wananchi ingawa wenyewe hawaridhiki, lakini sasa ni lazima kwa sababu ni suala la kitaifa uzio lazima ujengwe na tayari umeshajengwa na nyumba zimevunjwa.

Pamoja na hayo, tuangalie baada ya kumvunjia mtu nyumba yake kunahitajika kitu gani, watu lazima wapate fidia ya kuvunjiwa nyumba zao. Mhe. Spika, hilo ndilo walilolifanya Kamati Teule ya kuona umepita uzio na ndani ya uzio umeathiri nyumba za wananchi, kilimo, matunda, miti iliyokuwemo ndani ya eneo lile.

Kwa hiyo, lazima wajue je hawa wamepata fidia au hawakupata, kuna kosa hapo na wala hakuna kosa ndani yake, nafikiri walichokifanya si kibaya kutaka kujua hali halisi.

Mhe. Spika, uzio huo umeathiri nyumba za wananchi pamoja na mazao mbali mbali yaliomo humo. Kutokana na hali hiyo, serikali lazima itoe fidia katika malipo. Sasa wanachokiangalia wao kama kweli fidia imekwenda kwa mujibu au uhalali kamili kutokana na nyumba walizonazo. Kwa mfano, mtu anaweza kuvunjia nyumba ya gharama kubwa na kulipwa fedha kidogo au miti ambayo iliyokuwemo ndani ya eneo lile ikakatwa miti yote na pengine asipewe kitu ama malipo aliyopewa hayalingani.

Kwa hivyo, wao walifanya suala hili na kulipitia vizuri na kuona, pia walihitaji kutaka kujua na kuingia ndani zaidi kutaka kuona namna gani malipo yalifanywa kwenye suala hili zima. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hawakuweza kuyapata yote, lakini walijitahidi katika kutafuta taarifa mbali mbali na kwa bahati waliona kwamba waingie kwenye *payment vouchers*.

Sasa katika *payment vouchers* bila ya shaka utapata kujua nani amelipwa na nani hakulipwa, kwa sababu unapopelekewa *voucher* ni lazima itie sahihi yako. Kwa mfano, umepewa shilingi 200/= au shilingi milioni 2 unatia sahihi yako kwa ajili ya kuonesha kwamba umepokea fedha zile. Mhe. Spika, hili ndilo walilolifanya wenzetu.

Kwa maana hiyo, wamepitia na katika kupitia wao wameona hali halisi katika mambo haya hayakutimia sawa kama inavyotakiwa, wengine walikuwemo na wengine hawakuwemo na hayo ndio waliyoyafanya. Mhe. Spika, hapo inabidi serikali ifuatilie uhalali wa suala hili, kwa sababu wanaofanyiwa haya ni wananchi wetu na wananchi wako chini ya mikono ya serikali. Hivyo, ni vyema serikali iweze kufanya kila jitihada ya kuona kwamba wananchi wamefaidika na athari zilizowafika. Mhe. Spika, kilichogundulikana ni kipi baada ya yote hayo. Kwa kweli hapa tunachokiona sisi ni kwamba Mhasibu bila ya shaka atakuwa anahusika kikamilifu kwa malipo ya watu hawa.

Mhe. Spika, Mhasibu huyu akuweza kufuata Kanuni za Fedha, kwa sababu zipo Kanuni za Fedha, malipo na wala hakuzifuata hizi, kwa sababu kama angekuwa amezifuata hizi Kanuni za Ulipaji wa Fedha, basi angeweza kuwalipa vizuri na malipo yakaonekana pamoja na sahihi. Mhe. Spika, baadaye nitatoa ushauri mbele huko kuonesha namna gani watu hao wajipange katika kazi zao.

Kwa kweli hii ni serikali Mhe. Spika na wala si Chama cha Ngoma, ingekuwa Chama cha Ngoma tungefanya tunavyotaka, lakini hii ni serikali basi ni lazima watu waweze kuwajibika katika shughuli zao vizuri. Kwa mfano, mtu akipewa kwenye *Job Description* umepewa kazi maalum, basi ni lazima kazi uliyopewa uweze kuifanya vizuri tena kwa uhakika na ukamilifu. Kwa hivyo, watu wengine wanafanyakazi kwa kubaisha tu na kuondosha njiani.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye suala la ajira. Mhe. Spika, suala la ajira katika nchi hii bado ni gumu sana na linawapa wasi wasi wananchi wengi suala hili, kila mtu ambaye yuko katika nchi hii anahitaji ajira. Kwa kweli watu au wanafunzi wengi baada ya kumaliza masomo yao wanahitaji kupata ajira hata kama hizo ajira haziwezi kuwatoshelewa watu wote waliomo katika nchi hii, lakini kila mtu anapenda kusoma na anapomaliza basi anahitaji kupata ajira.

Lakini huu utaratibu wa ajira ndio unaowahangaisha wananchi hawajui utaratibu gani unaendelea, yaani ajira zinakwenda kinyemela na hii ndio hali halisi na wananchi wanapiga kelele, kwa sababu wanaona watu wanapatiwa ajira, lakini sasa utaratibu watu hawaufahamu isipokuwa wanawaona watu wanapatiwa ajira tu. *(Makofi)*

Kwa kweli utaratibu hawauelewi jinsi gani watu wanaajiriwa na ukienda kuuliza kuhusu habari ya kazi utaambiwa kazi hapana, yaani ajira zinakwenda kwa sekta maalum. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, lakini ukienda sehemu nyengine ajira zinaendelea kama kawaida.

Mhe. Spika, katika Kamati Teule hii ilikuwa pia inafuatilia suala zima la ajira, kwa kweli imefanyakazi ya kuona hali halisi. Kwa hivyo, Kamati imeweza kugunudua baadhi ya mambo. Kwa mfano, imeweza kugundua mfanyakazi ambaye ameajiriwa bado yuko masomoni, inawezekana mfanyakazi ameajiriwa, lakini bado anaendelea kusoma. Kwa maana hiyo, ni wajibu wao kuona watu wangapi wameajiriwa na bado wako masomoni na hiyo sio mbaya.

Vile vile ilihitaji kujua Kamati Teule hii mtu ambaye aliajiriwa zaidi ya mara moja, ni wajibu wao kufuatilia Kamati hii, ili ione huyu ambaye ameajiriwa *once* au mara mbili ama tatu, pengine imeshawahi kutokezea mtu huyo mmoja anaajiriwa zaidi ya moja, yaani huku na kule ameajiriwa. Kwa hivyo, kuna ubaya gani watu hawa kuifanya kazi hiyo, nadhani wanaisaidia serikali kuweza kujua watu wangapi walioajiriwa na wameajiriwa vipi?

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo Kamati iliweza kulifanyiakazi wameona kwamba kuna ajira ambazo ni kutoka Tanzania Bara kupitia Pemba moja kwa moja. Lakini hao waliopitia katika njia hizo pia na wao walionekana kuwa ni Wazanzibari. Kwa hivyo, hicho walichokifanya ni kuijuilisha serikali mwenendo mzima wa ajira uko vipi. Nadhani haya ni mambo muhimu.

Kwa maana hiyo, ninachosema katika suala hili, ili katika Utumishi wa Umma au sehemu nyengine yoyote ya ajira, basi hizi ajira zisitolewe kiholela na badala yake ziende kwa mnasaba wa mtu na kazi ambayo anataka kupewa. Lakini ukichunguza katika mawizara yetu, basi wizara nyingi utawakuta watu ambao wameajiriwa na pengine hawana uwezo, ujuzi na hata pamoja na kukaa elimu yake ni ndogo. Kwa hivyo, ikiwa elimu yake ni ndogo hata mtu yule umemuweka miaka 10 au 15, ili aweze kujiendeleza kwa sababu uwezo wake wa kielimu ni mdogo, basi mtu yule hawezi kuzalisha kitu na tunataka watu ambao wanaoweza kuzalisha katika mawizara.

Mhe. Spika, hatuwezi kuchukua mkururo watu tukawaingiza katika mawizara na kusema *for the sake of public interest*. Kwa maana hiyo, tunachagua watu ambao huyu ukimpa kazi basi ataweza kuifanya. Kwa hivyo, elimu ya mtu, uwezo na hata nidhamu, yaani *discipline* katika kazi ni muhimu, lakini sasa *discipline* katika kazi hamna, mkubwa haheshimiwi, mdogo anakuwa na maneno mengi kuliko mkubwa.

Mhe. Spika, katika kumtafutia mtu ajira, basi ni lazima mtu awe na *discipline* na wala tusiokote tu watu, kwa sababu mtu mnamfanyia *interview* pamoja na kumchunguza mtu katika kumpatia ajira na wala ajira hazitolewi hivyo tu. Kwa hivyo, ni vyema kumuona mtu huyu ni mwenye nidhamu, pengine huko anakotoka ni mtu ambaye hana nidhamu nzuri na wala hatuwezi kumpa mtu ajira ambaye hana nidhamu sawa, kwa sababu tuanze kumlea yeye kwa nidhamu na halafu tumpe kazi, sasa hiyo kazi atakayoifanya itakwenda vipi na mtu hana *discipline* hata huyo mkubwa wake pengine iko siku anaweza kumtukana humo ndani.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo si vibaya kwa Kamati Teule hii kuangalia katika suala zima la ajira kuangalia idadi ya wafanyakazi, pengine wafanyakazi wamekuwa ni wengi sana kuliko idadi ambayo inahitajika. Kwa hivyo, Tume ya Utumishi nchini ina wajibu kuangalia idadi ya wafanyakazi waliopo na tunaowahitajia kwa mujibu wa mahitaji tunayoyataka.

Kutokana na hali hiyo, mimi sitaki niendelee sana katika haya, isipokuwa kuna mambo angalau hawa ambao wenye dhamana, maana yake *responsibility*. Kwa mfano, kuna watu wamepewa *responsibility* labda mtu hakuwajibika na yeye anaangalia madughuli tu na haya mengine ameyatupa, anasibiri mwezi uandame madughuli yatakuja vipi apate kirambi mambo yamalize. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni vyema kuangalia utaratibu mzuri wa kusema hao watendaji wa serikali, nafikiri tuangalie katika wizara pamoja na taasisi zote. Kwa mfano, wizara au taasisi yoyote inataka kuuza au kununua kitu na hayo ni mambo muhimu katika wizara, kwa sababu wizara inaweza kununua au kuuza kitu, kama vile magari pamoja na vifaa vyengine mbali mbali vya afisini.

Sasa kama mambo ni haya inataka kuuza na kununua au kuuza viwanja vya serikali, basi ifuate sheria pamoja na taratibu za mauzaji na manunuzi. Mhe. Spika, sasa kama mambo haya wanayaelewa na wakifanya kwa makusudi kuwa zipo taratibu katika taasisi zetu za kuuza na kununua, kama vile kuuza viwanja, magari au kununua vitu mbali mbali vya afisi vinavyohitajika, basi lazima kutakuwa na utaratibu maalum.

Kwa hiyo, hawa wanawajibika wafuate sheria na taratibu za mauzaji na manunuzi kwa ajili ya serikali, kwa sababu hawa wanasimama kwa ajili ya serikali. Mhe. Spika, hilo ni jambo muhimu kwa watu wetu na ninawausia wafanye hivyo na wala wasiende tu wanavyotaka wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ama vyenginevyo itakuwa watu hawa wakifanya kinyume na haya ninayoyasema, basi itakuwa watu hawa wamekiuka sheria na taratibu za serikali. Sasa mtu ambaye amekiuka taratibu na sheria ya serikali afanywe nini? Aachiliwe tu na tayari ameshaambiwa kwenye taratibu hizi unatakiwa ufanye hivi na vile na wala hakufanya vile inavyotakiwa. Kwa hivyo, hapa ni lazima mtu yule unaweza kumchukulia hatua kidogo za kumuweka sawa.

Vile vile katika kuuza kama tunauza viwanja basi tuuze viwanja, ili kero au balaa lisitokezee, kwa hivyo tukiuza hivi viwanja tuone kwamba kile tulichokiuza kina thamani ya mauzaji, yaani ile fedha inayopatikana ilingane na kile kitu chenyewe. Kwa mfano, inawezekana ardhi ni kubwa sana, lakini fedha zilizochukuliwa kutokana na kiwanja kile fedha ni kidogo na hapa bila ya shaka pamepita mambo. Kwa hivyo, haya ndio mambo tunayoyakataa uwe muwaminifu tunasema uaminifu na uadilifu ni kitu muhimu sana, sasa mfanyakazi wa serikali ameajiriwa katika kuisaidia serikali lakini bado haisaidii serikali inakuwa serikali anaimaliza. Kwa hivyo hapa thamani ya uuzaji ilingane na ukubwa wa kiwanja chenyewe hiyo ndio kitu muhimu.

Jambo jengine kwa watu kama hawa walioko katika maofisi wajaribu kufuata taratibu za utawala, *administration* kwa sababu kila wizara inao utaratibu wa *administration* kwa nini hataki kufuata utaratibu huyu mtu apewe habari zake aelezwe kwamba bwana wewe hufuati taratibu za utawala.

Mhe. Spika: Mheshimiwa zingatia muda.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Inshaalla kwa hivyo mikataba itakayotolewa iwe wazi vile vile Mheshimiwa, kamati ya PAC ipewe taarifa sahihi wasipewe taarifa potofu watendaji wote tunawaomba wafuate maadili ya kazi ya serikali, viongozi wasitumie madaraka yao vibaya kila kitendo kitakachofanywa waangalie kanuniz za wizara wasiamue mambo kuangalia nafasi au uwezo wao walioupata. Vile vile watu kama hawa wasibebe madaraka yasiyokuwa yao, watu wengine utamuona wanapewa kazi hizi utamuona mtu anataka achukue mambo yaliyokuwa sio yake yeye, hapa kila mtu kapewa kazi zake kwa nini unataka kubeba mambo yaliyokuwa sio yako, wako wengine wanapenda hao kuchukua mambo makubwa ya wenziwao wakati sio yao.

Kwa hivyo akaona kwamba yeye kutokana na nafasi aliyopewa hakuna mtu wa kumhoji, halafu vile vile katika hayo namalizia kumbu kumbu katika wizara zetu hazionekani, risiti hazionekani baada ya mauzaji na manunuaji, kwa hivyo tunasema risiti ziwepo za manunuzi na mauzaji ni jambo muhimu, waweke kumbu kumbu ya mali ya serikali. Vile vile waweke hadidu rejea haya ni mambo muhimu ambayo najaribu kuwasaidia hawa ambao wamepewa dhamana.

Mhe. Spika, naheshimu wakati wako ijapokuwa kuna mengi ya kuzungumza, lakini nashukuru kwa hivyo na mimi naunga mkono ripoti hii mia juu ya mia. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kamati teule, kwanza naipongeza kamati teule kwa kazi nzuri ambayo wametuletea na kuweza kutuelimisha mengi ambayo tulikuwa hatuyafahamu.

Kamati teule hii ni nzuri na imefanya kazi zake kima ilivyoagizwa na Mhe. Spika, ili kutuleta katika baraza hili, nashukuru imefanya kazi nzuri na safi na ambazo zimeleta haki za kuwajibika watu wanaohusika, pale pale naikumbusha kamati teule kazi iliyofanya ni nzuri isipokuwa naomba tu kamati teule tuipe uwezo zaidi kuleta mengi sio kwa awamu ya sita tu lakini ianze kwenye awamu ya pili ambapo ndipo kulipoanza mchafuko wa hali ya hewa, tukisema tufanye awamu moja tu hivyo itakuwa hatukuipa haki kamati teule na wala hatukuipa uwezo wa sheria kuweza kututafutia habari zote tulizozihitaji. Kwa sababu tunaelewa wazi kipindi kilichopita awamu zote kuanzia awamu ya pili hadi kufikia awamu ya sita serikali ilikuwa na uamuzi wake na vyovyote ilivyokuwa inachukua ilikuwa ni sawa. Nafikiri awamu zilizopita si jambo geni kwa kiongozi yoyote kupewa nyumba bure ama kupewa gari bure ama kupewa gari kwa pesa kidogo, ama nyumba kwa pesa kidogo hiyo ilikuwa ni haki moja kwa moja. *(Makofi)*

Kwa hivyo ni nafasi nzuri kamati teule ingelipitia yote ambayo tunahitaji kuyapata kwenye hii awamu ya saba, kwa sababu awamu ya saba ni awamu ya serikali ya kitaifa, kwa hivyo serikali ya kitaifa inayo haki ya kuchangia yote ambayo wanahitaji tukaacha yale ya zamani. Kwa sababu tukifuata yale ya zamani itakuwa tunachangia kuwashirikisha awamu ile ambayo ya upande wa chama kimoja tu, lakini hii ya kitaifa ni ya vyama vyote, kwa hivyo sio kosa kwa hivi sasa tukaweza kuchangia kuanzia awamu ya pili ama tukaanza kuchangia kama ulivyo itoa kamati teule kwamba imeanza katika awamu ya saba na tukapiga mstari tukaanza kutafuta ya awamu ya saba tu. *(Makofi)*

Tukisema tutafute ya awamu ya sita au awamu nyengine tu ndogo itakuwa tumevunja sheria au tumewavunjia haki wengine wengi, kwa sababu tunaelewa wazi viongozi waliopita sijui kama wote walikuwa wasafi kiasi hiki, kwa hivyo mimi sitokuwa na mengi sana ya kuzungumza isipokuwa kuhakikisha kwamba kamati ipewe meno irudie sehemu yake na ichangie hasa mambo kuanzia awamu ya pili.

Kwa sababu mimi naona mimi mwenyewe sikufanyiwa haki kwa sababu katika kamati hii nilitaka niwemo na sikupata hiyo nafasi, kwa sababu nayafahamu mengi ya awamu ya pili na awamu nyengine, naweza kukwambia mimi mwenyewe ni mmoja wapo katika waliopitia nafasi ya jeshi la wananchi wa Tanzania na nilikuwa katika kambi ya Mtoni muda mrefu, nilikuwa najua habari nyingi hasa pale kwenye *deport* ya mafuta pale Mtoni naelewa ilikuwa vipi na imeuzwa. Mimi mwenyewe nilikuwa jeshini nimekaa sana katika kambi ya Iddi Bavuai Camp sehemu ya Migombani, nawelewa vibanda kuanzia Migombani sehemu nyingi ilivyouzwa kiholela wakati huo.

Sasa tukisema kwamba tunaichangia awamu ya sita wazi tumeivunjia haki vibaya sana serikali, tukitaka tuwe safi tuanze kuchangia awamu ya pili. Ahsante Mhe. Spika, sina zaidi naiunga mkono kamati asilimia mia kwa mia mimi na wananchi wangu wa jimbo la koani Asante sana *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau kwa mawili matatu hivi nipate kuchangia ripoti hii ya kamati teule ya Baraza la Wawakilishi, ripoti ambayo imewasilishwa jana.

Mhe. Spika, kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kuunda kamati hii kwa mujibu wa kanuni zetu za baraza, kamati ambayo kama wenzangu walivyotangulia katika miaka kumi iliyopita ilikuwa ni uwezekano mdogo sana kuweza kuundwa, lakini tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba katika kipindi hiki imeweza kuundwa.

Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa kamati teule Mhe. Omar Ali Shehe namna alivyowasilisha ripoti yake kwa ujasiri na umahiri na utulivu wa hali ya juu, pamoja na kwamba aliweza kunywa gilasi za maji kama nne hivi lakini hatimae ameweza kuimaliza, lakini pia niwapongeze wajumbe wakamati hiyo ambao wameshirikiana nao kwa pamoja katika kufanya kazi hizi ambazo baraza lako tukufu liliwapa kwa ajili ya kutufanyia utafiti.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuchangia ripoti hii naomba kwanza nitoe maelezo yafuatayo kwa ruhusa yako. Mhe. Spika, Chama cha Mapinduzi kina taratibu zake na miongozi na mambo mengine lakini katika taratibu zake Chama cha Mapinduzi kina katiba yake, kuna ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi, lakini pia kina mwelekeo wa sera za msingi ambazo vyote ninavyo hapa. Lakini katiba yetu ya Chama cha Mapinduzi ina ahadi yake na kwa lugha nyengine tunaweza kusema ni kiampo, pale mwanachama wa chama cha mapinduzi anapopewa kadi ya chama cha mapinduzi basi huwa anakula ahadi kama ni kiapo na kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba nikinukuu.

Kiapo hicho kinasema kwamba.” Binaadamu wote ni ndugu zangu na afrika ni moja nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote, nitajitolea nafsi yangu kuondosha umasikini, ujinga magonjwa na dhulma, nne inasema rushwa ni adui wa haki sitapokea wala kutoa rushwa, lakini pia katiba hii inasema cheo ni dhamana sitotumia cheo changu wala cha mtu mwengine kwa faida yangu, nitajielimisha kwa kadiri ya uwezo wangu na kuitumia elimu yangu kwa faida ya wotem, nitashirikiana na wenzangu wote kujenga nchi yetu, nitasema ukweli daima, fitina kwangu ni mwiko, nitakuwa mwanachama muaminifu wa CCM na raia mwema wa Tanzania na Afrika”. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii ni ahadi ya chama cha mapinduzi na kama ni kiapo kwa chama kwa maana hiyo Mhe. Spika, kiongozi yoyote wa chama cha Mapinduzi au mwanachama wa chama cha mapinduzi atakayekwenda kunyume na haya maana yake anakiuka taratibu za chama na kutokuwa mwaminifu kwa chama cha mapinduzi.

Lakini pia kuna mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya 2010/2020 nitanukuu mahala padogo tu kwa ruhusa yako ambayo ni sura ya sita inazungumzia utawala bora demokrasia na madaraka ya wananchi, kifungu cha 115c kinasema “Chama cha Mapinduzi kitahakikisha kwamba serikali inayozingatia uwazi katika kuendesha masuala ya nchi, kuimarisha usimamizi na matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za umma, uadilifu katika utendaji katika kuzingatia misingi ya sheri, uwajibikaji na kujenga utamaduni uliojengeka nchini na kubadilisha uongozi wa juu katika nchi kwa amani na mashirikiano kwa faida ya taifa letu na kukamilisha zoezi la kuipatia upya sheria zinazoongozana kwa lengo la kuimarisha demokrasia na utawala bora na haki za kijamii”.

Mhe. Spika, kwa nini nimeanza na nondo hizi za Chama cha Mapinduzi kwamba chama chetu cha mapinduzi hakikubaliani na njia yoyote ya upokeaji wa rushwa, lakini pia mbali na rushwa kinahimiza uwajibikaji na utendaji kazi, kwa hivyo hiyo ndio misingi ya chama cha Mapinduzi, kwa hivyo mwanachama yoyote

anayefanya mambo yanayokwenda kinyume na misingi ya chama cha mapinduzi hayo yanakuwa ni mambo yake mwenyewe binafsi sio chama. Wala chama cha Mapinduzi hakiwezi kubeba msalaba wa mtu wa aina hiyo, inakuwa lake na sio la chama cha mapinduzi.

Mhe. Spika, sasa baraza lako tukufu limeanza kufanya kazi zile za kusimamia serikali kwa mujibu wa katiba yetu ibara ya tano, ambayo kwamba katiba imempa madaraka baraza la wawakilishi kusimamia shughuli zate za serikali ikiwa ni pamoja na kwamba ni shughuli za umma. Kwa hivyo ripoti yetu hii ambayo imewasilishwa hapa na kamati teule ya baraza inaelekea kwenye kusiamia serikali.

Mhe. Spika, tumeona hadudi rejea ambazo tayari zimewasilishwa na zimeshafanyiwa kazi ambazo hadudi rejea hizi ziko kama tisa zimechambuliwa katika kitabu hiki, zimetolewa ufafanuzi wa kutosha pengine yanaweza kuwemo makoseo ya kibinaadam lakini tunaamini kwamba karibu asilimia tisini ya taarifa hii inaweza kuwa na ukweli ndani yake. Kwa hivyo nafasi hii ambayo imepata au chombo chako hiki kimepata tuitumie vizuri katika kuhakikisha kwamba tunaisimamia vyema serikali yetu kwa lengo la kuona kwamba inakwenda vizuri kwa manufaa ya wananchi na si vyenginevyo.

Katika hadudi rejea ambazo zipo nitaanzia hii ya uhaulishwaji wa kiwanja cha Miundombinu na Mawasiliano ambacho kipo kwenye aneo lilipokuwa karakana ya Wizara hiyo eneo la Mtoni Mjini Zanzibar, kwa kweli nimejaribu kusoma na kuipitia ripoti hii lakini kinachoonekana kwenye ripoti hii ni tatizo la ukiukwaji wa taratibu za kisheria na kanuni ambazo tumejiwekea *(Makofi)* pengine Mhe. Waziri wa Wizara hiyo aliyepita ambae kwenye ripoti hii amezungumzwa sana, pengine aliyafanya haya kwa sababu ya nia njema pengine na kwa sababu Ofisi yake au jengo lake lilikuwa ni bovu na akahisi hakuna uwezekano kwa wakati ule kulitengeneza na ndio maana akawa katika harakati za kuona kwamba atafute utaratibu au njia ya kupata ofisi kwa ajili ya kuendesha shughuli za serikali pengine.

Lakini baada ya kuangalia zaidi na kutafakari zaidi nikaona hata ile azma ambayo alikuwa nayo kwa wakati hule haikuweza kutimizwa kwa kipindi kile, adhma ilikuwa ni kuhaulisha au kuuza kiwanja kile na kwenda kujenga kiwanja chengine kwa kujenga *foundation* au nyumba kwa ajili ya Ofisi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini pengine sivyo hivyo jengo hilo mpaka sasa hivi halijaanza kujengwa, sasa mimi nimekuwa na mashaka juu ya jambo hilo na pengine hakuwa na dhamira hiyo alikuwa na dhamira nyengine.

Mhe. Spika, kwa sababu hamu ni kitu kibaya Mhe. Waziri aliona kuwa alikuwa na hamu ya kuona anakuwa na jengo lake ikampitikia hamu ile kukiuka taratibu na sheria, lakini sasa ile hamu haikuendelea ilikatika na hatimae ameshindwa kuwasilisha mchoro wa huyu mtu ambae ameuziwa hichi kiwanja na hatimae jengo hili mpaka sasa hivi halijajengwa.

Sasa ukweli hili ni tatizo la ukiukwaji wa sheria na kanuni ambalo wenzetu waheshimiwa mawaziri na watendaji ni lazima mara zote wajaribu kufuata taratibu za kisheria na kikanuni ili kuepukana na masuala kama haya, kama mheshimiwa waziri angefuata taratibu na kanuni nadhani leo tusingekuwa tunazuangumzia jambo hili. Lakini kwa kuwa sheria na kanuni hazikufuatwa maana yake sasa leo tunazungumzia suala hilo ambalo tunalijadili.

Mhe. Spika, kamati imetoa mapendekezo juu ya hatua za kuchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo, mimi nakubaliana zaidi pamoja na haya mengine hili la mwisho ambalo linazungumzia naomba kunukuu Mhe. Spika, linasema. “Uhaulishwaji huu sio halali kisheria na kiutawala hivyo kamati inapendekeza kiwanja hicho kirejeshwe serikalini mara moja”.

Mimi naungana na hoja hii au pendekezo hili na kwa sababu serikali bado ina mahitaji makubwa sana ya maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuendesha shughuli zake, kwa kuwa sheria haikufuatwa na kwa kuwa mhusika mhaulishwaji hajapatiwa hata *single sent* kwa ajili ya ujenzi wa Wizara ya Mawasiliano basi kiwanja kile na hata kama kilikuwa kimeshatolewa hati, basi hati ile ifutwe na serikali na kirejeshwe mikononi mwa serikali na hili linawezekana, na ikiwezekana katika kufuatilia hili waziri anayehusika na wizara hii atoe taarifa kabla ya kikao cha bajeti taarifa inayoonyesha kwamba kiwanja kile tayari kimefutwa na kimerejeshwa serikalini kabla ya kikao cha bajeti au wakati wa kikao cha bajeti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hadidu rejea nyengine inazungumzia suala la uwanja wa ndege wa Zanzibar kwa kweli inasikitisha kuona mambo ya ukiukwaji wa taratibu yanafanywa na watendaji wetu wa serikali, mambo ambayo yanasababisha serikali kukosa fedha nyingi na ripoti hii imeeleza mambo mengi kuna maduka kadhaa wa kadhaa hayana mikataba ama mikataba waliyokuwa nayo imeshapitwa na wakati, fedha zinazohusika na mikataba hiyo hazilipwi kikawaida fedha nyingi za wananchi zinapotea. Kwa kweli inasikitisha na inaonyesha

jinsi gani watendaji wetu ambao tumewachagua au tumewateua kwa ajili ya kuisimamia na kushughulikia masuala ya serikali jinsi wanavyoshindwa kutekeleza wajibu wao.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na taarifa iliyowasilishwa hapa au pendekezo lililowasilishwa hapa ya kuchukuliwa juu ya uamuzi huo wa maeneo haya ya biashara ambayo Mkurugenzi wa Mamlaka hii anahusika kwa namna moja au nyengine, kwa sababu Mkurugenzi pengine kabla ya kuwa Mkurugenzi kwa mujibu wa taarifa hii alikodishwa hanga kwa dola 200 kwa mwezi, lakini na yeye baada ya kukodishwa amemkodisha kampuni ya *ZAN AIR* kwa dola 1000 ina maana anapata faida ya dola 800 kila mwezi za bure.

Jambo hili linahitaji kuchukuliwa hatua kwa sababu kama serikali yetu hii tunaigeuza kama shamba la bibi kila mtu anakwenda kuvuna hivi tutaipeleka katika pahali pabaya, hata wananchi wetu watakuwa hawatuelewi katika hili.

Huku tukizungumzia umasikini uliokithiri lakini kuna baadhi ya watendaji wetu wananufaika na serikali, wanachukua fedha nyingi wanajinufaisha wao wenyewe na familia zao jambo ambalo sio la kupendeza hata kidogo, nakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa juu ya jambo hili.

Mhe. Spika, eneo jengine kuhusu utaratibu wa ajira kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Unguja na Pemba, kwa kweli taarifa hizi zinasikitisha huku wananchi wetu wakilalamikia suala zima la kupata ajira lakini inasikitisha kwamba ajira zilizofanywa katika Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu imejaribu kuajiri wafanyakazi bila ya kupata taarifa, bila ya kufuata taratibu wakati ajira hizo wapo vijana wetu watoto wetu wengi wanazihitaji, kwa kweli inasikitisha. Ripoti iliyotolewa na Kamati juu ya wafanyakazi hawa wameelezwa mmoja baada ya mmoja, elimu yake, namna alivyoomba, namna ya ubadhilifu aliyoufanya, namna ya udanganyifu alioufanya kwa kweli inasikitisha.

Mhe. Spika, serikali inahitaji kuchukua hatua zinazostahiki juu ya jambo hili. Mimi nakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na kamati. Kidogo kumekuwa kuna mkanganyo juu ya taarifa ambazo zimetolewa kuhusiana na suala la ajira. Kuna maelezo yanayosema kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi haikushirikiana na Wizara ya Utumishi katika masuala ya ajra. Kwa maana hiyio imejifanyia yenyewe tu bila ya kushiriki na Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kuna maeneo inaonekana kwamba hata Wizara ya Utumishi nayo imehusika. Katika hatua za kuchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo inasema kwamba viongozi na watendaji wakuu wa Wizara zote mbili Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndio waliohusika na kadhia hii wawajibishwe kisheria. Kwa maana hiyo inaonekana kulikuwa na mashirikiano. Kwenye maelezo ya mwanzo inaonekana kwamba Wizara ya Mawasiliano au Wizara ya Miundombinu na uchukuzi ilijifanyia wenyewe utaratibu wa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani utakuja kutupa kidogo uwazi pengine wakati tunapopitia haya hatukuwa sawa. Hebu tupe uwazi jinsi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilivyohusika na jambo hili.

Mhe. Spika, jengine hadudi rejea nyengine ni kuhusu uhaulishaji wa kiwanja kinachopakana na *living stone house*. Maelezo yametolewa yamewagusa watu wengi, Kampuni na *F&K enterprises*, jinsi walivyokipata hichi kiwanja, jinsi baadaye kilivyouzwa. Taarifa inaeleza kwamba lengo na madhumuni ya kupewa kiwanja hiki hii Kampuni ya F&K ni kufanya biashara. Ilikuwa si jambo baya.

Lakini kama nilivyotangulia kusema hapo awali, serikali sasa hivi ina mahitaji makubwa sana ya ardhi kwa ajili ama ya kujenga ofisi zake au kufanya shughuli mbali mbali. Si vyema maeneo kama haya hasa yaliyokuwa mijini ambayo yanamilikiwa na serikali kupewa watu binafsi. Ni bora watu aina hii tuwape ardhi katika maeneo mengine. Tatizo ni kwamba hii kampuni iliyopewa kiwanja hiki kwa ajili ya kufanya biashara, lakini baada ya mwezi mmoja tu kiwanja hicho wakakiuza wakamuuzia mtu mwengine kwa zaidi ya shilingi milioni 200. Wakati kampuni hii kiwanja hicho ilipewa bure na serikali. Kwa kweli hapakuonesha uwadilifu hata kidogo.

Kwa sababu tu kwamba Kampuni hii *F&K* haikuwa na uwezo wa kuliendeleza eneo hilo kibiashara. Haiwezekani ndani ya mwezi mmoja ukafikia uwamuzi kama huo. Unepewa ardhi ndani ya mwezi mmoja unauza kwa sababu kwamba umeshindwa kukiendeleza. Nadhani mimi nikubaliane na taarifa ya Kamati kwamba pengine biashara iliyokusudiwa pale ni kupewa nakuuza. Zaidi ripoti inasema uhaulishaji wa kiwanja hicho haukuzingatia masharti ya utolewaji wake kama yalivyokusudiwa na sheria hiyo kamati inapendekeza kiwanja hicho kirudi serikalini mara moja. Mimi nakubaliana na wazo hili mia kwa mia kwamba kiwanja hichi

kirudi kwa wananchi wenyewe kwa manufaa ya nchi na Waziri anayehusika kabla ya Kikao cha Bajeti au wakati wa kikao cha bajeti basi atupe taarifa namna alivyoweza kutekeleza agizo hili la Baraza.

Mhe. Spika, hadudi rejea ya pili kutoka mwisho ambayo ningependa niizungumzie ni namna ya kutafuta ukweli kuhusu matatizo kwenye ujenzi wa jengo jipya la Wizara ya Fedha Chake-Chake Pemba. Nimekuwa na masikitiko makubwa sana juu ya taarifa iliyotolewa na Kamati Teule. Nimekuwa na masikitiko kwa sababu moja kubwa, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Baraza la Wawakilishi kwa muda mrefu kidogo. Kati ya kamati ambayo ilisisitiza ujenzi wa jengo hili ni Kamati ya Fedha na Uchumi, tokea Baraza lililopita.

Mhe. Spik, wenzetu wa Wizara ya Fedha Pemba walikuwa hawana jengo la kufanyia kazi lakini walikuwa wanavyo vifaa vingi vya kisasa. Tunapowatembelea huna hata pa kuweka mguu. Msisitizo wetu ulikuwa mkubwa ni kuitaka serikali ijenge jengo la Wizara ya Fedha Pemba kuondosha matatizo hayo. Baada ya kelele nyingi hatimaye Wizara ya Fedha na Uchumi ikathubutu kuitisha tenda kwa ajili ya ujenzi ule. Matokeo yake kama vile yalivyojitokeza. Lakusikitisha zaidi kamati yetu kila inapoulizia juu ya jambo lile basi watendaji wanatwambia kwamba mambo yalikwenda vizuri, tenda ilitangazwa vizuri. Waliopewa tenda ile ni watu wazoefu, wana uwezo wana hiki na hiki lakini ndio bahati mbaya watatulipa, watafanya hivi. Ni lugha ambazo zinaonesha kwamba Watendaji wa wizara hawakuwa na kasoro yoyote juu ya upitishaji wa tenda ile.

Mhe. Spika, baada ya Kamati kuingia ndani imebaini kwamba yule *contractor* aliyepewa ile kazi hana utaalamu wowote na amekiri mwenyewe. Hatuelewi ni vipimo gani ambavyo wenzetu walivitumia katika kumpaka *contractor* yule, wakati yeye mwenyewe amekiri kwamba siyo mkandarasi. Asipokuwa anapopewa kazi anawatafuta mafundi wanakwenda kujenga. Ni vigezo gani walivyovitumia hatimaye kwamba jengo lile halijakamilika, limekuwa halifai na fedha za serikali zaidi ya milioni 700 zimekwenda.

Kwa kweli jambo hili ni la kusikitisha. Tuwaombe sana wenzetu wanapopewa dhamana hizi za kusimamia masuala ya umma wawe na uchungu wa fedha za serikali, wawe waadilifu. Wahakikishe kwamba yale majukumu waliyopewa na umma basi wawe wanayatekeleza. *At list* jengo lile lingekuwa limesimama sasa hivi linatumika, basi tungesema kwamba wamefanya jambo la maana, fedha imekwenda na hakuna kinachoendelea. Lengo lililokusudiwa la kupata ofisi halipo, bado matatizo yapo pale pale. Hatujui yatatatuka lini, hili linasikitisha.

Mwisho Mhe. Spika, hadudi rejea ya mwisho ambayo napenda niizungumzie ni suala la jengo la Mambomsiige. Jengo hili limepigiwa kelele sana. Wenzetu kila walipokuwa wakitupa taarifa hakuonesha kama kulilikuwa na matatizo. Wenzetu walitwambia kwamba kulikuwa na nia njema katika kulikodisha jengo lile, hakuna matatizo, mambo yote yanakwenda vizuri. Pamoja na nia njema iliyokuwepo lakini kulikuwa na matatizo ya kukiuka taratibu za kisheria. Hilo linaonekana matatizo yote yaliyojitokeza ni ukiukwaji wa taratibu za kisheria na kanuni. Unapokiuka taratibu na kanuni maana yake unatia shaka. Kwa nini ukiuke taratibu, kwa nini ukiuke sheria ya manunuzi na mauzaji. Sheria inakutaka unapotaka kuuza au kununua utangaze tenda, kwa nini usitangaze tenda. Hapa ndipo panapotia mashaka, kwani ungetangaza tenda na huyu mtu wako ukamwambia aombe baadaye ukampitisha kutakuwa kuna tatizo gani. Unapofanya mambo haya kimya kimya kwa kumfata mtu, wakati mambo mengine wala hayahitaji utaratibu huo. Hili linatupa mashaka na wananchi wanakuwa na mashaka makubwa.

Mhe. Spika, nakushukurukwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa maoni yangu. Niiyombe sana serikali, niwaombe sana watendaji wetu wa serikali, mambo haya wakati unabadilika, tuachane na yale mazoea kama anavyosema Mhe. Rais Dokta Shein kila wakati *business as usually* tuache, tuache mazoea yale ambayo tumeyazoea ni lazima tubadilike. Turidhike na kile tunachokipata, tusitake utajiri wa haraka haraka hautufikishi pahala. Wananchi wetu ni wanyonge, serikali yetu haina kitu. Kila wakati imekuwa tunatembeza bakuli kuomba lakini kumbe fedha tunazo ndani.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono ripoti hii isipokuwa nikubaliane na wazo la Mhe. Ismail Jussa kuhusiana na suala la Mambomsiige kwamba katika maamuzi yetu tuwe na tahadhari, tusije tukatumbukia katika matatizo mengine makubwa zaidi. Niungane naye kama alivyosema kama kuna matatizo ya ndani yalijitokeza katika taratibu zetu za kuhaulisha au kuuza yabakie yetu ya ndani na hatua zile za kinidhamu zichukuliwe, lakini tusije tukakata mkataba baadaye tukaingia katika matatizo.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua fursa hii kwanza kukushukuru kwa jinsi unavyoendesha kikao hiki na jinsi unavyotoa nafasi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutoa michango yao mbele ya hoja hii, hoja ambayo imewasilishwa na Kamati yetu Teule chini ya Mhe. Mwenyekiti, Omari Ali Shekhe.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati hii ambao tumefanya kazi kwa pamoja kwa muda wote na leo hii ripoti yetu ndiyo inajadiliwa. Kwa hivyo nataka kwanza Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Spika, niseme wazi kwamba sisi kama wajumbe waliotuamini hatukuwahi kufanya kazi hii kwa utashi wala kwa chuki ya mtu yeyote. Ni kupe siri mara nyingi watendaji walikuwa hawawajui CCM na CUF na walikuwa wanaulizana nani CCM na nani CUF. Tuliambizana kwamba tujitahidi kudhibiti utashi wetu wa vyama kwenye suala hili. Tulifanya kazi kwa uwadilifu na tumeandika kile ambacho tumekiona, inawezekana ni kizuri na inawezekana ni kibaya lakini ndicho tulichokiona.

Mhe. Spika, nikienda kwenye hoja ya mwanzo kabisa ya uhaulishaji wa Kiwanja cha Mtoni, kila tunaemuhoji alitwambia wazi kwamba hakuna mazungumzo yaliyofanywa baina ya Kampuni iliyoomba na Wizara ila kuna maagizo kwa njia ya simu na mdomo. Tulipoangalia mikataba wizara walituletea mkataba wake ambao huo ulikuwa na saini na upande mwengine wakatuletea mkataba ambao ulikuwa hauna saini. Nidhahiri kwama mikataba ilikuwa ni miwili baada ya kuonekana kwamba kuna Kamati. Tulipomuita Mkurugenzi wa Kampuni hii ndani ya jengo lako hili alitwambia naomba ninukuu.

> "Mimi sikuwa na haja ya kiwanja lakini ni Mzanzibari, nimeombwa na nikiombwa hukubali maombi. Nilipigiwa simu kwamba kuna mtu anashida na ana kiwanja anauza, sikukiona, niliwatuma watu wangu na nikapeleka watu wangu na ndivyo wakakubaliana kulipana. Sijauona mkataba ila ndio naambiwa leo hapa"

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba mnunuzi wa kiwanja hichi alipigiwa simu na Mhe. Machano Othman Said kwamba ana kiwanja anauza na yeye akawapeleka watu wake ili wafanye *process* husika. Kwa mujibu wa sheria taratibu za uhaulishaji wa kiwanja hiki hazikufanyika. Huu ndio ukweli ambao sisi hatuna haja, hatuna hamu wala hatupendi kumzulia mtu kwa sababu sisi sio lengo letu hilo.

Mhe. Spika, baada ya hapo tukaona kwamba hoja ya serikali kwamba kiwanja kile ni kidogo, lakini tulipoangalia kiwanja cha Mtoni na kile cha Mazizini cha Mtoni kina *square miter 700* na zaidi cha Mazizini kina *square miter 300*, kwa hivyo ni mara mbili ya kiwanja cha Mtoni juu ya kiwanja cha Mazizini. Kamati ikaridhika kwamba hoja ya Wizara kwamba kiwanja kile pale kidogo hakifai hiyo siyo hoja ya msingi.

Mhe. Spika, nataka nikuthibitishie mbele yako na wananchi wote wajue kwamba sisi tumefanya kazi hii kwa uwadilifu na tumeeleza kile ambacho tumekiona. Tafsiri ya sheria ndiyo itakayosema ni tatizo gani, ni kosa au si kosa sisi tumeeleza kile ambacho tumekiona kwamba taratibu za kisheria za uhaulishwaji hazikutumika.

Mhe. Spika, sisi kama wajumbe tumesikitishwa sana kwamba tumeambiwa kwamba kuna agizo la Rais, bahati mbaya hatukuiyona barua ya Rais ila tumeiyona Barua ya Katibu wa Rais. Kama kamati tumejiridhisha kwamba ile ilikuwa ni njama baina ya wahaulishaji na Katibu Harub kwa ajili ya kukitoa kiwanja hichi.

Mhe. Spika, jengine ni suala la Uwanja wa Ndege, suala la jenereta. Baada ya kukaa na pande mbili zote, baina ya Miundombinu na Wizara ya Fedha tuligundua kwamba walikuwa wanavutia *tendor* ile. Kila mtu alikuwa anataka apewe kazi ya kufanya manunuzi kwa hiyo hapa ndiyo yakaanza matatizo, kwamba Wazara ya Fedha wanataka waachiwe wao kwa mujibu wa sheria na Miundombinu wanasema tuachiwe sisi, hatimaye jenereta likaletwa likatelekezwa kwa sababu ya ukosefu wa milioni sabini za kufanya *installation* muda wa *guarantee* ulikuwa ni mwaka mmoja jamaa aliyetoa jenereta lile aliwaarifu wahusika kwamba muda unapotea na jenereta litaangamia, hakuna hatua aliyechukuliwa.

Mhe. Spika, mapendekezo ya Kamati naunga mkono kwamba lifanyiwe ufungaji, liangaliwe bado lipo zima au bovu, kama ni zima kazi imekwisha kama ni bovu waliohusika na uzembe huu warejeshe fedha ambazo ni milioni 300 za Tanzania.

Suala la fidia vile vile tumeliona kweli wananchi tuliwaita wote na majibu ya watendaji yalikuwa si sahihi, wananchi walikuwa hawajapewa fidia yao hadi tunaondoka kwenye Kamati na watendaji kweli waliidanganya kamati.

Mhe. Spika, jengine mikataba ya Uwanja wa Ndege. Mikataba yote ambayo tuliichunguza yote ina dosari za kisheria na wengine walikuwa hawana mikataba. Lipo duka la *IZMIR Pharmacy* Muuzaji alitukimbia kwa muda

wa masaa mawili. Alikimbia kwa sababu alikuwa hana mkataba. Tulimpitia mtu mmoja mmoja tukataka atupe mkataba huyu jamaa alikimbia tukabakia mlangoni zaidi ya masaa mawili hatukumuona. Mwisho tukaridhika kwamba maduka yote yaliyokuwepo pale mengi yao mikataba yao ni feki na mengine yalikuwa hayana mkataba. Tukapata ushahidi kwamba fedha za maduka yale mengine zinaingia mikononi mwa watu binafsi. Baada ya kuchunguza tukagundua kumbe Mkurugenzi mwenyewe wa Mamlaka ambaye alikodi kwa dola 200 yeye mwenyewe alikuwa anadaiwa fedha ya kodi ya miaka mitatu. Ingawa yeye alikuwa anakodisha hanga hilo kwa US$ 1000, lakini alishindwa kulipa kodi na alishindwa kusimamia wapangaji wake ambao wapo chini ya mamlaka yake.

Mhe. Spika, mapendekezo ya Kamati naunga mkono kwamba ni vyema achague moja achague kubakia Mkurugenzi wa Mamlaka au achague kufanya biashara ya hanga ambayo amekodishwa na serikali.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo tumeliona ni uharibifu wa mazingira. Tumefanya ziara hoteli ya Pemba Misali, Maruhubi na *Ocean View*. Nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mmiliki Mkuu wa hoteli ya Pemba Misali, alitwambia nataka niwape kazi kwa ufupi msihangaike wazee wangu. Akatwambia sikutumia sheria, sikupita ardhi, sikupita mazingira, nimetumia ubabe CD ipo, *Hansard* ipo itaonekana tulimrikodi. Tukamuuliza ubabe huu uliupata wapi? Akatwambia nina mtu amenibeba.

Tukamwambia wewe Mkuu wa Mkoa anazuia, Makamo wa Kwanza anazuia nani aliyekubeba. Akatwambia nimetoa asilimia 10 ya *share holder* kwa Mhe. Machano ili anibebe, CD ipo akitaka mtu akasikilize. Tukamwambia tunakushukuru, kumbe asilimia 10 ndio umebebwa tunakushukuru. Huo ndio ukweli ulivyo kwamba hakupita taratibu zozote kwamba kuna mtu anambeba. Akaondoka.

Pia akatwambia mimi mle nina watu watatu ambao wananisaidia kazi zangu. Hivyo hivyo Ocean View, hivyo hivyo Mtoni, na wate aliwataja CD ipo ikifunguliwa itasikilikana. Mhe. Spika, ubabe huu wa muwekezaji huyu ambaye mimi namshukuru sana kwamba alitupunguzia kazi kwamba alibebwa, alikiri na akatoa asilimia kumi kama zawadi wa kubebwa.

Mhe. Spika, suala la *Living Stone* limezungumzwa na mapendekezo ya Kamati bila shaka yalizingatiwa. Suala jengine ambalo nataka niliseme ni ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba. Tulimwita mkandarasi, baada ya kuona taratibu zimevunjwa tukamuuliza, kwa nini wewe ukapewa kazi hii. CD ipo akasema hata mimi nashangaa kwa nini nimepewa.

Mimi si fundi mimi plamba ni fundi mifereji, kwa nini nikapewa muulize Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa nini nikapewa. Kwa hivyo sisi tukapata urahisi. Yeye mwenyewe hajui kwa nini akapewa. Akasema au nendeni Wizara ya Fedha mtauliza kwa nini nikapewa miye akaachwa Mazurui, akaachwa Rans kwa nini nikapewa miye wakachwa wengine. Si majibu yangu muulize Waziri wa Fedha na Watendaji wake.

Mhe. Spika, baada ya kuchunguza tumegundua kwamba huyu ili uwe mkandarasi ni lazima ujisajili kwenye bodi ya wakandarasi, hajulikani huyu kwamba ni mjumbe wa bodi ya wakandarasi. Hana ofisi, vifaa pia aliazimwa na serikali baadhi ya vifaa. Lakini ndio plamba, kazi yake aazimwe vifaa.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kutoa tahadhari serikali ina mawazo kwamba huyu mtu wampeleke kwenye usuluhishi *arbitration*. Taratibu wa *arbitration* ni lazima mkandarasi awe amejisajili kwenye bodi ya wakandarasi. Huyu hayumo kwa hivyo mkimpeleka huko mtashindwa. *Solution* ama arejeshe pesa au mumsamehe. Bodi ya wakandarasi haiwezi kumuhukumu mtu ambaye sio mwanachama wa bodi ya wakandarasi, huyu hayumo ni plamba. Serikali isijeikafikiria kupoteza za umma wakafikiria twenda kule, sisi wawakilishi hatukubali kwa sababu amesema mimi si *engineer* tumekwenda Wizara ya Maji ma- *engineer* wametuthibitishia kwamba huyu hatumtambui wala si *member* wa bodi wa wakandarasi ya wajenzi Tanzania.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuiyomba sana serikali isiende kwenye *arbitration* jamaa anatashinda kwa sababu hajulikani yeye mwenyewe anasema ameshangaa kwa nini akaaminiwa wakati yeye si fundi.

Mhe. Spika, suala zima la Mambomsige, mimi nimefahamu sana *concern* ya Mhe. Salmini Awadh na Mhe. Ismail Jussa, lakini najiuliza sisi pale hatuoni mkataba. Jamaa yule kapewa *lease* kama ambavyo anapewa *lease* mtu mwengine, lakini kisheria itaangaliwa kama ile *concern* ya Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Salmini Awadh sisi kama Kamati tupo tayari iangaliwe, lakini tunaona hakuna makataba kuna *lease*.

Lakini taratibu za kisheria zimekiukwa. Bahati nzuri Waziri wa Nchi Afisi ya Rais tulimwita juu humu ndani ya Afisi yako. Tukamuuliza mlifanyaje, akatwambia mimi nimepewa agizo na Mhe. Rais kwamba nikodishe.

Tukaambiwa kwamba umepewa agizo na Mhe. Rais akasema ndiyo. Tukamuuliza je, unayo barua akasema ninayo barua tena ya wino mwekundu. Akasema wewe ukipewa barua ya wino mwekundu utekelezi. Tukamwambia tutatekeleza kwa wino mwekundu kwa sababu ni tishio.

Kamati imamuomba basi kama unayo barua ya wino mwekundu basi tuletee tuiyone. Siku ya pili akatwambia sina barua naomba samahani, *CD* ipo ukitaka tutakuonesha.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba Mjumbe aeleze maneno sahihi niliyomwambia asipotoshe analipotosha Baraza kwa kusema naomba airekebishe kauli yake. Maneno sahihi niliyomwambia yapo ndani ya ripoti, naomba asome nilichomwambia, asipotoshe Baraza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi sina nia ya kupotosha na katika kiapo nilichokula sijawahi kukusudia kupotosha, ni kwamba alitwambia mbele ya kikao kwenye ukumbi wa *briefing* kwamba ana barua ya *red ink*. Mhe. Spika, siku ya pili akatwambia kwamba sina barua labda mumfate Mhe. Rais, sisi tukaona hatuna haja ya kumfuata Mhe. Rais. Kwa hivyo, mimi sikusudii kupotosha, sipotoshi na wala sitojaribu kupotosha namuheshimu sana. Tulipoipata hiyo barua ya *red ink* na Mhe. Spika, ofisini mwako imo hiyo barua kwa Katibu kwamba wambie wajumbe wende kwa Rais. Mhe. Spika, sisi Rais hatuna haja nae wewe ndiye uliyetoa agizo la kukodisha. Mhe. Spika, mimi sina nia ya kupotosha wala simzulii katika hilo.

Mhe. Spika, jengine kwa vile barua ya Rais aliikosa kamati ikaridhika kwamba yeye ndiye muamuzi kwa sababu yeye ndiye aliyemuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwamba akodishe. Kwa hivyo, sisi tulikuwa hatuna haja ya kwenda kwa Mhe. Rais kwa sababu barua yake ndio tuliyoiona. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hakukuwa na *red ink* wala hakukuwa na agizo la Rais kwa msingi huo, na kamati ikaridhika kwamba yeye ndiye aliyetoa maamuzi.

Mhe. Spika, suala la *generator* 12 ambalo tulitoa hoja kwamba kamati imejitahidi, imehangaika, imeyaona ma-*generator* 11 ambayo nusu na robo ni mabovu. Moja hadi hii leo hatukuliona na Mamlaka ya Maji watatwambia liko wapi tumehangaika Mhe. Spika, hatukulipata. Kwa hivyo, mimi ninachosema kwamba najiuliza suala la ajira kwa nini ikafanywa hivi.

Mhe. Spika, Pemba tumewaita vijana 37 wote tumeambiwa kwamba kuna ajira za vijana 37 ambao wana sifa, mmoja tukamwita nikamuuliza wewe una elimu gani akaniambia mimi nimemaliza kidato cha nne. Nikamwambia andika maneno yafuatayo kwenye karatasi, nikamwambia andika mimi Othman Ali Othman naomba kazi Miundombinu. Mhe. Spika, basi masaa mawili ilimshinda mpaka akalia.

Mhe. Spika, ni *form IV* gani na wa nchi gani asiyeweza kuandika maneno hayo, *wallah* nakula kiapo na mimi ni Muislamu kwamba mimi Othman Ali Othman naomba kazi ya Miundombinu andika maneno hayo mbele ya Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini basi alishindwa. Nambieni Wazanzibari wenzangu ni form IV gani aliyekuwa hana uwezo wa kuandika Kiswahili hicho. Mhe. Spika, mwisho yeye mwenyewe alitwambia kwamba barua hii nimeandikiwa na cheti nimepewa na wakubwa kutoka *VETA*. Kwa hivyo, ajira zote za Pemba watu waliitana wakagawana, wamo waliokuwa wanamuhusu Waziri, wamo waliokuwa wanamuhusu Afisa Mdhamini, wamo waliokuwa wanamuhusu *Engineer*, wamo waliokuwa wanamuhusu Katibu Mkuu, huo sio utawala bora. Mhe. Spika, suala la mtoto wa Katibu Mkuu tumegundua kweli ameajiriwa akiwa na diploma, lakini alikuwa akipewa mshahara wa digrii tena akatwambia kwamba mimi mshahara wangu sijauona maana ninatiliwa benki moja kwa moja. Mhe. Spika, anachukua mshahara hajauona kwa jicho anaambiwa mshahara wako uko benki.

Mhe. Spika, vile vile tumegundua kwamba kuna muajiriwa ameajiriwa mara mbili, anapokea 192,000 Bandari na anapokea 105,000 Ofisi Kuu ya Miundombinu. Kwa hivyo, kama kuna nyongeza ambayo ameongenzwa Bandari na Miundombinu maana yake ana zaidi ya mishahara miwili. Hayo tumeyaona mbele ya Makatibu Wakuu na tumeyaona mbele ya Wakurungenzi. Mhe. Spika, baya zaidi ambalo tumeliona ni kwamba wafanyakazi wako chini ya kipindi cha maangalizi, wamepatiwa nafasi ya kwenda nje kusoma, hivi sasa mtoto wa Naibu Katibu Mkuu Miundombinu yuko nje. Mhe. Spika, kipindi cha majaribio mtu anaangaliwa kwamba kweli kazi ataiweza tayari yeye amepatiwa nafasi ya kwenda nje hajafanyakazi hata kidogo unampa nafasi ya kwenda nje.

Mhe. Spika, hii nchi ni yetu shirika Wazanzibari wanategemea kwa hiyo tumeridhika kabisa kwamba ajira za Miundombinu zilikua ni ajira za kugawana, na kama leo wataitwa hapa ukiwapiga mstari basi kila mtu

atakwenda kwa mzee wake ndani ya Miundombinu. Humo hamna mtoto wa mkwezi na mkulima wa Unguja na Pemba, hebu waiteni muwapige mstari basi mwenyewe atakwambia mimi wangu huyu na huyu.

Mhe. Spika, nimeangalia ilani za uchaguzi nimejiuliza ni ilani gani iliyotumiwa, CUF haimo na CCM sijaiona. Kwa hivyo, wenzetu wanatumia ilani ipi kutoa huduma kwa Wazanzibari, leo nawaambia hawatusemeshi humu. Mhe. Spika, maana yake sisi tunamjua Mhe. Waziri wa Utumishi Mhe. Haji Omar Kheir kwa nini hatukumtaja, tunampenda. Ni kwa sababu hajahusika kila ambaye tumemtaja ndiye ambaye amehusika. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi kama wajumbe ukiamini usiamini tumefanya kazi yetu kwa uadilifu hatuna shuku na mtu yeyote. Kwa hivyo, sisi tumetumwa na kazi yetu ambayo tumetumwa tumeifanya maamuzi ni ya serikali na maamuzi ni ya Wazanzibari. Mhe. Spika, lakini kwa hakika huu ni mfano wa serikali kama hivi ndivyo ilivyo serikali ndani ya wizara moja katika ajira, je wizara 16 itakuwa vipi?

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kinga, fursa na haki za wajumbe mtu ana haki ya kutoa taarifa bila ya kubughudhiwa kwa bahati mbaya kuna watu wanaadhibiwa kwa sababu ya kupita Kamati Teule. Hili naomba liachwe na wala watendaji wasifikirie kwamba sisi tumepewa taarifa na wao, sisi Wazanzibari hatujapewa taarifa na Mkurugenzi yoyote, tumepewa taarifa na Wazanzibari wanyonge wanaoumia. Kwa hivyo, watendaji Mawaziri na Makatibu Wakuu nawaomba sana musisikilize maneno mukawahukumu watu kwa kuwaonea, sisi tumepewa taarifa ndani ya mikono yenu wakubwa. Baada ya kugawana nafasi wengine mkaponya ndio wamesema. Mhe. Spika, watu wamegawana nafasi wengine hawakupata ndio wametwambia sisi jamani tumeoneana.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema ni vyema serikali kwa busara chini ya Mhe. Waziri wa Utumishi naomba utaratibu utumike hatukusudii mtu kumdhalilisha, lakini nidhamu ya nchi iwepo na kila mtu apate haki yake na huo ndio msingi mzuri. Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi ikiwa kila siku itaundwa Kamati Teule kwa makosa ya watu, nchi hii itabidi iwekwe fungu maalumu kwa Kamati Teule, kwa sababu wanafanya kusudi.

Mhe. Spika, juzi imeundiwa ya umeme, jana ukaunda Manispaa, kesho kutwa ya barabara kwa sababu ya uzembe wa makusudi. Kwa hivyo, na sisi kwa mujibu wa kanuni hutuzuii ni haki yetu kuunda Kamati Teule, hivyo serikali iseme na watu wake wasiharibu. Mhe. Spika, dawa peke yake ni kwamba wasiharibu, wakiharibu sisi ndio haja yetu nimemwambia Mhe. Juma Duni mimi naomba Mungu uharibu nikuseme, hiyo ndio kazi yangu mimi. Kwa hivyo, msitubane kwa Kamati Teule cha msingi Waziri wa Nchi nikuombe uwadhibiti watendaji wako wasiharibu hiyo ndio dawa ya kuunda Kamati Teule.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa heshima kubwa sana nawapongeza wenzangu Wajumbe wa Kamati Teule, lakini kama kuna pongezi kubwa ya kupewa nikupe wewe Mhe. Spika kwa sababu sisi ni Wazanzibari ilikua tunapewa taarifa kwamba kuna watu walikuwa wanakusakama, kwa nini ukaunda wale. Mhe. Spika, wanasema umemteua Mhe. Hija kwa sababu ndiye aliyetoa hoja, kama ambayo umemteua Mhe. Asha Bakari kwa sababu ndiye aliyetoa hoja, hivyo ndivyo inavyosema kanuni. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakupongeza naendelea kujenga heshima ya Baraza hili jana nimekwenda Ubalozi wa Oman na salamu nitakupa baadae tumeambiwa kwamba katika Baraza zuri kwa Afrika Mashariki ni Zanzibar kwa demokrasia, kwa uwazi na kwa umakini wa Spika.

Mhe. Spika, nimemwambia Katibu wako wa Baraza kwamba nimeambiwa nije nipeleke ujumbe kwamba kuna mwaliko na barua itakuja ya kwenda Oman wewe binafsi kwa umakini wa Baraza lako. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, naunga mkono kamati yangu na naomba serikali ifikirie na inisaidie kuokoa nchi hii kwa maslahi ya Wazanzibari wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Asha Bakari Makame nina vitabu hapa hivi ni *volume* mbili tu za vielelezo, kuna na mbili nyengine naziweka kwenye meza ya Makatibu kama kuna Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu kutoa hizi kwa kila mjumbe ingekua kazi kubwa sana. Kwa hivyo, itakua ziko mezani kama kuna Mhe. Mjumbe atapenda kufanya rejea humu basi zipo hapa katika meza ya Makatibu.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Spika, *Bismillahi Rahmani Rahiim*, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kuchangia katika Kamati Teule ambayo miongoni mwa wajumbe na mimi nikiwemo. Lakini pia niwashukuru wale wote ambao kwa kweli wamechangia kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, kabla sijachangia nitakuomba uniruhusu kuna gazeti hapa limeandikwa Ikulu Zanzibar kuna sehemu ndogo tu nataka niisome, maneno hayo ameyasema Mhe. Rais sio mimi kama “Zanzibar kubadilika inawezekana” Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraa la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein mara kadhaa amekua akisisitiza umuhimu wa Wazanzibari na hasa watendaji serikalini kubadilika, akimaanisha kuachana na

utendaji wa kimazoea. Kwa falsafa ya Rais wa Zanzibar hatua hiyo ni miongoni mwa hatua muhimu na za lazima zinazopaswa kuchukuliwa katika kuleta maendeleo endelevu kwa haraka ili kufikia hatua hiyo, Dk. Shein anasisitiza mambo yafuatayo. Mhe. Spika, mambo hayo sitoyasema kwa sababu ni mengi sana, lakini nitasema moja tu tushirikiane kupatana kutokana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma kwa lengo la kujenga taifa lenye kufuata utawala bora, usawa na haki za binadamu. Mhe. Spika, muna dondoo nyingi lakini nilisema niseme hizi tu, hili gazeti tulipewa hapa kwa hivyo mtu anaweza akalitafuta akasoma zile dondoo.

Mhe. Spika, kwanza nizungumze suala zima kwamba Kamati Teule ni binadamu, na binadamu hakuna mkamilifu siku nyengine katika kutembea kwetu kuangalia baadhi ya mambo haya, siku nyengine mambo mengine tumekosea. Lakini lengo la Kamati Teule nikutaka kuhakikisha Serikali ya awamu ya saba yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa inawapa matumaini wananchi wake. Mhe. Spika, kwa makusudi Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kila hotuba yake, kila akifanya ziara suala hili mheshimiwa analizungumza Rais.

Mhe. Spika, kitabu hiki na hivyo vyengine ulivyoviweka hapo ni vielelezo tosha kwamba tubadilike. Kubwa utungaji wa sheria tunazitunga sisi ni watu wa fasaha wa kutunga sheria, lakini matokeo yake hatuzitekelezi sheria ni miongoni mwetu sisi ndio tunaovunja sheria. Kwa hivyo, naiomba sana serikali kwa sababu mimi wenzangu wameshadondoa kila kitu kimoja kimoja, mimi naiomba sana serikali Mawaziri, Makatibu Wakuu, watendaji wote wa kila wizara hatutomstahamilia mtu yeyote tunataka tubadilike tumechoka. Mhe. Spika, dhamira kubwa ni kwamba tubadilike ili tuwape matumaini wananchi wetu.

Mhe. Spika, kazi hii imefanywa kwenye mazingira magumu, mengine ni aibu kusema watendaji wetu walipata tabu sana hao ndio maana ukaona imechelewa, walikuwa saa nyengine hawaoni kitu, wanaumwa, wanaanguka kitandani. Mhe. Spika, ndio nikasema mambo mengine ni aibu kusema. Kwa hivyo, lengo na madhumuni nikutaka kuhakikisha tunatenda haki kwa kila raia wa nchi hii.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha kubwa ni kwamba matendo haya mengine yamefanyikana wakati wa pirika za uchaguzi. Kwa sababu kila mmoja yumo katika harakati za uchaguzi, watu wamefanya mambo yao kwa kujijua, kwa sababu kuna kipindi mawaziri wanaambiwa warejeshewe gari. Lakini kuna watu wanakwenda ofisini kwa kufanya mambo yao binafsi, hilo ndio lakusikitisha hivyo natoa indhari ee! Mhe. Rais Dk. Shein nakuonea huruma, lakini Mwenyezi Mungu atakusaidia na atatusaidia na sisi. Mhe. Spika, naomba sana neno Ikulu nakuomba Mhe. Rais uwe makini, Ikulu sio pahala pa biashara, ndio pakaitwa Ikulu.

Mhe. Spika, jengine naiomba sana serikali iwe makini kwa sababu sisi hatukumuonea mtu ni Baraza lako tukufu limetutuma, kwa hivyo tumekwenda kwa mujibu wa taratibu na sheria kwa hadudi rejea ulizotupa wewe mwenyezi Mhe. Spika. Mhe. Spika, maana ilifika hadi watu wakawa wananuna hawatusemeshi, jamani haya ni mambo ya kupita tu ya dunia haya. Kwa hivyo, niseme tu kwamba usile na kipofu mpaka akakukamata mikono, ule kipofu asijue. Mhe. Spika, fedha za serikali za nchi hii wanajinufaisha watu wachache kwa maslahi yao sio kwa maslahi ya nchi.

Mhe. Spika, sasa hivi hatutokua tayari pesa za umma za wavuja jasho ambao wao ndio wanachangia serikali yao tukawadhulumu. Mhe. Spika, mimi amenimaliza Mhe. Salmin Awadh Salmin ameonesha ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio chama tawala, amesoma katiba na nilisema juzi kwamba Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa hao CUF wanatimiza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, mimi kama mwanachama wa Chama cha Mapinduzi sitokuwa tayari serikali yangu inayoongoza na iko madarakani kumuacha mtu kwa sababu ni wa Chama cha Mapinduzi au ni wa CUF kwa maslahi yake mwenyewe. Siasa tumeshacheza zamani sasa lililobakia ni kujenga nchi, na nchi hii haitajengwa isipokuwa na sisi wenyewe wananchi wa nchi hii. Kwa hivyo, naiomba sana serikali tena naiomba sana kwamba tubadilike, namuomba sana Mhe. Rais na naomba Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba ripoti hii yote apelekewe Dk. Shein na vielelezo vyake vyote Dk. Shein apelekewe ili aone mambo ambayo yalifanyika. Sasa kazi kwako kwa sababu sisi baadhi ya mambo hatuna madaraka nayo, lakini kuna mambo ambayo ya dondoo ndogo ndogo itabidi tuulize katika kikao chako hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa sababu wenzangu wamezungumza mengi wao wamechukua yale madondoo ambayo yamo katika kitabu hiki. Lakini mimi nilisema nizungumze hayo ili serikali sasa iamke isilale usingizi na sisi kwa sababu tunaisimamia serikali tutaisimamia serikali ipasavyo, hatutoacha chochote ng'oo mradi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria ya nchi hii. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niseme la mwisho kwamba hatukuwa na dhamira mbaya mmetutuma, na mtu akitumwa hutekeleza wajibu wake na vielelezo vimo, *hansard* ipo. Mhe. Spika, basi hiyo *hansard* ndio yenye visa, *hansard* ndio yenye mambo yote kwa hiyo namuomba sana Rais pamoja na Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Makamo wa Pili wa Rais wawape matumaini wananchi wa Zanzibar katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii mia kwa mia na pale pakuchukuliwa hatua pachukuliwe tuondokane na muhali na udugu na ushoga na urafiki na ushemeji. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo niweze kuchangia katika ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza lako la Wawakilishi. Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukakutana jioni hii ya leo tukiwa wazima na afya njema kabisa. Vile vile nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa kamati, pamoja na wajumbe wenzangu wote. Mwenyekiti wetu amejitahidi kutusimamia wajumbe wake tukaweza kufanya kazi moja nzuri kabisa, hii ambayo tumeiwasilisha hapa mbele yenu leo.

Mhe. Spika, mchangao wangu hautokuwa mrefu sana, nitachangia maeneo mawili matatu hivi, nitaanza na hili la kiwanja cha iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Mhe. Spika, kwa kweli tukiangalia pale kiwanja kile ni mali ya serikali, kiwanja kile cha iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ambapo hapo zamani walikuwa wakiweka zana nzito watu wa *UUB* zile gari zao kubwa za *bulldozer*.

Ukiangalia utaratibu mzima ambao ulitumika pale, ni dhahiri unaonekana una harufu ya rushwa. Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ule utaratibu wenyewe wa kukihaulisha kile kiwanja kutoka katika milki ya serikali kwenda kwenye milki ya kampuni au mtu binafsi, haukufuata kabisa zile taratibu zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria, kilichofanyika pale Mhe. Spika, kama ambavyo kimeelezwa kwenye ripoti hii, ni utashi tu wa mkubwa mmoja hivi, mimi nauita utashi. Kwa sababu ukiangalia katika hii ripoti yule mtendaji mkuu wa wizara ile ambaye ni Katibu Mkuu, ambaye angepaswa kusaini mikataba ile hakuhusishwa katika uhaulishwaji wa kiwanja kile. Kwa sababu angekuwa amehusishwa tungeona saini zake.

Lakini ukiangalia zaidi ukienda ndani kwenye hadidu rejea hii, utakuta namna ya mikanganyiko ya hata ile mikataba yenyewe inaonekana kama iko miwili, mmoja ulitengenezwa awali ukasainiwa na aliyekuwa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ikisha na wa pili vile vile ukasainiwa na huyo huyo, ukiitizama unakuta kama kuna mikataba miwili, na tulipojaribu kufanya mahojiano nao wale wenzetu wa upande wa pili kutoka kwa Bakhresa kule, wao wenyewe walikiri kwamba ile mikataba wanaiona ni miwili, lakini na wao ndivyo walivyopewa. Sasa sijui kilichochanganyikiwa kitu gani tukafika mahala kukawa na utata kiasi hicho.

Mhe. Spika, lakini lile zoezi zima la uhaulishaji wenyewe basi lilikuwa linakwenda *speed* kuliko maji yaliyoachiwa kwenye mlima, maana yake hapo kwa hapo. Tulipomwita bwana mkubwa yule kuja kumuhoji namna alivyokipata kiwanja kile, labda kuna maombi au kitu gani, cha kushangaza Mhe. Spika, hakuna hata ombi anasema mimi sikuwahi kuomba hichi kiwanja, mimi sikuomba nimekuja kuitwa hapa kwamba kuna kiwanja kama unakitaka hichi hapa kinauzwa.

Huo ndio utaratibu uliotumika Mhe. Spika, tuone ni namna gani baadhi ya viongozi wetu hawa wanavyotumia madaraka yao vibaya, wanapewa nafasi hizi lakini kwa utashi tu mtu anaamua kufanya anavyotaka yeye, badala ya taratibu za kisheria zilizowekwa, ndio maana nikasema hapa pana harufu ya rushwa. Kwa sababu kama mtu atafuata taratibu, hakuna tatizo atahaulishiwa tu huyo mtu, lakini taratibu zifuatwe.

Mhe. Spika, hata nilipokuwa nimeleta hoja hii hapa Barazani, kwa sababu mimi ndiye niliyeileta hapa wakati wa Bajeti, nilisema mimi tatizo langu sio kuhaulishwa, tatizo langu ni utaratibu sheria hazikufuatwa, hiyo ndiyo iliyokuwa hoja yangu na kweli tulikwenda kuthibitisha hiyo hoja kwamba hilo jambo kweli halikufanyika. Kwa hivyo, ndio maana nasema kwamba huu ulikuwa ni utashi tu wa mtu na watu wake wawili waliokubaliana na hilo, lakini ni ukiukwaji mkubwa wa sheria ambazo Baraza lako hili tukufu ndio hukaa kazi yake kuzitunga na kuwataka hao watekelezaji kule wazitekeleze.

Mhe. Spika, mimi niendelee tena kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuhusu ajira. Kwa kweli Mhe. Spika, kama watangulizi waliochangia katika hadidu rejea hii, wengi wamekubaliana kwamba kuna upendeleo wa dhahiri katika suala zima la uajiri kwenye miundombinu. Lakini vile vile kuna ukiukwaji wa taratibu za kisheria katika suala la uajiri katika Wizara hii ya Miundombinu.

Mhe. Spika, mnadhimu wetu pale alikuwa akichangia, aliuliza swali aliliona kwenye ukurasa wa 103 naomba nisome kidogo muhutasari wa mambo yaliyobainika na kamati kufuatia uchunguzi wake wa hadidu rejea hii.

> “Kiuhalisia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndiyo iliyohusika na uajiri wa wafanyakazi wake kuliko mamlaka husika Idara ya Utumishi serikalini, kutokana na wafanyakazi hao kuajiriwa katika nafasi zilizokuwa hazijaelekezwa na mamlaka husika, na hivyo Wizara ya Miundombinu na

Mawasiliano bila ya utaratibu wowote kwa kuona wao tu inafaa, wameamua kuondosha au kutomuajiri mfanyakazi katika nafasi zilizoelekezwa na kujaza nafasi walizotaka wao bila hata ya kuangalia sifa na uwezo wa wafanyakazi hao".

Mnadhimu alipokuwa akichangia pale Mhe. Salmin Awadh, alitaka kujua kwamba ah! Mbona huku mmesema wamefanya wao peke yao, huku mnasema wameshirikisha Idara ya Utumishi. Hapa ni namna Wizara ya Miundombinu ilivyofanya ile ajira yenyewe, kwa sababu wao Wizara ya Miundombinu ndio walioomba Idara ya Utumishi, wanaomba ajira ya watu kwa namna ya zile nafasi walizonazo, waliomba nafasi nyingi sana lakini Idara ya Utumishi kwa kuangalia na Mfuko wa Serikali ikasema hatuwezi kukupeni zote hizi, lakini tutakupeni nafasi kadhaa katika yale maeneo ambayo wao waliyaomba.

Lakini cha kushangaza na kusikitisha kabisa Mhe. Spika, baada ya wao wizara kuruhusiwa kufanya zile taratibu za kuajiri, maana yake lazima wao ndio wanafanya pale usaili na mambo mengine, wao wakaajiri watu tofauti na zile nafasi walizoomba, ndio maana hapa tukawa tumeeleza kwamba wao walijifanyia hili suala kama wao tu, lakini Idara ya Utumishi imehusika kwa sababu wao ndio waliotoa kibali cha kwamba ajirini, sasa na baada ya kufanya hilo kawaida ni lazima warejeshe kwao utumishi kwamba tumewaajiri hawa na sifa zao hizi.

Sasa ndio maana hapa nataka kumtoa shaka Mhe. Salmin Awadh kwamba, hichi ndicho walichokifanya Wizara ya Miundombinu kwamba hawakuajiri watu wale wenye sifa ambazo wao wenyewe ndizo walizokuwa wameziomba, baada ya kupewa ile nafasi tu wakasema aaa ndio hapa hapa, ndio pale walipokuwa wanaita tena nani yuko wapi njoo, nani yuko wapi njoo, wakaajiri wanavyotaka wenyewe, ndio maana tukasema hili zoezi limekwenda kiubinafsi zaidi, kwa sababu wale waajiriwa wengi wao hawana sifa za zile ambazo wao wenyewe walikuwa wakizitaka. Hii ni kusema mtu anajikaanga mwenyewe kwa mafuta yake, kwa sababu wao ndio waliotoa zile sifa za watu wanaowataka, lakini wao wao ndio waliofanya kosa lile la kuajiri watu ambao hawana hizo sifa walizozitaka.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka niitolee ufafanuzi hii Mhe. Spika, ili mnadhimu wangu asije akaniwekea kitimoto kule kwenye chama chetu, maana yake leo kachafuka kaanza na Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Tume ya Uchaguzi, na mimi kule kwenye chama chetu Mhe. Spika, nataka nikuarifu naitwa Kada wa Chama cha Mapinduzi. Sasa anapokuwa mkubwa wangu wa chama akisema namna hiyo mimi nakuwa natetemeka huku.

Mhe. Spika, nilitaka kueleza hilo tu lakini wenzangu wameshalifafanua sana suala la ajira. Kwa hivyo, mimi nasogea kwenye hadidu rejea nyengine ya jengo la Mambomsiige pamoja na mambo yaliyojitokeza.

Mhe. Spika, tulipokuwa tunafuatilia suala hili, tuligundua matatizo mengi sana, kwenye suala la Mambomsiige Mhe. Hija Hassan Hija alilizungumza vizuri kidogo pale na akasema kwamba hakuna mkataba. Mimi nakubaliana naye kweli hakuna mkataba wa makubaliano yoyote baina ya hiyo kampuni iliyopewa na serikali, isipokuwa hawa wamepewa *lease* ya kumiliki ardhi na *lease* ile wamepewa kwa miaka 99, sijui kama mjukuu wangu atakuwepo, lakini wakati huo huo wakapewa *grace period* msamaha wa kutoilipia wa miaka 10, yaani miaka kumi pale wao wakae tu hakuna kinacholipwa serikalini, miaka 10 na mimi najua utaratibu sijui kama ndio uhakika ni miaka miwili au mitatu kama sikosei kwa wawekezaji hao, lakini huyu kawekewa yake 10 kabisa atulie asiwe na wasi wasi.

Hapa Mhe. Spika, ukipaangalia kwa ghafla tu basi hata hapataki tochi, ile harufu kama iliyokuweko kule kwenye kiwanja cha Wizara ya Miundombinu na hapa ipo ya rushwa kwa mbali naisikia. Lakini ukiangalia namna ya upewaji au utolewaji wa jengo hili haukufuata taratibu, huyu ambaye kapewa kama alivyopewa yule wa mwanzo hana hata barua ya maombi, huyu kwamba angalau naomba hili jengo nataka kufanya nini hakuna, si Wizara ya Fedha wala Wizara ya Maji na Nishati waliotupatia barua hizi, hata tulipomwita huyo mwenyewe kumuhoji alisema yeye hakuandika barua aliitwa tu kuja kukabidhiwa mali na mazungumzo yalifanyika Wizara ya Fedha, yalisimamiwa na mawaziri mawili, aliyekuwa Waziri wa Fedha wakati huo, yaani Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akisimamia mambo ya fedha nafikiri, na aliyekuwa Waziri wa Maji, Nishati na Ardhi wakati huo sijui ilikuwa inaitwa hivyo au vipi, ndivyo yalivyofanyika.

Mhe. Spika, ndio maana hata katika kuangalia namna lilivyotokea, tulianzia tukakuta kuna barua tu ambayo ilikuwa inatoka kwa Mhe. Waziri wa Fedha inampelekea Katibu Mkuu wa Fedha kutaka kuwakabidhi jengo hili hawa. Sasa ukiangalia ule utaratibu mzima pale basi hawa watu walikaa tu wakamwita na kufikiria wampe tu hawana hata barua ya maombi, wakasema sisi labda ile zamani tulipokwenda kufungua Hoteli ya *Kempiski*, tulizungumza kama itawezekana tupewe ile nyumba ya Mambomsiige na eneo lile tuweze kufanya hoteli ya kisasa zaidi kule, wakati wa kufungua ile sherehe huwa kuna ile risala pale, wakasema tulipokuwa tunasoma risala yetu ndio tuliitumbukiza pale.

Sasa akasema nadhani ile ndio wameitafakari wakaona ni vyema kutuita, sasa ndio pale tunaposema Mhe. Spika, utaratibu mzima wa utoaji wa eneo lile haukufuata taratibu, nafikiri mapendekezo ya kamati ukiyasoma vizuri mle, utaona namna ambavyo imeelezwa vizuri. Sisi katika kamati tulisema kupewa mtu kitu sio tatizo, lakini tunachokisimamia ni zile taratibu ambazo sisi wenyewe tunakuwa tumejiwekea.

Mhe. Spika, Baraza lako hili linatumia fedha nyingi sana za walipa kodi katika kutunga sheria, sasa kama tunatunga sheria hapa zinakwenda kule wasimamiaji au wale ambao wanatakiwa wazifuate wale tunaowapa maagizo kule, hazifuatwi na wanaofanya hivyo ni watendaji wa serikali, ambao wao ndio wangepaswa kuzisimamia. Kwa kweli hatuwatendei haki wananchi wetu, tutakuwa hapa tunakuja tunatunga sheria, tunakula hizi pesa za wananchi walipa kodi, lakini yale maudhui ya hivi vikao vyenyewe yanaonekana hayafuatwi.

Sasa Mhe. Spika, ndio maana tukasema katika ufafanuzi wetu hapa juu ya suala zima la jengo la Mambomsiige, jengo hili lirudishwe serikalini mara moja. Kwa sababu wenyewe wananchi kwanza hawataki jengo hili litoke kwenye mikono yao, na kama utakumbuka Mhe. Spika, lilipokuja jambo hili likajulikana kwamba limetolewa kulikuwa kuna kelele kweli huko mitaani, kuna watu walitishia mpaka kwenda mahakamani kwa suala hili.

Lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Spika, namna ya wale wafanyakazi au zile taasisi za serikali zilizokuwemo katika jengo lile zilivyofukuzwa, mimi nasema kufukuzwa, maana kuondoshwa utapewa *notice* mambo yanakwenda kidogo kidogo, lakini wao tarehe kama 22 imeandikwa barua unaambiwa mpaka tarehe 25 uwe umeshahama, sasa siku tatu taasisi kama zile unazihamishaje, lakini unawaambia wahame hapo hujawatayarishia mahala pa kwenda, huku na huku wakapelekwa *PBZ* pale, nenda Mhe. Spika, ukapatizame, huwezi kujua nani mfanyakazi nani aliyekuja kuchukua huduma, maana wanachanganyika tu pale wote, ukiingia tu *typist* kacha kacha akikosea mkono kakugonga, jinsi watu walivyobanana.

Mimi nimeshakwenda pale siku za mvua, nilivyozikuta *document* zinavyoroa kwa mvua Mhe. Spika, nilitaka kulia, maana ninaangalia kumbukunu zetu namna zinavyoondoka kwa utashi tu wa mtu kuwaondosha katika eneo ambalo zilikuwa zimehifadhika *document* zile. Kwa kweli Mhe. Spika, pale mahala wanapokaa wafanyakazi wale hapastahiki, pamebanana kesho na keshokutwa tusishangae baada ya muda mchache wafanyakazi wale tukawakuta wote kama hawana kifua kikuu basi pumu jinsi wanavyovuta pumzi mbaya za zile karatasi zilizokaa siku nyingi. Kwa kweli Mhe. Spika, hili jambo linasikitisha sana kabisa.

Mhe. Spika, lakini pia tuangalie hata zile tarehe zenyewe za uhaulishwaji wa jengo hili. Mhe. Spika, kama unavyokumbuka mwezi wa Oktoba, 2010 wakati wa uchaguzi, jengo lile ile speed iliyokwenda kutoka huko kuanza harakati mpaka kumaliza, mpaka kuondoshwa, na wafanyakazi wale kuhama ni ndani ya kipindi cha siku kama kumi na saba tu, sasa unajiuliza kwa nini kuwe kuna uharaka kiasi hichi?

Mhe. Spika, hapa tuna uchaguzi kitu kikubwa sana hichi kwa taifa letu, mimi nafikiria pale serikali inatakiwa kukaa kwa makini kuangalia namna ya uchaguzi ule utakavyokwenda, kuusimamia na mambo mengine tunakwenda kukimbilia kuhaulisha jengo na kuwahamisha wafanyakazi kabla ya tarehe ya uchaguzi, ili ukimaliza uchaguzi kiongozi anayekuja au Rais anayekuja akute yale mambo yamemaliza jana yake, mimi ndio tafsiri yangu sijui wenzangu wanaionaje, lakini kwa kweli muda uliofanyika lile zoezi ukiitizama Mhe. Spika, hapataki tochi ile harufu mmh ipo. Hiyo ndiyo iliyopelekea kufanya hivyo, kwani ungesubiriwa uchaguzi ukamaliza hiyo inayokuja si serikali nayo vile vile, kwa nini isije ikafanya ile serikali itakayokuja.

Mhe. Spika: Muda Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika nakusikia, nasikitika sana kwa kitendo hichi kilichofanywa. Mimi na wananchi wangu wa Mkwajuni katika jambo hili tunakubaliana na mawazo ya kamati, jengo hili lirejeshwe serikalini libakie mali ya wananchi. Mwekezaji huyu kama anataka atafutiwe eneo jengine huko yako maeneo kwendea Nungwi, kuna uwanda mkubwa sana kama kwa kutaka kujenga hoteli ya Kimataifa anapata atafutiwe huko apewe.

Mhe. Spika, kwa kunihimiza kwako ili na mwenzangu naye awahi hapa, basi mimi naiunga mkono hoja ya kamati kwa asilimia mia moja sina tatizo nayo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mbarouk Wadi umekula chakula chote, sasa unamwambia mwenzako awahi. Waheshimiwa Wajumbe nashukuru kwa michango juu ya shughuli hii iliyoko mbele yetu, nadhani tumekwenda kwa utaratibu, na kesho tunategemea kumaliza wachangiaji wawili na baadae kumuomba Mtoa hoja aweze kusema aliyonayo, wachangiaji nilionao ni wawili.

Waheshimiwa Wajumbe kuna matangazo mawili, nimeombwa na ofisi yetu niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba, kuna zile fomu za dodoso au dadisi ambazo ni kuhusiana na mradi wetu wa programu mbali mbali na *UNDP* zinatakiwa ili kuweza kufanya tathmini ili tuweze kuendelea kufanya kazi pamoja na *UNDP*. Kwa hivyo kesho Mwenyezi Mungu akipenda asubuhi turejeshe fomu, na tunategemea itakuwa zimeshajazwa. Hilo la kwanza.

Tangazo la pili ni tangazo la msiba, tangazo la msiba nimeombwa na familia ya Brg. Gen. Mwakanjuki pamoja na taarifa ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, nikuelezeni kwamba mwenzetu aliyekuwa Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala Bora Brg. Gen. Mwakanjuki amefariki dunia leo saa saba mchana katika Hospitali ya Lugalo Dar es Salaam. Matayarisho ya kuleta maiti hapa Zanzibar yanafanywa, hatujapata taarifa kutoka kwa wanafamilia kwamba maiti atafikishwa saa ngapi hapa, na bila shaka tena baadae na matayarisho ya mazishi, tutapeana taarifa hapo baadae.

Kwa hivyo, naomba nikupeni taarifa hiyo kama nilivyoombwa na wanafamilia, ndugu John Mwakanjuki ndiye aliyetuma taarifa hiyo nikupeni Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kuwa Mheshimiwa mwenzetu huyu alikuwa ni mfanyakazi wa wizara hiyo.

Basi baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nichukue nafasi hii na kuakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 20/04/2012 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 20/04/2012 saa 3:00 asubuhi)